# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## Verbatim Report Of

## DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL,

## MALINDI CONSTITUENCY

## HELD AT CLEOPATRA CINEMA HALL

ON

11TH OCTOBER 2002

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, MALINDI CONSTITUENCY, HELD AT CLEOPATRA CINEMA HALL, ON 11TH OCTOBER 2002**

**Present**

Com. Dr. Mohammed Swazuri

**Secretariat Staff in Attendance**

1. Noor Awadh - Ass. Programme Officer
2. Lydia Moraa - Verbatim Recorder

The meeting started at 9.37 am with a prayer from Mr. Shee Abdalla Shee.

**Mr. Shee:……** Mwenyezi Mungu ajalie tangamano hili litoe mazao mazuri yenye kuongoza umma huu uelekee katika njia ya haki na njia sawa kuwe na mapenzi na mahaba, kuwe na uungamano wa kutoa natija na kuwe na furaha ya kudumu katika ulimwengu huu na ahera. (………Inaudible).

**Com. Swazuri:** Karibuni katika kikao hiki cha leo. Mimi naitwa Mohammed Swazuri ni mmoja wa wale wanatume. Niko na wenzangu hapa Noor Awadh na Lydiah Moraa. Sisi ndio tumekuja leo hii kujumuika nanyi. Halafu kuna District Co-ordinator ambaye amefuata microphone nzuri. Halafu na nakala zaidi za ile Katiba. Kuna wengine ambao wako na nakala zao, kuna

wengine hawana. Kuna wengine kwa bahati nzuri wamepata, lakini wameenda. Sasa hizi leo tumezileta ili mje nazo hapa watu wajadili, sisi kuchukua na kwenda kuweka. Baadaye mtazitumia nyumbani lakini tunataka watu wazisome, waziangalie, tutawasaidia kwenda through ili tujadiliane. Tumeanza mapema, sheria imetuambia tuanze kikao saa nne, vile ilivyotangazwa lakini kwa sababu ya leo tumeiweka siku ya Ijumaa na hapa Waisilamu wana haki zao, kwa hivyo tunataka kuanza mapema ikifika saa sita na nusu tuwe tumemaliza watu waende wakafanye ibada zao. Kwa hivyo ikiwa kuna wale watu ambao hawajapata ile copy ya Draft tuko na kidogo hapa, hao wasichana wataenda round wawapatie na mkae pale pale mlipo, tafadhalini. Itakuwa si vizuri kuanza kipigana tena kwa sababu ya hii Katiba. Na copy nyingi pia zimefuatwa, kwa hivyo mtu asikute kwamba tumewaonea au tumewanyima. Make hapo hapo, ambaye hana lakini si kwamba uchukue ya pili ukapatie mtu mwingine ambaye hakuja, ambaye hana. Yule ambaye hana tu ndiye umpatie.

Haya naona tutaanza tuendelee kwa sababu hivi vipaza sauti bado vina shida.
Madhumuni ya sisi kuja hapa leo hii na ni hadhara ambazo zinaendelea Kenya nzima, ni kwamba tuliahidi tutachukua maoni yenu. Tutaenda twandike ripoti halafu tuwaletee. Watu wengi siku zile pale Social hall walikuwa wakisema hatuamini kwamba mtaenda na mrudi mtuletee kwa sababu ya uzoefu ule uliofanyika pale nyuma. Lakini tumekuja tumewaletea ile ripoti ya yale maoni yenu. Kwa hivyo lengo la leo ni kuwazungumzia yale mambo ambayo yako hapo ndani na nyinyi wenyewe msome ambao wanajua kusoma ambao pengine hawajaisoma tutawaeleza kwa ufupi halafu mchangie Katika kufanya marekebisho zaidi ikiwa yapo. Ikiwa mnakuta ni sawa mseme, ikiwa kuna vitu ambavyo havikutiwa ndani mweleze mradi tukimaliza hapa tuwe tumeweka msingi wa kwamba tutaandika ile Katiba tuitakayo. Hayo ndiyo madhumuni.

Kwa hivyo nitawasomea kwa kifupi nitawaeleza mambo gani tumefanya halafu fursa kubwa itakuwa ni yenu wananchi kueleza vile mnavyotaka. Na baada ya kukusanya maoni haya mara ya pili tutakwenda kuandika tena, tufanye marekebisho ambayo mtasema, halafu tukimaliza hapo tutakuwa na kikao cha kitaifa cha Katiba kama tu nilivyosema kulingana na sheria.

Na kikao hichi tumependekeza kianze tarehe ishirini na nane mwisho wa mwezi huu, kwa mwezi mzima. Pale kwa wakilishi wenu wa kutoka wilayani watatu washachaguliwa. Bwana Kingi, wameshachaguliwa? Walishachaguliwa. Watu watatu walichaguliwa ambao watawaakilisha. Wabunge wenu watakuweko na makundi ya dini kuna waakilishi. Tulisema ni watu mia sita na hamsini, watakuwa Nairobi, Bomas of Kenya kuanzia tarehe ishirini na nane. Hao nao watakaa kama hivi na watapitia huu mswada kurasa baada ya kurasa wa jadiliane hii ni sawa, ndio imepita haya kipengo cha pili. Waende hivo, hiyo haifai tubadilishe hapa, tumekubali mpaka wamalize kitabu kizima. Wakimaliza hapo ndio inaenda Bunge inapitishwa kwamba ni Katiba mpya. Kwa hivyo sisi tuko katika zile stages ambazo tuliwaeleza kulingana na sheria.

Kitu cha kwanza nitafanya ni kuwaeleza mambo ambayo ni mapya katika hii Katiba ambayo katika Katiba ya zamani, na ya zamani ni ile ambayo tunaitumia sasa, mambo yale hayammo. Hizo ni highlights ya mambo ambayo ni mapya, hayamo katika hii Katiba ya sasa. Tunapendekeza yawemo katika Katiba ijayo. Halafu baadaye tutaenda kifungu kwa kifungu tuwaeleze vile ambavyo tumependekeza.

Kitu cha kwanza kipya ni kwamba, Katiba hii ni ya wananchi imetengenezwa kupitia kwa maoni ya wananchi si Katiba ambayo imetengenezwa na kikundi fulani cha watu au wataalamu fulani. Wale wataalamu sisi tuliweka pale ilikuwa ni njia ya kukusanya, lakini Katiba hii imetengenezwa na wananchi na kwa sababu hiyo maadili yake mengi hapa ukisoma utakuta bado yarudisha mamlaka kwa mwananchi. Atakaye tengeneza Katiba ni mwananchi, atakaye ilinda tumesema sasa ni mwananchi na atakaye iladilisha tena tumesema ni mwananchi. Kuanzia sasa Katiba ikipitiishwa hii itakuwa ni wananchi wanarekebisha sio Bunge peke yake. Hilo ni jambo ambalo ni jipya maanake Katika Katiba ya sasa Wabunge ndio hurekebisha Katiba.

Jambo jingine tumetumia lugha ambayo wale wanafahamu kiingereza tumetumia lugha ambayo ni rahisi, sio lugha ile ya kisheria. Yale maneno ya kilatini, ya kiitaliano, yale ya kisheria tumejaribu kuyapunguuza inavyowezekana na kunapo kufika mwisho tutaiondoa kabisa lugha geni na kutumia lugha ya kitaifa.

Halafu pia Katiba hii itaandikwa kwa Kiswahili, nafikiri mpaka sasa wameshamaliza wale tuliowaacha Nairobi, wakifanya tafsiri. Hii iliyotoka ni ya kiingereza lakini kuna wataalamu ambao wanatafsiri Kiswahili na ile nakala pia tutalieta. Katiba ya sasa officially iliandikwa kwa lugha ya kiingereza peke yake.

Halafu Katiba hii ina utangulizi preamble ambapo Katiba ya zamani ilikuwa haina. Katika utangulizi ule mtaona inataja maadili ya taifa la Kenya.

Neno jingine jipya ni kwamba maswala ya human rights, haki za binaadamu, haki za kimsingi sasa zimetajwa peupe. Zimetajwa ni nani atakaye zitoa, ni nani atakaye zitekeleza, zimetajwa mtu asipozifuata adhabu yake ni nini, kinyume na ile hali iliyoko sasa. Na hizi haki za kimsingi ziko kitabu kizima. Zimeandikwa sasa kitabu kizima kinatingatia haki za kimsingi.

Jambo jipya katika Katiba hii ni tumeondoa ubaguzi wa aina yoyote. Wananchi wa Kenya hawatakiwi kubaguliwa au kubaguana. Discrimination of any type, kama ni ya kidini, kikabila, kirangi ya mwili, kieneo, aina yoyote ya discrimination, tumesema wananchi wote wako sawa mbele ya Katiba ya Kenya. No one is above the law.

Jambo jingine jipya tumesema kwamba Bunge sasa litakuwa na Nyumba mbili, kutakuwa na Bunge la wale Wabunge wa kawaida tuliowachagua mia mbili na kumi na tutaawaongezea wengine. Tumependekeza wengine tisaini kulingana na vyama. Halafu kutakuwa na Bunge la pili- Upper House- Bunge la waakilishi ambao watatoka kila wilaya. Kila wilaya itakuwa na mwaakilishi mmoja watakuwa kule. Hii ni kinyume na Katiba ya sasa ambayo iko na Bunge moja. Madhumuni yake ni ile mlitaka checks and balance. Hawa wakifanya wale wanaangalia, wale wakipendekeza hawa wanaaangalia. Mmoja asifanye maneno zaidi ya yule mwingi.

Pia jambo jipya jingine tumesema kwamba nguvu za Rais, nguvu za ofisi ya Rais ambao wananchi wengi walilalamika kwamba

ofisi ya Rais iko na nguvu nyingi, tumezipunguza. Tena tukaandika haswa hususan kazi za Rais ni nini. Tumeziandika kabisa kazi ya Rais ya kwanza ni hii, ya pili ni hii, ya tatu ni hii, hawezi kufanya hivi, hawezi kufanya hivyo. Makamu wa Rais wake pia tumemwandikia kazi zake ambazo anapaswa kufanya. Halafu kazi zile tukazipunguza tukazigawanya tukaweka ofisi ya Waziri Mkuu.

Waziri Mkuu huyu atachaguliwa na kile chama ambacho kina Wabunge wengi katika Lower House. Waziri mkuu huyu atakuwa na manaibu wa mawaziri wawili. Waziri Mkuu huyu ndiye atakuwa mkuu wa Cabinet na yeye ndiye atakuwa akiendesha shughuli za serikali katika Bunge. Kazi zake pia tumeziangika. Mtu huyu pia atateuliwa na Rais lakiini atapitishwa na Bunge. Bunge likikataa haiwezekani. Pia tumesema kwamba katika Katiba hii waziri mkuu au Rais anaweza kushtakiwa. Anaweza kushtakiwa ikiwa amefanya makosa katika kazi yake. Na anaweza kuondolewa katika kazi yake. Pia hapo tumesema Rais ili kuchaguliwa ni lazima awe amepata kura asilimia hamsini au zaidi na apate asilimia shirini katika mikoa nusu, zaidi ya nusu ya mikoa ya Kenya.

Halafu tukasema umri wa Rais ni miaka thelathini na tano mpaka miaka sabini. Hapo ndio mwisho. Na atatawala pasipozidi kipindi cha miaka kumi, miaka mitano mitano mara mbili.

Tumesema Wabunge wale wa Bunge lile la kawaida watakuwa na umri wa miaka ishirini na moja mpaka sabini. Lakini Wabunge wa Upper House watakuwa lazima wawe na miaka thelathini na tano na zaidi maanake wale tunataka wawe kidogo wamekomaa kwa umri.

Halafu tukasema katika Katiba ya sasa vyama vya kisiasa sasa tumeandika kazi zao ni nini, sio kupigania kura tu wakimaliza wanaingia gizani. Sasa tumeandika kazi ya vyama vya siasa. Chama chako kama hakifanyi kazi kitatolewa au hakisajiliwi. Kuna kazi maalum tumewapatia. Halafu vitakuwa vikisajiliwa ni Electoral Commission, sio Registrar of Societies tena. Electoral Commission ndio ambayo itasajili vyama hivi. Halafu vyama hatukuweka namba kama mlivyosema. Tumesema watu waunde vyama vyao kama wanavyotaka maanake katika human Rights tumetoa freedom of Association. Lakini tumeweka vikwazo vingi ambavyo si kweli kwamba vyama, vitakuwa ishirini au kumi na tano. Tumeweka vikwazo vingi sana na nitaeleza hivyo vikwazo. Halafu vyama vikiwa viko sawasawa vitapata pesa za serikali kuendesha shughuli zao.

Halafu tukasema kwamba si lazima uwe mwanachama wa chama Fulani ndio ugombee kiti cha uBunge, udiwani au cha urais. Independent candidates wanaweza kusimama kibinafsi. Hiyo ni tofauti kubwa tumeiweka. Halafu tukasema viongozi wa kuchaguliwa na umma kama hawafanyi kazi wanatolewa. Tumeweka hiyo kama diwani hafanyi kazi, kama mbunge hafanyi kazi vizuri basi kuna ruhusa ya kumtoa kabla wakati wake kafika. Tumesema pia Wabunge hawataamua mishahara yao. Wananchi walilalamika kwamba Wabunge wajiongeza marupurupu na wananchi hawana pesa, uchumi uko chini. Kwa hivyo tumeandika hapo kwamba mishahara ya Wabunge sasa itaangaliwa na Commission. Tumeweka commission – Salaries and Remuneration Commission. Wanachama wake pia ni wananchi wa kawaida watatu watakuwa hapo.

Halafu viongozi wote wa umma, viongozi wa mashirika tumeweka leadership code. Mswada au mwafaka ambao watafuata katika kazi zao ni wakikosea hapo wananchi wana haki ya kulalamika na kumwondoa.

Pia tukasema mawaziri hawatakuwa Wabunge. Kulikuwa na malalamiko kwamba mawaziri walikuwa Wabunge aidha wanufaishe sehemu zao wanazotoka au waziharibu kabisa maanake hawana time wanaangalia mambo ya nchi. Kwa hivyo tumesema atakaye kuwa mbunge awe mbunge, atakayekuwa waziri awe waziri. Atachaguliwa na atateuiliwa na Bunge ndio watapigania kiti kile, ndio wata-approve mtu awe waziri. Tumesema lazima wawe professionals katika zile wizara zao. Hatutaki mtu aliyesoma ualimu awe ndiye waziri wa afya. Kwa hivyo tumesema kama ni waziri wa elimu awe alikuwa mwalimu zamani. Kama ni waziri wa kilimo basi amefanya mambo ya Egerton huko.

Halafu tukasema pia jambo jingine jipya, ile serikali ya Unitary State tumeiondoa nguvu zake sasa kutakuwa na serikali ya kijiji, kutakuwa na serikali ya location, tutakuwa na serikali ya wilaya na tutakuwa na serikali ya majimbo. Kwa hivyo tumeweka ngazi hizo nne na ya tano itakuwa ya wananchi. Kwa kulingana na hivyo, tumeondoa provincial administration.

Halafu upande wa mahakama, wananchi walilalamika kwamba ukifanya rufaa katika mahakama ya High Court, uamuzi unatolewa hujui uende wapi tena, sasa tumeweka Supreme Court ili wananchi wanaweza kulalamika zaidi pale. Halaru tukasema majudge sasa watakuwa wanastaaafu wanapofikia miaka sitini na tano badala ya sabini na nne. Halafu mahakama za Kadhi, kwanza makadhi tunawaongeza watakuwa ni thelathini katika Kenya nzima, wale wa Districts, halafu tunasema kutakuwa na Provincial Kadhi, halafu tumesema ofisi ya Kadhi itakuwa na Appeal Court ya Kadhi halafu tumesema kwamba Chief Kadhi atachaguliwa na Judicial Service Commission, kupitia kwa waislamu wenyewe.

Halafu tumesema kuna tume tumeiunda ambayo ni tume ya kusikiliza malalamiko ya wananchi, ni tume ya kuwashataki wafanya kazi wa umma ambao wamewakosea: Kama polisi, administrators, tumeiweka tume hiyo ili kama umekuta haki yako imekiukwa huwezi tena kudhulumiwa unaenda kwa hii ofisi ambayo itakuwa na branches katika kila wilaya. Kulingana na hiyo pia tumetoa administration police kwa sababu walikuwa wanaambatana na provincial administration. Kwa hivyo sasa hao watawekwa kwa regular police.

Police force ni moja. Pia tukasema kwamba polisi sasa tunabadilisha jina lile lao la police force tunawaita Kenya Police Service. Sasa kwenye Katiba ile ya siku hizi iko kwenye Office of the President. Sasa ni office independent iko kwenye Katiba na askari watafundishwa masomo ya kiprofession, Public relations, jinsi ya kushika watu, jinsi ya kuhudumia watu vizuri. Tumeziandika sasa kazi zao, ni nini kazi za polisi.

Halafu upande wa ardhi, tumesema kwamba kwanza tumeunda Tume ya ardhi- National Lands Commission, ku-replace Commissioner of Lands kwa sababu kunasemekana kuna madhambi mengi sana kule. Watu hupata title deeds watu watatu ploti moja, watu hupewa title deeds kutoka kule wakija wafukuza watu hapa na kadhalika. Kwa hivyo tunaondoa hiyo ofisi

tunaweka National Lands Commission ambayo itakuwa na branches kwa kila district ikiwezekana kila location. Tumesema ardhi tumezigawanya mara tatu; kumiliki ardhi, ardhi ya umma, public land tunaiandika ni ipi. Kuna ardhi ya Private land tunaiandika ni ipi, halafu kuna ardhi ya wananchi; community land. Trust land tunaiondoa tunarudisha kwa wananchi. Nyinyi wenyewe ndio mtaamua mtaimiliki vipi ile ardhi.

Halafu upande wa mazingira tunaweka sheria ngumu pale ili tulinde mazingira maanake Kenya inalaumiwa kwamba ni nchi ambayo ni moja kati ya zile nchi kumi bora kwa kuharibu mazingira, misitu, ardhi na kadhalika. Tumeweka pale Commission ya mambo ya mazingara.

Upande wa kura tukirudi nyuma nilikuwa nimeruka hapo tumesema kwamba kura zitakuwa niza siri. Hakuna kura ya mlolongo. Kura zitakuwa ni za siri kwa sababu katika serikali za majimbo na za wilaya zile serikali zinafanya kazi mbili – elective jobs na administrative jobs. Sasa administrative ni utawala. Ukijua kwamba fulani hakukupigia halafu amekuja kwa kesi mbele yako utashindwa kumwadhibu vizuri. Kwa hivyo tumesema usijue ni nani aliyekuchagua ukawa District Governor ili kufanya kazi yako iwe rahisi. Kura zote ni za siri. Halafu kura zitapigwa kwenye madebe transparent. Yale ambayo yanaonekana. Kuhesabiwa kwa kura ni pale kwenye kituo kile kile kitakochopigiwa kura. Kwa hivyo kwa ufupi hayo ndio mambo ambayo wananchi waliyataka na ni mambo ambayo ni mageni katika Katiba ukilinganisha Katiba ile ya sasa na hii ambayo tunaipendekeza.

Pia ukiangalia katika sura ya pili tumeandika mipaka ya Kenya, sasa tumeitia katika Katiba. Zile beacons, vile vikingi vya Kenya kuanzia kiunga mpaka Marsabit mpaka wapi, ile mipaka ya Kenya pia tumeitia katika Katiba.

Halafu tukasema sasa lugha ya kitaifa ni Kiswahili. Ingawaje official languages zitakuwa zote mbili – English na Kiswahili lakini lugha ya taifa la Kenya sasa ni Kiswahili.

Halafu upande wa sikukuu za kitaifa, tumebakisha tatu, Madaraka Day, jamhuri Day na Ile siku ambayo Katiba yetu itapitishwa tunataka iwe sikukuu ya kila mwaka. Hizo nyingine haziko.

Halafu katika Katiba hii tumependekeza pia jukumu la mwananchi, sio jukumu la serikali saa yote, serikali itafanya, serikali inatakikana, serikali infanya hivi. Tulisema pia wananchi wenyewe pia wawe na majukumu yao. Kwa hivyo ukiangalia section 15 inaeleza wananchi kwamba ni lazima wailinde Katiba yao, ni lazima wawe wanafuata sheria, ni lazima wakubali kukosoana, mambo yao wayafanye kwa open, mambo yao yawe transparent. Tumesema wafanye democrasia, na wawe ni wananchi huru. Tumeandika pale.

Upande wa uraia tumesema kwanza in lazima kila mwananchi wa Kenya anayetaka apatiwe passport. Hiyo tumeandika. Nafikiri ilikuwa tatizo kubwa tulipokuja hapa watu wakaeleza haswa waislamu walisema kwamba wanabaguliwa, huwezi

kupata passport na kadharika. Sasa tumeandika kuwa ni jukumu. Sio priviledge tena au favour. Ni right ambayo ni lazima upewe ukitaka; na tumeweka Citizen Registration Board ambayo itakuwa na matawi kila mahali kuhakikisha kwamba haya yanapatikana.

Halafu katika neno jipya hapo tumeongeza tukasema wale wanotaka kuwa na uraia mara mbili , sasa wanaweza kuwa. Dual citizenship tumeiweka ingawaje tumeiweka na vikwazo. Ukikosea, ukikiluka kikwazo hicho basi automatically unakuwa si mwanachi wa Kenya.

Upande wa haki za kimsingi na kibinadamu, hizo, nimesema ndizo nyingi kushinda mambo yote. Tunaweka haki ya kuishi tukasema kwa sababu hiyo tukajadiliana tukakubali kwamba death penalty, kuuawa kwa sababu ya makosa tumesema kwamba iwe sasa ni life sentense. Tukasema kwamba equality, ni lazima kila mtu yuko equal. Tukasema kwamba haki zote za kimsingi zizingatiwe zisidhuru wengine. Tukasema kwamba kina mama wanahaki zilizosawa na kina baba. Kulingana na mila na desturi za dini tukasema kuna haki za wazee- wazee wamelalamika kwamba wakifika miaka hamsini na mitano watoto hawawapi heshima, wanabaguliwa, wakichaguliwa katika kazi nyengine watu wanasema huyo ameiimaliza miaka yake hiyo, mzee aende akapumzike. Tumeandika haki za wazee. Hata wale ni wananchi wa Kenya. Watoto ndio ambao wana haki nyingi zaidi tumewapatia. Lakini ya muhimu kabisa ni kwamba watoto wote wanatakikana wapatiwe elimu ya bure. Elimu ya kutoka pre-nursery mpaka primary school ni bure, na ni lazima. Na tukaandika ni nani atakaye hakikisha inapatikana. Na mtoto yeyote akishikwa au kama amefanya makosa ya kwambo apelekwe kotini, serikali lazima impatie wakili.

Halafu tumeweka pia haki za wale wenye vilema tofauti tofauti kuangalia kwamba elimu yao, maji yao, maisha yao yanakuwa sawa, wanapatiwa haki sawasawa na watu wengine ikiwa wanaqualify.

Security – hapo tumesema kwamba serikali ni lazima ihakikishe kwamba wananchi wake wako secure; tuko na usalama katika taifa. Ndio maana tukaunda National Security Council ambayo itakuwa na watu karibu ishirini na mmoja ambao nitataja hapo.

Halafu tunaondoa habari ya utumwa utumwa. Watu wengine walalamika sehemu nyingine za Kenya kwamba ukiangalia indirectly kuna utumwa fulani vile. Slavery, servitude. Yaani kufanyishwa kazi ambazo hawazitaki sasa ni kinyume cha sheria.

Freedom of religion, uhuru wa kuabudu tumeutoa lakini tumeweka pia mikakati sio kwamba ufanye vile unavyotaka lakini tumesema ukifanya ibada yako isiwe inaadhiri maadili ya yule mwenzako, jirani yako pale, na mtu asiruhusiwe kuadhibiwa. Asiadhibiwe kwa sababu ile siku ambayo anatakikana kupumzika ni siku ya dini yake basi akafutwa kazi. Kwa mfano watu wa Islamu Ijumaa wakitaka baada ya saa tano unusu, wakisema wanaenda msikitini huwezi kumwambia nenda lakini utakiona baadaye. Kama mtu hafanyi kazi Jumamosi wakati wa sabato, sasa ni free hawaendi. Wakristo Jumapili ni free hawaendi.

Halafu haki ya kujieleza, freedom of expression nimeandika pale. Halafu tumesema haki ya mwananchi kupata information kutoka kwa serikali. Access to official information. Sasa itakuwa si favour kwamba mtu anafichaficha. We nenda utakuja kesho ama hakuna haijafika. Lazima sasa. Mwananchi akipenda information on ofisi ya serikali sasa ni lazima apatiwe.

Freedom of Association nimeeleza pale una haki ya kujiunga na mtu yeyote na kufanya mikutano, demonstrations, unakubaliwa haki za kisiasa nimetaja pale. Unaweza kujiunga kwenye chama cha siasa au ukatae uwe independent ni sawa. Mtu anaweza kuishi mahali popote anapotaka, unaweza kutembea Kenya hii.

Tumeweka pia hali ya wale refugees kuiingana na sheria ya kimataifa, wakimbizi wa kisiasa. Harafu tukatoa pia haki za kimsingi za umilikaji wa mali, property tukasema pia kina mama wana haki ya kupata mali kulingana na dini yao, kulingana na mila yao, wawe wasiwe wanabaguliwa kwamba wanawake hawawezi kuridhi.

Upande wa wafanyikazi tumesema ni lazima wapewe mishahara ya kutosha, tumeandika pale, wafanye kazi katika mazingira mazuri, pia wawe na haki ya kugoma, na kujiunga na vyama vya wafanyi kazi.

Fair administration, section 65. Wananchi wanalalamika kuwa wanaamrishwa kufanya mambo ambayo si kisheria. Sasa tumeandika katika section 66 kila mtu anaweza kukataa akifikiria kila kichunga ile mambo anayoambiwa afanye si ya kisheria ana haki ya kukataa kusema mimi sifanyi basi nipeleke unapokwenda. Ikaandikwa section 66 hapo.

Halafu tukasema mahakama ziwe zinapatikana karibu na wananchi, kwa sababu yale mambo wananchi walisema kwamba unasafiri mwendo mrefu ndio upelekwe kortini halafu kesi zinachukua miaka na mikaka haziishi ni kutoa starehe tu. Sasa tumesema kesi ni lazima zisikilizwe katika muda fulani.

Rights za wale ambao wameshikwa au wameshukiwa. Tumeandika hapa kwamba rights za wale miwa sababu wananchi walalamika prisons zetu, jela zetu ni sawasawa na kifo. Sasa tumeandika pale wananchi hawawezi kushikwa hivi hivi mpaka askari aonyeshe mambo yake. Wananchi hawawezi kushikwa kinyama, kushikwa hapo umeshikwa hapa, “twende, twende” Hiyo sasa haiwezekani. Na tukasema mtu aliye rumande awekwe tofauti na mtu ambaye amesha hukumiwa, Si sawa kuwaweka katika cell moja. Halafu kukasema yeyote kati ya hawa aliyerumande, au aliye ndani kabisa lazima wapate mazingira ya kibinadamu. Decent clothing, nguo nzuri, malazi mazuri, chakula kizuri, afya na choo na kama hakuna daktari yeye mwenyewe kama aweza kulipia daktari wake aruhusiwe daktari aje amtibu. Na kama ana dini yake anataka kufuata asikatazwe maanake ni mfungwa. Kama ni Muislamu wa swala tano ikifika adhuhuri mfungwa anaachwa kwenda kuswali. Ikifika alasiri anahaki ya kwenda kuswali kama ni Mkristo jumapili lazima aende kanisani. Halafu haki nyingine nyingi nimesema tumezitaja hapa mtaziona wale walio na kitabu mtasoma.

Halafu tukija upande wa kura nafikiri nimeeleza kwamba Electoral Commission pia tumeipatia kazi ya kuangalia mipaka ya hizi

sehemu za wakilishi Bungeni. Electoral Commission twaipatia kazi hiyo, kazi zake tumeziandika katika section themanini na nne, katika vyama tukaandika kazi zao katika section 88. Tukatoa sifa za vyama, requirements. Halafu upande wa uchaguzi wa vyama ni lazima usimamiwe na Electoral Commission na independent body kwa sababu wananchi wa vyama vingi wanalalamika wachaguzi hufanya kiholela, wengine wakatolewa wengine wakawekwa. Sasa uchaguzi sio wao wenyewe tu, ni lazima Electoral Commission itahusika katika uchaguzi wa chama chochote.

Bunge kama vile nilivyoeleza, tumetoa sasa kazi za Wabunge, katika section 102. Zimeandikwa sasa. Na ni full time job, sio ile ya kwenda siku mbili siku tatu anarudi. Sasa tunawekea ni full time job kama mlivyotaka. Halafu Bunge kazi yake kubwa ambayo tunaiongeza kwa sasa ni kwamba hakuna mtu, kiongozi mtumishi wa umma atakaye teuliwa na Rais peke yake. Hakuna. Ni lazima Wabunge wajadili, wakubaliane ndio wamwandike kazi. Tume hizi za ardhi, tume kama hizi zetu, tume za, wote wale mkubwa wa KPA, mkubwa wa wapi, wote kwanza waende Bunge wajadiliwe ndio wapitishe. Sio mtu mmoja kuchagua wala kufuta. Hata kufuta pia ni Bunge. Kama amefanya makosa mfanya kazi yule, Rais atasema fulani yule nataka afutwe, apeleke Bunge akatoe sababu zake, aki-convince wale Wabunge ndio watasema eeh mtoe. Lakini si hivi hivi.

Bunge pia lita appoint majudge, sio ofisi moja. Halafu kama nilivyoeleza Wabunge wanaweza wakatolewa ikiwa hawafanyikazi zao. Kazi zao zimeandikwa kwa hivyo mkiona hafanyi, taratibu ya kumtoa imeandikwa katika section 112; barua itaenda kwa Speaker, wale watu wa thalathini kwa mia ya wale waliomchagua wakitia sahihi wanaandika barua kwa speaker halafu yule bwana kiti anapokonywa uchaguzi tena unafanywa.

Halafu tukasema katika kupitisha sheria, wananchi wanalalamika kwamba Wabunge hujadili halafu Rais ndiye anatakikana kuweka kidole ili iwe sheria halafu huwa inachukua muda mrefu. Sasa tumesema kwamba ni siku saba. Kama Wabunge wamejadili mswada na inatakikana kuwa presidential assent ndio iwe sheria, sasa hakuna kuhepahepa. Ni lazima katika siku saba iwe imetiwa sahihi.

Halafu tukaja upande wa Parliament calender. Tumeunda parliamentary service commission na hao ndio wataamua Bunge litaanza lini, Bunge litapumzika lini, namna hiyo. Siyo kwamba iwe ni ofisi moja ndio inaamua. Bunge lenyewe litakaa liseme sisi tutakaa miezi sita, tupumzike wiki mbili, turudi tena miezi mitatu, tupumzike mwezi mmoja, namna hiyo. Halafu kulingana na hapo pia tumetaja tarehe ya uchaguzi. Itakuwa katika Katiba. Tume-suggest kwamba ile jumanne ya kwanza ya kila mwaka ya mwezi wa nane, itakuwa ndiyo siku ya uchaguzi. Huu uchaguzi sio huu tunasema wa sasa maanake uko na shida shida lakini pindi inapopitishwa hii Katiba, ni Jumanne ya kwanza ya kila mwaka, itakuwa ndiyo siku ya uchaguzi. Kwa hivyo itakuwa si siri tena.

Upande wa urais kama nilivyosema, tumechagua Rais na kazi zake tumeziandika, makamu wa Rais ambaye alikuwa hana kazi anazozijua tumempatia kazi zake. Mtu anayetaka kuwa Rais ni lazima awe na miaka 35, ni lazima awe na shahada ya chuo kikuu, na asizidi miaka 70.

Halafu upande wa Waziri Mkuu, huyu ni mbunge ambaye mmoja kati ya Wabunge atachaguliwa pale awe na mawaziri. Wizara ni kumi na tano kwanza. Kumi na tano peke yake. Na mawaziri mmoja mmoja kwa kila wizara. Manaibu wa mawaziri ni kumi na tano mmoja mmoja katika kila wizara.

Upande wa mahakama sasa tumezitaja zile mahakama, subordinate courts; magistrate courts tukaenda mpaka kama nilivyosema Supreme courts na Kadhi Court tunaipatia ile Appeal court na kama nilivyosema majaji watakuwa wakifanya kazi mpaka miaka sitini na tano. Hapo ndio tuna (….inaudible) hapo. Na Chief Kadhi nimeeleza pale tumeandika pale section 202. Kadhi's watakuwa na sifa gani, watasomea elimu ya kisheria na dini tumeandika pale.

Halafu tumeunda Judicial Service Commission. Itakuwa na wanachama kutoka kwa jaji mkuu, atakuweko mama mmoja wa kiislamu, atakuweko mkuu wa sheria, jajaji wa Supreme court mmoja, jaji wa Court of Appeal mmoja, High court Judge mmoja, Chief Kadhi atakaye kaa katika Judicial service commission, mawakimu wawili wa kawaida, na kadhalika, mpaka kutakuwa na watu wa NGO katika Judicial Service Commission. Watu watatu wananchi wa kawaida watakuwepo.

Serikali za kitaifa sasa, Chapter 10 tumesema kwamba madhumuni ya kutawanya kazi katika serikali hizi zote ni kwamba wananchi walilalamika services ziko mbali, huduma zapatikana kwa gharama, kwa hivyo tumeweka serikali za majimbo, za wilaya, za kijiji ndio madhumuni yake hayo. Kwa hivyo sasa itakuwa ni kazi ya serikari zile tulizozitengeneza huduma kwa wananchi. Si lazima tena licence itoke Nairobi au passport itoke Nairobi, zitakuwa zinapatikana somewhere else.

Tukasema kwa kijiji, village government hiyo itakuwa na wanachama sita mpaka kumi kama mtaamua mchague au mwateue ni juu yenu wenyewe, halafu hiyo ndiyo serikali ya kijiji. Halafu wao wataamua wataendesha vipi mambo yao. Pia tumeacha open nyinyi wenyewe mtaamua mtaendesha vipi mambo yenu. Serikali ya location, tumesema itakuwa na wakilishi wawili kutoka kila kijiji, wachaguliwe lakini yule location administrator ambaye ni sawasawa na diwani, councilor atachaguliwa na wananchi wa location nzima, ulio na wananchi wenyewe wasipungue ishirini, wasizidi 30. Tuseme hao ni kama wale macouncillor. Lakini watakuwa na debe lao hao, watachaguliwa na wananchi wenyewe. Mimi nataka kuwa district council member. Watafanya campaign wachaguliwe. Na yule district administrator au district governor pia naye atachaguliwa na wananchi directly.

Halafu sasa serikali ya majimbo itakuweko na hii itakuwa na wale wakilishi wawili wawili wa district council ndio wataunda serikali ya jimbo na itakuwa na governor wake; provincial governor. Na hasa mambo yote mlikuwa mnataka yako hapa. Serikali hizi zimepewa uwezo na kazi zake tumeziandika pale. Kwa hivyo ni nyinyi wenyewe sasa. Uwanja uko kwenu.

Halafu tukaenda upande wa ardhi na tukaeleza vile navyo ardhi tumezigawanya, lakini la muhimu ni kwamba tumesema wananchi pia ambao si wakenya au wananchi wasio raia wa Kenya hawatakua na uwezo wa kumiliki ardhi tena. Wananchi wa Kenya peke yao ndio watapata title deeds. Hao wengine, yao ni lease peke yake. Tena lease ya miaka tisaini na tisa ndio

maximum. Halafu tukasema kwamba lazima tupitishe sheria katika miaka miwili kuanzia Katiba hii ambayo itarahisisha upatikanaji wa stakabadhi za ardhi. Kwa muda mrefu sana haswa mzazi akifariki kupitisha ile ardhi kwa wale watoto huwa inachukua muda mrefu sana. Tumesema lazima ifupishwe.

Tukasema zile kesi za mashamba zote ambazo zilikuweko kutoka ile mikataba ya kina Mazrui, ya kina Lenana, ya nani, ni lazima ichunguzwe iangaliwe, na wenyewe wakipatikana wapatiwe ardhi. Nafikiri watu wa pwani hapo ndio wamefaidika sana, kwa mbao kama hayo.

Tukaja upande wa mazingira nimeeleza tumeweka tume. Kwa upande wa public finance, pesa za umma na makadirio ya pesa, kwanza tumeandika katika Section 244 kwamba hakuna kodi itatozwa mpaka kodi hii either imepitia kwa serikali ya jimbo au ya wilaya lakini mwanzo lazima ikangote kule kwanza, ikubaliwe ndio mwambiwe, "okay, kila matatu shilingi hamsini". Lakini si watu tu waje waseme, "hapa shillingi mia mbili ndio gari yako ianze kazi hapa". Halafu tukasema budget, yale makadirio ya fedha kuwa si siri tena. Kwamba mngoje mpaka tarehe sita Juni ndio mjue sigara zimepandishwa bei. Sasa yatakuwa yanazungumzwa miezi miwili, mitatu kabla na wananchi halafu ndio ipitishwe iwe ni budget.

Central Bank ilikuwa ofisi ambayo haiko katika Katiba.Tumeiweka katika Katiba, na tukaandika kazi zake ni nini, nani aweza kuchaguliwa kuwa Governor wa Central Bank lakini hata huyo atachaguliwa na Bunge. Na tukasema kwamba kazi yao moja ni kutengeneza sarafu za Kenya. Tukasema sarafu ya Kenya isiwe na picha ya kiongozi aliyoko.

Public Service Commission tumeiandika tena tukaipatia kazi zaidi, wale wanao-serve katika Public Service Commission, tumewaandika watakuwa wana-serve miaka kumi. Halafu tukaja upande wa Kenya Police tukabadilisha jina lao- Kenya Police Force, tumeiita Kenya Police Service na watumishi hao ni watumishi wenu sasa. Kazi zao zimeandikwa katika 264. Tukaandika pia kuwa mkuu wa polisi, yule atakayekuwa commissioner wa police pia yeye ana security of tenure sio kwamba mtu aweza kuchaguliwa wakati wowote akafutwa wakati wowote. Huyo ataserve miaka kumi. Kwanza lazima awe graduate, awe na shahada, lakini awe amefanya kazi katika Police force kwa miaka kumi ndio aweze kuchaguliwa kuwa mkuu wa polisi. Prisons, jina hilo linasumbua watu, tumeiita Kenya Correctional services, watu wa kurekebisha tabia. Nao pia tumewaandikia kazi zao pale, kutakuwa na commissioner.

Halafu pia majeshi tumeyaweka kwenye Katiba sasa. Jeshi la angani, ardhini na majini ambapo yako sasa katika ministry of Defence, in the office of the President. Sasa wako na sehemu yao katika Katiba. Katiba imeunda haya majeshi, na itakuwa na wakuu wao kama ambavyo imeandikwa hapa.

Halafu upande wa leadership, uongozi, kama nilivyosema tunaweka ile leadership code. Ni lazima kila kiongozi aeleze mali yake ameipata vipi. Kutoka permanent secretaries mpaka Rais wakati wa kupigania ni lazima ueleze mali yako umeipata vipi. Halafu kuanzia waziri mpaka juu, kuna sehemu hapa ambayo ilikuwa ina-suggest kwamba wasiweze kuweka pesa zao nje. Pesa zao

lazima zikae papa hapa Kenya.

Halafu tumeunda tume nyengine zile zile za sasa tumezirekebisha, nyengine ni mpaya, nyengine atakayechaguliwa katika tume zile. Bunge ndio litachagua, na kufuta, mishahara yao itaangaliwa na commission na kati ya moja ya hizo tume ni commission for Human Rights and Administrative Justice. Hapo ndio tunapata ile tume ya wakina mama, Gender Commission, Human Rights Commission, kuna People's Protector, yule Ombudsman ambaye ni mtu anaweza kushtaki mtu wa kawaida hata ukitoka tu unaweza kwenda kushtaki. Tumeweka tume hizo hapo. Madhumuni ni kwamba tunataka kuprotect services kwa wananchi. Halafu tumechagua tume ya kuangalia mishahara ya wafanya kazi ya umma, pamoja na Rais, Wabunge, mawaziri na kadhalika.

Swala la mwisho tumeliangalia pale nani anayeweza kubadilisha Katiba ya Kenya. Kwa sasa ni Wabunge, two thirds, thuluthi mbili ndio wanapitisha. Tumesema kwamba Wabunge wataendelea kubadilisha Katiba kwa maswala madogo madogo. Lakini kwa maswala yafuatayo, mpaka kura ya maoni, tena mje mwulizwe ndio wabadilishe: Ikiwa kuna swala la kuhusu ile mipaka ya Kenya inataka kubadilishwa either tupigane na Uganda tuchukue zaidi au tuwapatie ndugu zetu Watanzania kilometer mbili zaidi, hiyo si kazi ya Bunge tena, ni kazi ya wananchi wote wa Kenya, wafanyiwe kura ndio wakubali. Uhuru wa wananchi-sovereignity kujitawala mambo yao. Pia kuna kitengo chochote hapa kinachohusiana na uhuru wako. Wabunge hawana ruhusa kukibadilisha, mpaka warudi kwako tena kwa kura ya maoni. Na hivyo ni vitu vingi. Hapo ni kura hata kama itakuwa ya siri ama ya mlolongo, ni human rights kama kutakuwa na nini. Hayo maswala ni lazima yaje yaulizwe kwako. Freedoom of movement hayabadilishiki tena. Sasa haya mpaka wananchi wenyewe. Kama swala lahusiana na serikali ya majimbo, serikali ya wilaya serikali tulizuziunda halibadilishiki na Wabunge. Ukikumbuka vizuri mwaka sitini na nne Lancaster House ile Katiba ilibadilishwa kule kule na Wabunge tu, majimbo yakaondolewa. Sasa tumesema ikiwa kuna haja ya kubadilisha jinsi serikali inavyoendeshwa sasa ni wananchi kupigwe kura tena Kenya nzima. Pia hawawezi kubadilisha bila wananchi mambo ya uraia-citizenship, haiwezekani.

Kwa hivyo hayo kwa ufupi ndio maswala ambayo tumejadili katika Katiba hii kwa hivyo sasa nitawapatia nafasi ambao wako na maswali kuuliza au kueleza ufafanuzi au kama kuna kitu ambacho hatukukieka pale au hakiko sawa sasa nafasi ni yenu. Ninawashukuru sana kwa kunisikiliza. Ahsanteni. Haya karibuni.

Nitachukua watu kama kumi hivi. Kwanza tuyajibu maswala yale halafu ndio tuchukue wengine namna hiyo. Kwa hivyo msifanye pupa kila mtu atapata nafasi. Haya na kila mtu nitampa namba. Wewe ndio namba one, umesikia, halafu yule wa pale mwisho, namba two, usiangalie nyuma wewe, namba two, haya namba three, namba four, namba five, hapa mwanzo hapa. Haya naenda upande huu. Yule pale namba six, wewe hapa namba seven, huyu hapa namba eight, huyu hapa namba nine, mama namba ten. Kila mtu ashike namba yake nitasema tu namba five. Haya. Nitakuja nimesema hao ni watu kumi wa kwanza. Nitajibu halafu nitakuja kwa watu kumi wa pili. Haya namba one kule mwisho.

**Namba one**: Nauliza katika transition, kuna miaka kadha imewekwa hapa, ambapo hii Katiba itakamilika kabisa. Je katika

muda ule, pengine serikali itakayoingia mmweka mbinu gani ambazo zitahakikisha kwamba hakuna kitu kitakacho badilika, kwa mfano hii provincial administration ambayo itakaa kwa muda kidogo.

**Com. Swazuri:** Watu wale wamepata namba wasongee hapa karibu.

**Mr. Steven:** Jina ni Steven. Swali langu linakuja katika haki za wafungwa. Umetueleza ya kwamba suspects au watu wa rumande wasiweze kupata mateso. Lakini hukufafanua zaidi ya kwamba ni hali gani inayoweza kuwaweka mpaka wakawa katika hali ya usalama katika magereza. Kwa sababu mtu anaweza kuwa suspected miaka miwili na akienda kortini ashinde. Na kule amepata taabu labda miaka ishirini. Nataka utufafanulie basi.

**Mr. Uhuru:** My names are Mr. Uhuru. Mimi nakushukuru Bwana Commissioner lakini nataka kuzungumza kidogo kuhusu chapter 8, part 2 na part 3. Katika draft yenu hii ambayo ni nzuri kabisa, kuna mambo hapa ambayo mimi yameniletea utata. Utata wenyewe Bwana Commissioner na wenzangu ni kuhusu huyu Rais, ambaye hapa amepokonywa madaraka, amegawanyiwa huyu Prime Minister. Kwa maoni yangu mimi nilikuwa nasema hivi. Huyu president, nilikuwa namwomba kama itawezekana awe executive president, awe president ambaye atakuwa hana Prime Minister. Awe na Vice. Ni maoni yangu hayo. Awe executive president ambaye pia atakuwa not above the law. Kwa sababu nasema hivi. Kulingana na population yetu kwa sasa, the majority of us sisi Wakenya wengi hawajafikia nyanja zile ambao wanaweza kuelewa who is the president and who is the Prime Minister. Kwa hivyo mimi kwa maoni yangu, nilikuwa naomba kama hii part 2 number 3 muifanyie marekebisho na tuwe na executive president ambaye atakuwa anaweza kawa impeached.

Swali lingine ni kuhusu mijikenda. Katika hii Katiba kuna watu watatu ambao kuna wenyeji wa Kenya na kuna waislamu na wakristo. Katika hawa kuna makabila mbalimbali hapa Kenya. Kuna mijikenda. Sasa katika hii marital Act ya sasa watu wanaoana kulingana na kimila zao. Lakini kufikia sasa, katika hali ya uchumi mimi mwenyewe nikitembea huku na huku, nakuta wadada au mabwama wanateseka kwa sababu ya mahari. Mahari yao wazee kama vile ulisema katika hii Katiba anything will be deliberated according to the custom, lakini mimi naomba tutiliwe kipengele katika mijikenda tuone, je mimi nikitaka kumuoa mtoto wa fulani nitatoa nini. Kwa hayo machache nashukuru.

**Ms. Khaemba:** Majina yangu naitwa Reginalta Khaemba. Maoni yangu inasema kuhusu mambo ya title deed. Mnasema watu wa Kenya wenyewe ndio peke yao wanapata hii title deed. Nami nauliza swali. Na wale ambao macitizen wamekaa hapa Kenya wanienunua mashamba na wamepewa hiyo matitle deed tutawafukuza au wataendelea kuishi?

Halafu swali lingine; juu ya mambo ya mashamba unasema shamba, kila mtu akiwa katika family lazima apate huo urithi wake. Sasa haswa urithi upande wa watoto, wasichana na vijana, itateketezwa je kwa maana katika mila za kale kwa watu wengine, wasichana hawastahili kuomba kwao. Wanahesabiwa mali mahali wanaenda kuoleka. Sasa itatengenezwa namna gani ili tuelewe vizuri. Sijaelewa pale.

Kitu kingine, mambo ya kupata pesa za kupeleka nje ndio hata uchumi na ukame ni shida za Kenya zile tunaendelea kuzipata juu hakuna pesa. Ni kwa ajili ya watu wale wanapeleka pesa zetu nje zikawekwa huko nje zirudishwe au zibaki kule

.

**Bwana Bawazir:** Mimi jina langu ni Mohammed Bawazir. La kwanza Bwana Commissioner naeza kujua (…inaudible) ya mabenki ambayo yamefilisika, ambayo wengine niwapesa yao, hatupati kitu bwana. Wananchi wa hapa compensation kwa pesa yao. Katiba itueleze. Kitu kingine ni kuhusu baraza la wilaya, mayor, machairmen wa nini watachaguliwa vipi. Kitu cha tatu nataka kujua, hii Katiba mpya itatumika baada ya hii kura (…inaudible) kura ya Bunge likija pia litakuwa ni direct likipitishwa moja kwa moja. Katika huu uchaguzi au Bunge ingine.

Jambo la nne ni kuhusu maswala ya majimbo. Jambo hili latukera sana. Wengi wetu hatuelewi majimbo ni nini. Kwa mfano kama sisi tuna port. Tutajua zile percentage za port zile zitabakia hapa au vipi. Au ni wananchi ambao kama ni sisi wa kwanza katika coast ambao tutapata haki kuliko hao wengine kutoka nje. Asante.

**Com Swazuri:** Namba sita. Jina lako

**Bwana Nyiro:** Ndoro Nyiro. Mimi sina swali, labda litatokea kadri ninavyozungumza lakini ningetaka kuzungumzia kuhusu chapter 10, ambayo inahusu devolution of powers.
Section 2, something, sharing of national resources jinsi ya kushare hizi national resources. Hapa, hebu kidogo, sioni vizuri. Tunaambiwa kwamba, can you help me by reading this. Usome hapa. Sioni vizuri mimi.

**Mzungumzaji:** Inasema hivi…
**Interjection:** (…inaudible)
**Mzungumzaji:** 2.2 (vi) One; districts shall be entitled to a substantial share of the national revenue from local resources and for the allocation of a fixed percentage to the communities in whose areas the resources are generated.

**Bwana Nyiro:** Okay, ningependa kuzungumzia kitu hicho. Nimempatia huyo anisomee kwa kuwa kidogo macho yangu yananitatiza. Alright. Kwa kuwa tulilalamika kwa mda mrefu kwamba mambo mengi yanafanyika at national level bila kujali mtu wa chini, tunashukuru kuwa sasa tumepatiwa nafasi hii kwamba tuwe na uwezo wa kukata shauri kwa mambo yetu wenyewe. Lakini sasa, katika kukata shauri kwa mambo yetu, ikiwa hatutapewa nafasi ya kudecide kuhusu kipato chetu, huwa hakuna uhuru kamili. Itakuwa ni kuchezeana tu. Inafaa, kile kinachotoka katika section yetu tuweze ku-decide. Hapa imesemwa ‘ substantial’. Hii naona mimi haitoshi. Tungekuwa very specific kwamba, kipato kitakachotoka katika kila district, I suggest 50% ya revenue kutoka district hiyo ibaki kwa district hiyo. 25% iende kwa provincial government. 25% iende kwa national government. Bila hivyo, tutakuwa tunachezeana. Maanake…

**Interjection:** Mzee tumeelewa hiyo. Ingine

**Bwana Nyiro:** Najua. Tumekuja kwa shughuli hiyo hapa.

**Interjection:** Sasa umeshaeleza hiyo. Sasa nenda kwa pointi nyengine. Tumeielewa.

**Bwana Nyiro:** Okay. Sawa. Alright. That is my suggestion na sitaendelea zaidi. Ikitokea need, I will come again.

**Com. Swazuri:** Namba saba.

**Bwana Muya:** Mimi kwa majina naitwa Alfred Munguni Muya na hapa nilikuwa nataka kuuliza juu ya mshahara. Kwa sababu mshahara wetu ni wa chini sana na tuna visomo mbalimbali. Wengine hawakusoma kabiza, wengine walikuwa mkate ule ule ananunua mtu yule hakusoma kabisa ndio ananunua mtu yule alisoma, kwa bei moja. Tena, katika hali ya ufanyaji kazi, unakuta ni kama utumwa maanake wewe unafanya kazi, huku yule boss wako akiwa amekutolea macho na kukupigia kelele, hata huna ule uhuru wa kufanya kazi. Yeye hukusimamia kama wewe ni mtumwa. Sijui hiyo mnafikiria vipi.

Pia kwa upande wa labor, ni mambo mengi sana watu wa labor wanapelekewa lakini hakuna kitu wanafanya sana wanalalia kwa matajiri. Wamelalia kwa matajiri, wakipewa pesa kidogo basi inakuwa wewe hata haki yako haiangaliwi. Sijui hiyo mmefikia wapi kulingana na hilo Asante.

**Com. Swazuri:** Namba nane.

**Bwana Migotsi:** Okay. Thankyou. Mimi naitwa Isoe Migotsi. Nina maswala karibu saba hapa. Kitu cha kwanza ni qualification kwa hawa governors. Sijui Constitution kama ime-provide qualification. Ni nani wana-qualify. Upande huu qualification zitatolewa. Ni nani watakuwa hiyo sehemu. Sehemu ingine ni kuhusu makamu wa Rais. Makamu wa Rais atakuwa mbunge au naye pia atakuwa hana constituency kama Rais. Hapo sikuelewa vizuri.

Upande mwingine ni Permanent Secretary na ministers. Tumesema minister ni mtu mwenye ujuzi wa ile kazi amepewa. Na huyu Parmanent secretary naye awe na ujuzi wa hiyo kazi. Mimi nilikuwa naona kwamba, kama waziri atakuwa na ule ujuzi, basi hakuna kazi ya Permanent Secretary kwa sababu yeye ana ujuzi huo. Huenda ikawa ni duplication of duty. Asante.

Ingine ni huku upande wa wanawake- rights za wanawake. Sijasoma hapo. Nilipokuwa nikiangalia draft ulisema kwamba mama atapatiwa mali kulingana na mila, kulingana na dini yake. Sasa, kama itakuwa hivyo, ni kama tumebaki kule kule tulikuwa. Kwa sababu, ni kulingana dini na kulingana na mila ndio wamama walikuwa wanaangaliwa na mila tofauti. Nafikiri angekuwa more specific iseme mama ana haki ya kurithi kama ni mila ama nini lakini ana haki na yeye ya kupata kitu kidogo ya

baba na mama yake.

Upande wa Prime Minister, mlisema Rais akipendekeza mtu akikataliwa mara ya kwanza na Bunge na mwingine akataliwe, ni kama atadissolve hiyo Bunge waende kwa uchaguzi. Will not be very expensive for the government, because it is possible. Tumeona kama kule Amerika kuna mtu alikataliwa mara nyingi sana, ilimpaka wakarudi. Mtu karibu wa nne ndiyo alikubaliwa kuwa Attorney General. Sasa, kama mtu atakataliwa hiyo twende kwa uchaguzi, will it not be very expensive for the government and the citizens? Another thing ni upande wa Prime Minister. Prime Minister naona ni Kama hana limit ya ofisi. Yeye ataweza endelea provided his party inaendelea kushinda. Mimi ningependekeza apewe limit ya hiyo ofisi yake. Upande mwingine ni National council. Hiyo kabisa sikuelewa vile inachaguliwa na ni nani anataka kuchaguliwa kwa Natioanal council. Pengine hapo ningekuomba Bwana Commissioner ufafanue kidogo ili tuweze kuelewa.
Asante.

**Com. Swazuri:** Namba tisa.

**Bwana Mbovo:** Majina yangu naitua Abdalla Mbovo na swali langu la Kwanza ni a Bill to become Law. Umesema kuwa president atalazimishwa na Constitution kuwa after seven days atie sign ile Bill. Na je sasa sielewi kwa sababu huyu Rais ana uwezo na je akikataa itakuwaje, akikataa kuisign hiyo piece. Na nyingine naenda kwa chapter 5. Hizi Bills of Rights tumeona kuwa, wamama, vijana na wazee na watoto wamepewa rights. Lakini vijana, youths hakuna rights zao. Hawako na rights kwa Government offices hawako na guaranteed future in the Constitution, the Constitution pia haiwaguarantee employment na pia hawawi defended kwa misuse na rights documents na pia ingekuwa vizuri youths wawe na ministry yao tofauti. Thanks.

**Bw.Abubakar:** Jina langu ni Abubakar. Kitu cha kwanza ni habari ya utility ya tax money. Utility. Pesa zinazokusanywa za kodi kama mfano hii road levy, inakusanywa kwa sababu ya barabara. Lazima kila mwezi zitolewe returns, tuko na billion ngapi. Halafu hizo zisiende kupewa loan mtu kwenda kutia ng'ombe katika shamba zake. Hizo za barabara zijenge barabara katika kila corner ya Republic.

Kitu chengine ni habari ya indigenisation. Uenyeji. Kuna makabila ambayo hapa pwani yameandikishwa katika uenyeji kwa mnajili ya idadi ya wingi wao- numerical figure. Na kuna makabila mengi ambayo numerical figure yao iko chini na wao ni indigenous wamekuwa omitted. Kwa mafano kuna Wabole katika kipande cha kaskazini cha Lamu ambao ndugu zao katika katikati ya pwani Wasanye na ukienda kusini utakuta kuna Wajomvu, kuna Washerazi katika Mombasa kwenda mpaka Tanzania. Hayo makabila hayakuandikishwa. Kuna Wangozi ambao ni Waswahili na lugha yao. Wana mila zao na desturi yao. Wana maisha yao. Hawakuandikishwa kwa sababu figure zao ni ndogo. Hata hawajulikani katika Kenya. Hata ukienda katika Registration ya makabila kwamba hao wanatambulikaniwa. Ndio mimi napendekeza watu waandikishwe kwa upande wa makabila kulingana na historical entity zao. Wale ambao history inaonyesha wako hapa katika museum unaonyesha kutoka $4^{th}$ – $10^{th}$ centuries. Inaonyesha wao ni indigenous. Wengine wamekuja three four hundred years, na kwa sababu figure yao ni

kubwa, wanapewa more land rights, property rights juu ya wale wengine ambao ni indigenous. Hiyo isiweko. Ime-affect sana Social Economic structure ya indigenous people ambao ni minority katika coastal strip upande wa mashamba.

**Eunice Mkiagawa:** Kwa majina Eunice Mkiagawa. Mimi yangu point moja ni kuchangia upande wa dini. Niliona yale maoni yaliyotolewa kuwa kuna hizi crusades na mijadala. Mimi mwenyekiti ninaomba hivi. Uhuru wa kuabudu tunaukosea na bado hatujaupata. Maanake ukiona kama ni siku ya Ijumaa, ni Jumapili, ni Jumamosi watu wanaenda free. Huo ni uhuru wa kuabudu. Lakini sio ule wa kwenda kuomba licence na kukaa kwenye uwanja wa public na kutoa (…inaudible). Mimi langu nachangia kuwa hizi crusades na majadiliano, mawaidha yawe kama ni Christians, kama wanacrusade wawe wakifanya pale pale ukumbi wa kanisani kwao. Na kama ni Muslims kuna mawaidha fulani wawe wanafanya pale pale kwa Msikiti. Na hii nasema kwa maana tunakosea.

Wakati tunapewa licence, unaona sio tena uhuru wa kuabudu lakini unakuwa ni uchochezi mwingi na matusi na kila kitu ambacho kinaleta chuki na sisi sote ni wa umoja. Hakuna mtu aliyeumbwa na shefani, sote tuliumbwa na Mungu. Kwa hivyo mimi ombi langu ni hilo kuwa kama kuna crusades ama mawaidha yoyote tafadhali yawe yanafanyika kama ni Christians wawe wanafanya kule kule kanisani, kama ni Muslims wawe wanafanya kule kule msikitini sio kwa public. Ahsante.

**Com. Swazuri:** Hayo ndiyo mambo ambayo tunataka kusikiliza kwa sababu tunaamini kwamba hatuko perfect lazima kuna sehemu ambazo hatukuzigusia au watu hawakuridhika. Haya, transitional mechanisms Bwana James ameuliza tumesema kwamba Katiba haiwezi kubadilishwa bila kupitia kwa Bunge au kupitia kwa wananchi. Upande wa hiyo provincial administration tumeweka 90 days kwa sababu hakuwezekani kuwa na vacuum. Maanake wananchi wanazaliwa kila siku, wengine wanakufa kila siku, ni lazima kupatikane birth certificate, death certificate, kuna case watu wanapigana kila siku. Kwa hivyo ni lazima itakuwako ile, lakini wawe kazi yao tumeandika hapa sio kubadili Katiba tena. Kazi yao ni ku-hand over to the next regime. Kwa hivyo si kweli kwamba wakati wa transition wale watabadili Katiba maanake hilo swala la provincial administration ni swala ambalo limehusu sovereignity of the people, ni lazima kura ya maoni.

Steven Ngumbao, wafungwa - suspects sheria zao sikuzisoma zote lakini ni nyingi sana na hapa tumeziandika. Haki za wale ambao wamefungwa, haki za wale washukiwa. Sasa tunawapatia cover kubwa sana hawawezi kudhulumiwa, hawawezi kunyanyaswa, kutukanwa ovyo ovyo. Tumeandika hapa pia kama ni mtu alikuwa anasoma, masomo yake apatiwe muda aendeleze na ni mfungwa. Tumesema kama ni mtu wa kufanya exercise, mtu wa kujogjog, mtu wa kucheza mpira, ni lazima apewe nafasi ile. Hizo ni haki zao tumeziweka kinyume na wakati huu. Ni nyingi sikutaka kuzisoma zote.

Bwana Uhuru amesema kwamba anataka executive president. Kwanza tunataka kumwambia Bwana Uhuru kwamba sababu moja ya kufanya marekebisho ya Katiba ilikuwa ni hiyo. Watu walilalamika kwamba executive powers za president ziko juu sana. Kwa hivyo tufuate sheria iliyotuweka hapa. Ni lazima tuzibadilishe. Ndio maana tumetoa. Sasa ukitwambia turudi kule kule, president awe executive, halafu awe na makamu wa rais hata kama utaandikiwa impeachment. President tumeona akiwa

executive ni kwamba hata judiciary ana-icontrol. Hata Bunge ana-licontrol. Kwa hivyo hata mkitaka kumshtaki ni kazi bure. Haiwezekani. Ndio maana tumeseparate hizi powers sasa. Watu walitaka separation of powers. Tunaenda kwa wingi wa watu waliosema. Mawazo mengi, sikumbuki pahali nilipokaa kusikiliza maoni ya wananchi ambapo hakuna mwananchi aliyesema presidential powers be reduced. Sikumbuki. Watu wote walisema hivyo.

Halafu upande wa mahari tumesema hayo sasa hatuwezi kuandika katika Katiba kwamba watu wasipeane mahari. Sasa hiyo tutakuwa kidogo tumekiuka ile ile freedom of culture, freedom of association, freedom of religion. Sasa basi ni wao wenyewe, tumesema tu kwamba haki za mtu zipatikane. Sio kwamba mtu azuiwe kuoa kwa sababu mzee amesema anataka ng'ombe mia tano. Sasa hiyo itakuwa ni unlawful administration na tumesema you can go against anlawful administration, lakini kuweka kwamba mahari yasiweko au yaweko sasa hiyo ni too much. Na tutakuwa twakanyaga haki za wananchi.

Title deeds, je wale wageni ambao si raia wa Kenya na tayari wameshapatiwa ardhi. Tumesema yeyote ambaye si raiya wa Kenya na yuko na ardhi, title deed sasa tutai-reduce, sio absolute ownership, tutaisema wewe lease yako sasa ni 99 years. Zikiisha basi. Sasa tunajua maana ya lease ni kwamba mwenyewe anampatia mtu fulani atumie kwa muda fulani for a certain amount of money hiyo ndiyo lease. Ngoja basi. Lease ikiisha mali inarudi kwa mwenyewe. Halafu mwenyewe ndiye anaamua anampatia nani. Ndio tunasema hapo kwamba zikiisha hizo title deed zote tutazi-convert tuwaeleze sio absolute ownership. Na ikiisha inarudi kwa Kenya. Sasa Kenya ndiyo itaamua inampatia huyu au yule. Kama ni mgeni ni lease, kama ni mwenyeji ni title.

Mama anaeleza tena habari ya urithi. Tumeambiwa pale kuwa kina mama pia wana haki ya kurithi. Na tumesema kama ni kina mama wasichana hawakuolewa na wako pale pale, tutawapeleka wapi, kwao ni wapi? Kwao ni pale pale. Kwa hivyo tumesema wana haki pia ya kuridhi. Kama ameolewa hiyo ni swala jingine. Huko huko ndio atajua mambo yake. Lakini kama yuko pale pale nyumbani na babake ni wewe, mamake ni wewe sasa utampeleka wapi? Huwezi kumfukuza mtoto wako, ukamwambia nenda uondoke hapa, na kwao ni pale. Hata kwa Waislamu pia, ndio maana tumesema according to mila na dini maanake Waislamu twajua it is sealed. Yao imeshaamuliwa kama hujaolewa, umeolewa haki zako ziko pale pale.

Upande wa bank. Zile bank ambazo zimefilisika - Sasa ni lazima sheria iko. Sisi tumetengeneza sheria ile inakuja lakini hivi sasa hizo ni sheria za sasa.

Mayors na council chairs. Wale walisema kwamba wananchi wanataka kuwachagua. Katika upande wa devolution of powers tulisema Serikali ya location au munispaa itakuwa ni sawa na serikali ya district. Kwa hivyo Governor – ambaye atakuwa ni mayor – atachaguliwa na wananchi.

Revenue ya ports, Bwana mmoja amekuja hapa – Bwana Nyiro – ameeleza na ametusuggestia tugawanye ile mali namna gani. Hilo kweli tutakwenda kuangalia maanake hatukuandika vile viwango. Amesema 50% kwa ile area, 25% kwa province, na

25% kwa national. Hilo kwa kweli ni wazo nzuri ambalo tutaenda kulijadili. Halafu Bwana mmoja akauliza kama hii Katiba hii itatumika kwa huu uchaguzi huu unakuja au ni mpaka baadaye. Maoni yetu kama Tume ni kwamba itumike kwa uchaguzi unaokuja lakini uwezo huo wa kuamua hivyo hauko kwenye Tume. Uko kwa wanasiasa.

Mwangome anasema mishahara tunayoiandika katika kitengo cha Labor Relations; kwamba kila mfanyakazi lazima apate mshahara unaofaa; tumeandika pale fair remuneration. Halafu tukasema kwamba afanye kazi katika mazingira yale yanayofaa kwa kazi. Kama si hivyo unaenda kwa Public Defender unshtaki, na mambo yanaangaliwa. Halafu, upande wa Labor Relations, kwamba kesi za labor zinafanyika hivi hivi; tumesema kwamba, kuna principle moja nimesahau kutaja. Katika Katiba hii sasa tume-outlaw, tumeharamisha hongo. Hongo ya aina yoyote sasa ni haramu. Tena si haramu kwa yule anayetoa. Wote wanaishusika – anayetoa, anayepokea, anayetumia, anaye-encourage, yeyote. Bora msururo huo ukiwemo. Ni kama vile pombe – mgema, mwenye mnazai anayeuza, anayekunywa, anayefaidika na pesa zile, hao wote kundi lao ni hilo hilo. Sasa, tumesema katika corruption na hivyo hivyo. Si yule anayetoa peke yake. Anayepokea, anayetumia, anaye-encourage, wote hao. Tume-outlaw. Na mwananchi akiona yafanyika, aende kwa Public Defenders.

Upande wa qualifications za Governors, hiyo ni kweli. Hilo ni swali ambalo tumeambiwa kila mahali. Tulisahau kuandika. Vice President. Si tulisema si mBunge? Huyu ni running mate. Yaani, yule Rais akizema, “Mimi mwaka huu nitapigania uongozi,….” Sasa atachagua naibu wake ambaye atapigiwa kura pia. Halafu tumekuja upande wa Women’s Rights. Nimeshajibu hiyo. Ni lazima kina mama wawe na haki zao. Tumeshazitaja pale.

Chief mme-suggest kwamba asiweko. Tutakwenda kujadili lakini unakuta ya kwamba PS kuwa aweko kwa sababu wakati wa transition ule; kama mawaziri, Bunge limevunjwa au mawaziri hakuna, lazima kuwepo na mtu pale. Ndio maana lile neno permanent likaja pale. Kuna mtu permanent ambaye ataangalia mambo ya wizara. Kuna Bunge, hakuna, lakini huyu mtu ni lazima awepo. Ukisema aondolewe, kidogo kutakuwa na shida pale.

Amesema kwamba itakuwa ni gharama kufanya uchaguzi kama hawawezi kupata kiongozi mwengine. Kwanza tukubaliane katika principle yetu mambo mawili kuanzia hii Katiba ikipitishwa: Kwanza, mtakuwa mkiitwa mkifanya uchaguzi kila mara. Maana mlitaka wenyewe. Kila kitu sasa ni uchaguzi. Sio ile kuamuliwa tu. Kila kitu ni uchaguzi. Kwa hivyo, kwa vile mlitaka hivyo, muwe tayari. Hilo ni la kwanza. La pili, uchaguzi una gharama. Na demokrasia ina gharama. Nafikiri umeona nchi kama Japan, Italy, Israel, uchaguzi ni kila siku. Waziri Mkuu mara ashatimuliwa, mara Bunge limekosana, mara chama kile kimekosana, mara…. Kwa hivyo muwe tayari. Wakati wowote mambo yatakuwa ni kuulizwa, “Mwasemaje?” Hii ndiyo wananchi walikuwa wanalilia – participatory governance. Mnataka ku-participate katika maamuzi ya nchi yenu. Kwa hivyo, ni lazima muwe mko tayari.

Halafu, Prime Minister mme-suggest tumpatie time limit. Hiyo ni sawa tunakubali tutakwenda kuangalia.

National Council . Lile Bunge la juu tumesema ni watu 100. Sabini watakuwa wanatoka mmoja mmoja kila wilaya. Na huyo atakuwa na debe lake siku ya kura mtachagua mbunge wa district nzima – wilaya nzima – ambaye atakaa kuwakilisha mambo yenu katika Bunge la Upper House. Thelathini, hivyo ni viti vya kina mama. Hawa sabini pia kama mtachagua mama ni shauri yenu. Lakini wale thelathini watakuwa ni lazima wawe ni kina mama. Wanne watatoka kila mkoa. Kila mkoa. Mikoa saba, itakuwa na waakilishi wanne wanne ambao watachaguliwa directly. Watakuwa na debe lao nao. Kama kuna mama hapa ambaye anataka kuwa mBunge wa Pwani kwenye National Council, atajitangaza Pwani nzima, "Mimi mama Eunice napigania, nipigieni kura" Debe lake litaenda Pwani nzima achaguliwe. Halafu, wawili watatoka mkoa wa Nairobi. Hao ni thelathini. Hiyo itakuwa ni mia moja. Wale watakuwa ni Wabunge 100 – National Council.

Halafu Bwana Abdalla amesema kwamba, "Je, Rais akikataa kutia sahini mswada ili uwe sheria katika zile siku saba tumeandika, hiyo ni sababu moja ya kufutwa kazi". Tumeandika hapo. Na akasema kwamba youth rights. Pengine hatukuzitaja, zimo lakini pengine hatukusitaja. Nafikiri tutaenda kuangalia mambo yao. Na ukasema unataka wizara ya youth. Tumesema wizara lazima ziwe kumi na tano. Ziangalie mambo yote ya Kenya. Lakini hatukuzitaja. Kwa hivyo tunaamini lazima itakuwa moja wapo. Abubakar; Returns. Tumeweka serious, strict regulations kwamba kwanza Waziri Mkuu atatakikana kila miezi sita, at least once, aje awaeleze wananchi pesa za serikali zimetumika vipi. Hiyo tumeiandika. It is now a Constitutional requirement. At least once kila miezi sita kutakuwa na address maalum ya Waziri Mkuu kusema tulikusanya shilingi billion tano, tumetumia billion mbili kwa hii, billion moja kwa hii, akiba yetu ni hii au twadaiwa hii. Haya twendeni. Miezi mitatu tena atarudi. Kwa hivyo hiyo ni accountability ya kutosha, ambayo saa hizi hakuna.

Halafu, zile kabila ndogo ndogo – Waboni, Wasanyi – tumesema ya kwamba hatutaki mwananchi wa Kenya abaguliwe. Na tumetaja aina za kubagua, kabila, rangi, alikotoka,historia yake. Tumesema hatutaki kuwabagua. Kwa hivyo siku tutayaandika yale makabila ya Kenya, lazima hao nao watakuwa wameingia.

Halafu Mama Eunice pale akaeleza dini, kwamba Miskiti wale Masheikh waseme mambo yao, wahutubie miskitini na wale mapadre nao wahubirie makanisani pekee sababu watu wanapakana matope. Tumesema kwamba kuna freedom of religion lakini religion ile yako isiwe inadhuru religion ya mwingine. Ikiwa hiyo itatusaidia isidhuru basi, tutaangalia hilo jambo.

Haya sasa wale kumi bora, sasa wengine. Tutaanza na namba moja, mbili, tatu. Tunaenda upande huu. Mama namba nne, kijana namba tano, halafu upande huu sasa. Namba sita, namba saba. Hapo katikati kule nyuma, namba nane namba tisa. Haya hapa katikati namba kumi – mwenye kofia nyekundu. Kila mtu ashike namba yake. Haya karibuni hapa.

**Interjection:** Karibieni, karibieni wale wamepewa namba. Namba moja

**Sheikh Abdalla:** Jina langu Sheikh Abdalla. Swala la kwanza ni kuwa, hii Commission yenu itabakia au ikimalizika kazi hii ndiyo imekwisha. Na ikiwa itabakia, naomba kuwa iwe na kazi nyingine muhimu kuwa itaweza kuendeleza katika kukua hii

Katiba na katika kufahamisha hii Katiba watu kila siku, na katika kusomesha pia. Ku-prepare syllabus katika maskuli na lectures za public. Na waweze kusimamia katika Constitutional Court ikiwa itawesekana.

La pili, ni katika, yule Bwana alipokuja akatoa figures zake za provincial, national and district. Mimi nitapendelea ratio hizo ziwe ni 70 kwa district, 20 kwa province na 10 kwa national. Asante sana.

**Bwana Salim:** Kwa jina naitwa Awadh Salim. Napenda kutoa maoni yangu kuhusu mambo ya taxation. Mambo ya taxation yameleta madhara sana kwa wananchi, maanake zinaumiza. Utakuta mtu amefanya kazi anakatiwa tax. Halafu akienda akinunua vitu pia kuna tax. Sasa hizi tax zimekuwa nyingi mpaka power, water, unalipa VAT. Kwa hivyo unakuta mtu ule mshahara ambao anaupata wote unaisha kwa matax.

Pili, ningetaka kuzungumzizia habari ya rights za uraia. Utakuta mtu anaenda ku-apply for birth certificate na yeye ni Mkenya. Halafu katika ile pass pale chini unaambiwa kwamba "hii pass haimaanishi kwamba wewe ni raia wa Kenya" Na mtu wewe umezaliwa hapa, wazazi wako wako hapa. Kwa hivyo inamaanisha ile pass yenyewe haifai kabisa kupewa. Maanake pale chini imeshaandikwa kwamba, "haimaanishi kwamba wewe ni raia wa Kenya"

Tatu, ningependa kutia mkazo kuhusu mambo ya banks. Hizi banks zimefanya wakenya wengi sana kuwa maskini. Unakuta mtu amefanya investment katika bank, halafu bank linafungwa na raia wenyewe hawapati pesa zao. Na serikali imekaa kimya kabisa. Watu pesa zao zimeenda, watu wamechukua pesa wametoroka. Serikali hailipi pesa za wale watu kutafuta njia yoyote. Asante.

**Com. Swazuri:** Shukrani. Namba tatu.

**Bwana Ngare:** Mimi kwa majina naitwa Charles Ngare. Nakuja na swali la free education. Nimesikia ukitaja ya kwamba kuna elimu ya bure kutoka darasa la kwanza hadi darasa la nane au saba. Sasa, mambo kama haya tulikuwa tukiyasikia yakinenwa lakini wakati mwingi haifanyiki hivyo. Kutakuwa na taratibu gani kuonyesha ya kwamba ni kweli, elimu itakuwa ni ya bure. Kwa sababu, sisi ambao tuko mashambani kule tutaelezewa kwamba elimu ni ya bure lakini kunakuwa na watu ambao ni lazima wanaitisha fedha. Sasa, nataka kujua kutakuwa na mwongozo au taratibu gani ili tuhakikishe kwamba elimu ni ya bure.

Pili, sijaelewa vizuri kuhusu hii title deed. Kwa sababu mimi nikiwa nimezaliwa na babu yangu yupo au mababu na mababa, lakini unashtukia ya kwamba hapo mahali pamekuja mgeni na anakuonyesha title deed. Sasa mimi kama mkaazi au Mkenya au Mmijikenda nitafanyaje mpaka nipate pale pahali. Asanteni.

**Mama Roni:** Kwa majina naitwa mama Roni. Roni Mwaloma. Mimi nina maswali mawili. La kwanza ni kwamba municipal

council zitaondoka na county councils zitakuja na Governor. Sasa Governor vile umesema ataact kama DC. Sasa, ikiwa ataact kama DC, hawa macouncillors ambao wanawania viti saa hii, wao pia wataingia kisiasa, maanake tutaondosha administration tunaweka karibu kila kitu political. Now, ikiwa councillors na huyu Mayor ameingia kisiasa katika kile kijiji au sublocation, it means yeye atachukua nafasi ya chief. Sasa, hii nafasi ya chief, huwa ni wazee ambao wanachagua councillor ama ataingia kisiasa?

Pili, amesema kuwa wale watu ambao wanamali huko nje, wamepeleka mali ya Kenya huko nje, tungependelea isizitiswe ile mali irudi Kenya na hii pesa iende iwe, kuwe formed department ya mayatima. Hizi pesa zije direct kwa department ya mayatima.

**Com. Swazuri:** Namba tano.

**Ndirangu:** Naitwa Ndirangu. Nilikuwa na jambo ndogo nilikuwa nataka kuuliza, maanake, baada ya kusoma Katiba, kuna mambo mengine ambayo ninaona mlisahau. Kwanza, jambo la wachuuzi. Huwa wakati mwingine wananyanyaswa sana katika manispaa. Wengine hawapati nafasi angalau ya kukata leseni, na kama wamekata leseni huwa wanafukuzwa, wengine hufungwa,wengine wanaitishwa hata pesa nyingi zaidi. Hapo ni vibaya, maana wachuusi ni wengi na wanastahili angalau wanapewa nafasi yao hata kama ni pahali fulani patengwe wawe wanauzia pale katika mabaraza, hata kama ni Mombasa au Nairobi. Huwa wanasumbuliwa sana. Hapo sikuona kama mliandika jambo lolote kama hilo. Tena wengine hata amejenga kibanda chake, anauzia huko ndani, halafu kinabomolowa, amekata leseni. Sasa ataenda wapi na kishabomolewa, na amekata leseni? Mwangalie jambo kama hilo.

**Com.Swazuri:** Namba sita.

**Bwana Ngala:** Asante sana. Kwa majina naitwa John Ngala. Ningelitaka kufafanuliwa zaidi kwa hao ambao wanagombania upande wa Rais. Nasema kwamba, wale ambao wanagombania nafasi ya urais, mtu anaweza kugombania urais hata kama hatoki kwa chama chochote. Sijui hizi kura zote ataziomba kwa kina nani. Maanake, wale wote huenda kupiga kura huwa kwa chama fulani na mpaka uwe na kadi ya chama fulani ndio uende kupiga kura. Sasa hao watu ambao watampigia kura, akipata ule urais, atakuwa ni Rais wa kutoka chama gani? Hapo ndio sikuelewa vizuri.

**Com. Swazuri:** Namba saba.

**Bwana Tsuva:** Kwa majina naitwa Kazungu Tsuva. Swali langu ni kuhusu dini. Kuna uhuru wa kuabudu lakini tunazo dini za Kiafrika. Je, Katiba imetilia mkazo kiwango gani? Kwa sababu kuabudu kiafrika, kwa mfano Mungiki ambalo hilo ni gengi la majambazi…..

Pili, je, katika dini zetu hizi zinaweza kupewa kipao mbele kufundishwa katika mashuleni kama hizi dini nyingine au zitakuwa zikibakia tu mle kichochoroni?

Tatu, ni swali la ardhi. Tulivyosikia kwamba hapa kuna wale wanaomashamba hapa na hawako hapa. Kutafanywa uchunguzi waletwe. Sasa kuna wale masquatters wanaokalia mashamba yale. Sikusikia wakitajwa zaidi. Baada ya kuchunguzwa, masquatter wale watafanywaje kulingana na wamekalia maardhi yale kwa muda mrefu. Hayo ndiyo maswali yangu.

**Com. Swazuri:** Namba nane.

**Bwana Njue:** Kwa majina naitwa George Njue. Mimi nagusia kuhusu Judge. Sikusikia Katiba ikielezea kama judge akihukumia mtu kimakosa, kama kuna mtu wa kumwangalia ambaye amewekwa na serikali. Huyo mtu ataenda kulia wapi kama judge akihukumia mtu kimakosa, kuna mtu ambaye atawekwa kwa court na Katiba kusikiza yule mtu ambaye amedhulumiwa au atakimbilia wapi.

La pili, kama polisi anaweza kukamata mtu ambaye ako rumande na huyo mtu aje kwa court na ajulikane hana makosa na amekaa rumande siku 28 na kule alikuwa anafanya kasi amefutwa. Ni nani anaweza kulaumiwa? Ni polisi, au yule mtu anaweza kukimbilia msaada wapi? Hapo sikusikia vile Katiba imepitisha.

La mwisho, mtu anafaa kungoja kesi siku ngapi; sababu wengine wanalalamika 28 ni siku nyingi sana, na yule mtu pengine si mkosaji. Hapo sikusikia,Katiba ikisema mtu aweze kungojea kesi siku tatu au nne au siku ngapi.

**Com. Swazuri:** Namba tisa

**Bwana Nassir:** Asanteni sana. Kwa majina mimi naitwa Nassir Khamis Said. Hamjambo nyote. Nasema kifupi, sitaki kueleza zaidi mengi tena hapa kupoteza wakati. Hii mambo ya ploti, sijui ardhi ama wewe wawaambia ni ploti elfu thelathini au arobaini, hamsini sijui vipi, ambapo wewe serikali pengine haikukupatia pesa kama hizo. Ikizidi sana hata masomo yenyewe ikizidi wewe umepata kuwa ni vigumu kusomeshwa, pengine hata hukumaliza. Sasa pesa kama hizo utapata wapi kazi hizo ambazo uweze kupata pesa hizo kulipia hiyo ardhi ndio ukae wewe? Hiyo itakuwa maisha ya aina gani sasa? Twataka tujue kitu kama hicho. Ama mtupatie pesa tujue tutanunua hiyo ardhi. Kitu kama hicho.

**Com. Swazuri:** Namba kumi.

**Bw. Charo:** Kwa majina naitwa Sammy Charo. Swali langu ni kuhusu pesa za uzeeni. Pesa hizo ambazo tutakuwa sisi tunapewa ni kwamba unakuwa na miaka hamsini na mitano, ama mtu ambaye amekufa. Je mimi kama kijana, nimefanya kasi miaka kama ishirini na tano, na pengine nimegonjeka, nimekuwa mgonjwa, nina haki ya kupata zile pesa nikiomba kwenye

Katiba ya sasa au haiwezekani? NSSF.

Swali lingine ni kuhusu permit za matanga. Utakwenda kwenye matanga, ukiangalia hakuna kaburi. Mtu amechukua permit na anaendesha matanga mahali hakuna kaburi. amechukua permit ya matanga, ukiangalia kwenye hiyo matanga hakuna mtu ambaye amezikwa. Sasa, hata kama ni mtu amekufa mbali amekuja, unaweza kumchukulia permit. Lakini, je ni siku saba pekee unazoweza kuondoa hiyo matanga. Je kama kuna ile matanga inaenda mpaka mwezi mzima. Ni matanga ama ni biashara?

**Com. Swazuri:** Yule mama mwenye mtoto.

**Ms. Mwanguo:** Habari zenu. Kwa majina naitwa Martha Mwanguo. Nimesikiza lakini kwa upande wa foreigners, wale wazungu kuna kitu kimoja ambacho wanafanya sijui Katiba itatuangalia vipi? Ijapo wanatuletea pesa, lakini tunapata matumizi ya wasichana hasa hapa Coast. Wanatuharibia vitoto vidogo sana, ambayo hata unakuta kwa hotels, unaweza ukaandikwa lakini iwapo utakataa yale mzungu atakwambia, anaweza kutupilia mbali bila hata malipo yoyote. Mimi mwenyewe nilikuwa nimefanya kai kwa hotel for 2 years as a tailor. Imefikia pahali, with no reason, mzungu ameniambia, "nimechoka na wewe". Nikienda kwa Labor officers nikitaka haki yangu, mzungu akaenda akaangusha pesa, Nimeshadidimisha kila kitu. Je hapo mtatufanyia nini katika Katiba yetu ya Kenya?.

**Com. Swazuri:** Haya. Haraka haraka tupitie ili tupate wengine. Upande wa CKRC; kama hii Tume itabakia ama itaenda. Kwanza tumependekeza kuwe na Constitution Commission ambayo itahakikisha Katiba hii imetekelezwa. Hiyo tumeiweka pale, ya watu watano. Halafu watu wamependekeza civil education ifanyike hata mashule. Hilo ni swala ambalo tumekubali tutaenda kulijadili.

Halafu mmetoa zile percentage za mali; tugawanye sabini kwa wilaya, ishirini kwa jimbo na kumi kwa taifa. Hiyo ni sawa. Taxation is too high.

Iko juu sana. Nafikiri hizo ni sheria ambazo ….. kuna mambo mengine ambayo yataingia kwenye Katiba na kuna mambo mengine hayawezi kuingia. Details hatuwezi kuingiza hapa, lakini tumesema ya kwamba relevant legislation lazima iangalie. Maanake tukishasema kwamba mwananchi hana haki ya kudhulumiwa pesa zake, hiyo ni broad principle ya Katiba. Sheria zote zitabadilishwa kuhakikisha kuwa mwananchi hadhulumiwi. Maanake tumesema kwamba siku ikipitishwa Katiba hii, sheria zote ni lazima zifanywe, zirekebishwe, ziwe sawasawa na hii constitution.

Birth Certificate. Ile pale huandikwa vile kwa sababu ya wageni. Kama kwa mfano, Mnigeria na bibi wake wa kinigeria wanakaa hapa Malindi, halafu wazae. Akizaliwa mtoto ni lazima aandikishwe. Lakini kwa vile ni Mnigeria, ni lazima kwamba ni Mkenya. Ndio maana ikaandikwa vile. Sio kwamba akishaenda pale hospitali Malindi akipewa ile certificate aseme "basi, mimi

nishakuwa mwananchi wa Kenya " huku babake na mamake ni Wanigeria wanafanya kazi halafu wataenda kwao. Hiyo huwa inaandikwa kwa sababu ile. Lakini ule ni mwanzo wa mwananchi wa Kenya kuanza kudai uraia wake. Na tunaandika ni hesabu ya kuhesabu watu. Banki zinazo-collapse: kuna Depositors Profession Protection Fund. Nafikiri hiyo ndiyo haijatiliwa mkazo lakini si sawa wananchi ku….

**Interjection :** (…Inaudible)

**Com. Swazuri :** Basi hapo ni sawa. Kwa hivyo tuiandike kwa foreigners iwe hivyo. Lakini kwa Kenyans, ukipata ile ujue ndio mwanzo wa uraia wa Kenya. Hiyo ni sawa.

**Interjection:** (…inaudible) kama mimi nina birth certificate ambayo ni ya 1946 British and Colonies.

**Com. Swazuri:** Kitu gani – birth certificate.

**Interjecting speaker:** Birth certificate ya Colony and Protectorate. Nikiipeleka kwokwote kule, basi birth certificate zile walizi-consfiscate ambazo zinaonyesha uraia wetu wa zamani, hata za mababa zimeandikwa 'Colony and Protectorate' kwa sababu ……. Inaudible.

**Com. Swazuri:** Haya sawa. Free education. Nani atahakikisha. Tumeandika pale. Sasa hii imekuwa ni haki ya lazima ya kimsingi. Serikali lazima ihakikishe kwamba iko. Halafu pili tumesema kwamba maana ya kuleta serikali za majimbo na wilaya na location ni hii sasa. Wale wazee wangu ambao watakumbuka, sisi tulisoma bure. Ilikuwa ni kazi ya nani? Kazi ya wilaya. Ilikuwa ndio iliangalia kuwa mashule yamepata vitabu, yamepata kalamu, choki, kila kitu. Ilikuwa ni jukumu lao. Tumerudisha ile sasa. Kwa hivyo ni jukumu la wilaya kuhakikisha, au jimbo. Kwa sababu mmesema mwataka serikali ya majimbo mjiangalie wenyewe. Hapo basi kazi yao ni hiyo. Hata barabara. Minister atakuwa pale akiallocate funds. Zinakuja kwa jimbo. Haya angalieni mambo yenu. Mkiharibu nyinyi wenyewe.

Halafu upande wa Councillors. Tumesema kwamba devolved government – serikali ambazo ni za chini, kuanzia za jimbo mpaka za wilaya mpaka za location, zinafanya kazi mbili. Ndio maana tukaondoa ile provincial administration. Serikali hizi zinafanya administrative work na zinafanya legislative work. Kwa hivyo wanafanya zote – sheria na utawala. Ndio maana tukaondoa ….. Kwa hivyo ile serikali ya kijiji siyo kwamba ni serikali ya wazee-tumesema ni serikali ya kijiji. Hatukusema ni serikali ya wazee – na Katiba imependekeza ya kwamba nyinyi wenyewe wanakijiji kile ndio mtaamua mtachagua nani. Kama mtaamua wazee wote ndio watakwenda hiyo ni jukumu lenu. Kama mtasema tutachanganya vijana, wazee, yeyote bora awe anaweza kutuongoza, hiyo ni kazi yenu nyinyi wenyewe. Lakini hiyo sio kwamba ni serikali ya wazee. Hiyo ni serikali ya kijiji. Halafu serikali ya location. Kwa hivyo hawa councillors, tumesema tutakuwa na mkuu wa location, na atafanya kazi zote mbili; administrative na legislative. Huyu atachaguliwa na wananchi wote. Halafu wale wa district, wale district council members. Hao

nao watachaguliwa na wananchi wote. Hata district governor atachaguliwa na wananchi wote.

Mali iliyoko nje irudishwe nchini, hilo ni wazo zuri. Hawkers small traders:Tumesema katika Section 53 kwamba kuna uhuru wa kufanya biashara unayotaka lakini tu iwe mahali ambapo imesemwa ifanyike. Kwa hivyo sasa ni upande wa ile government iliyoko pale, itaamua hawa wafanyikazi hawa wataenda mahali gani. Lakini tunajua ya kwamba ingawaje tunasema hawking, watu waruhusiwe kufanya biashara pahali popote, Lakini unajua taabu ambazo huwa zinakuja ikiwa biashara itakuwa inafanyika mahali popote unapokwenda, ni biashara. Huwa kuna shida kwa wananchi; hata kutembea hawezi kutembea vizuri, gari pengine zinazuwika kwasababu watu wamepanga mali mpaka karibu na barabara. Lazima tufanye biashara kwa hali ya kibiashara. Siyo kwamba kwa vile tuna uhuru wa biashara, basi ni popote hata chooni watu wanaweka mali tu. Hiyo haitakikani hata sisi ni binadamu. Lazima tuishi good decent living. Kwa hivyo ile serikali ya pale ndiyo itapitisha hizo sheria sasa.

John Ngala: Independent presidential candidate atapata kura wapi. Atapata kura huku kwa wananchi. Tofauti ni kwamba yeye hana haja akapigiwe kura huku sijui chama gani mara wamepigana huko mara ……Yeye anasema, "mimi nataka kuwa rais na sina chama nipeni kura zenu" basi. Mkimpa atakuwa rais. Iko hiyo. Nchi nyingi iko kwa maana kuna wapiganiaji wa urais wa vyama ambao wanasema wanapunjwa katika vyama vile na wanahakika wakiwa huru wanaweza kupata kura, basi wapate nafasi. Kila mtu apiganie anavyotaka.

Kazungu; African Religion - Dini za Kiafrika tumesema kwamba kila mtu ana uhuru wa kufanya dini yake. Nimeeleza kwa kinaganaga, lakini dini hizi zisiwe ni kwamba zinadhuru maisha ya wananchi. Hapo tumeandika kwa kinaganaga kabisa kwa sababu isiwe ni dini halafu ni dini ya kuua watu au ni dini ya kufanya devil worshipping au ni dini ya kusumbua wengine usiku au ni dini ya barabarani hakupitiki tumefanya tumesema ufanye dini yako vile unavyotaka lakini angalia maslahi ya mwingine. Hatukusema kuna European religion wala African religions wala nini. Tumesema freedom of religion and belief.

Squatters, hilo ni swala ambalo tumesema hapa. Hatukulitaja hilo neno squatters, lakini ukiliangalia lipo, maanake tumesema serikali ihakikishe kwamba kila mwananchi wa Kenya anapata arhi. Ardhi ni ya wananchi wa Kenya. Halafu tukasema kwamba ukiangalia section mia mbili thelathini na mbili, kifungu cha nne tatu, tumesema kwamba serikali ifanye mbinu hata kama ni mikopo, fund iweko ili watu waweze kununua ardhi. Hiyo pia iko hapo.

Kama jaji amefanya makosa mtu ametumiwa kwa hongo, hiyo sasa ni rahisi kabisa. Unaenda kwa public defender, basi, mambo yashaisha. Hongo yoyote unaenda kwa public defender. Yule si polisi wala si serikali. Sasa yuko yeye ni mtu wa wananchi. Na ana legislative powers yule. Na tumesema kwamba mwananchi asishikwe akakaa zaidi ya masaa arubaini na nne bila ya kupelekwa kotini. Tumeandika sasa wacha kuwa iko kwenye zile judicial Acts. Sasa tumeiweka hapa katika Katiba kabisa. Ni kinyume cha Katiba mtu kuzuiliwa zaidi ya masaa arobaini na nne. Sasa ni kinyume cha Katiba. Halafu akaeleza kuhusu kesi kwamba zinachukua muda mrefu. Tumesema kwamba tumeipatia Bunge wahakikishe kwamba wapitishe sheria katika miaka miwili inayokuja kuhakikisha kwamba kesi zote zinafanyika kwa muda ule unaotakikana wa miaka miwili

haraka kabisa.

NSSF hiyo unaweza kupata pesa zako kama hujafika miaka hamsini na mitano. Hiyo wananchi wamelalamika sana. Tumesema sasa kumepitishwa sheria inayoitwa Retirement Benefits Act ambapo zile benefits za wafanya kazi zinatakikana ziwe invested na wale wanachama tayari wao huwa ni members wa ile fund kwa hivyo wana benefit pale, lakini sasa nafikiri tutaiachia sheria kusema kama kila mtu ana uhuru wa kuzichukua kabla au baada. Wazungu hawa ambao unasema wanaonea watu tumesema kwamba kila mfanyakazi ana haki ya mshahara unaofaa, tumeondoa utumwa, vile nilivyosema mama. Utumwa huu tumeuondoa katika kazi, katika siasa, katika maofisi, katika mahali popote. Mwananchi wa Kenya atakikana awe mtu huru na tumesema hawezi ku-obey unlawful instructions. Kama hazifai hizo unaenda na Katiba yako unamwambia "Katiba yangu imesema siwezi kufanya mambo kama haya. Ni kinyume na Katiba." Hataki unaenda kwa public defender. Hiyo ni very simple sasa, badala ya kwamba uende sijui kwa inspector wa labour, sijui wapi, wapi, upelekwe mbali, tumesema huko ni mbali sana. Waweza kwenda kulalamika hapa hapa, na yule mtu atachukuliwa hatua. Ikiwa kuna hongo zimepitishwa tumeshasema kwamba sasa hongo ni hatia. Tena tumewekea penalty zake.

Haya round ya tatu. Watu wazidi, naona napunguza. Haya nitaanza pale. Namba moja ni wewe na uje tayari, halafu namba mbili mzee wangu pale, uje karibu, namba tatu uko karibu tayari, twende kule nyuma, namba nne haya ushike namba. Namba tano, mama umeshasema kwa hivyo utatuwia radhi kidogo. Namba sita halafu nitarudi upande ule. Hakuna mtu. Mwenye shati nyekundu namba saba. Namba nane, namba tisa vijana msije mkasema tunawatoa. Halafu mzee wangu namba kumi. Tuishie hapo halafu tutaongeza. Maalim kumi na moja, bwana miwani kumi na mbili. Mpaka tumalize. Maalim pale kumi na tatu. Haya. Kila mtu ashike namba yake.

**Francis Kalume:** Kwa majina mi naitwa Francis Kalume. Sasa swali langu linasema hivi, ukiangalia ile mitunda ambayo inakuzwa hapa pwani ni mingi sana kulinganisha na ile mitunda ambayo inauzwa kule sehemu za bara. Sasa ukiangalia upande wa bei, yale mazao ambayo yanapatikana kule bara ni ya hali ya juu sana, ukilinganisha na hii bei ambayo inafanyika hapa upande wa coast. Iko taabu gani ndio mazao hapa kwetu iko chini sana.

**Bw. Abud:** Kwa majina mimi ni Abud Swaleh Baseif. Sina maswali lakini moja nataka kulizungumzia na Bwana commissioner swazuri utanipa ruhusa. Kwa miaka arobaini tulikuwa tunalia twataka Katiba ya majimbo. Katiba ya majimbo ndio hii hapa imefika. Mwangoja nini msishangilie?

**Bwana Nzai:** Ronald Nzai. Mimi niko na maoni na maswali. Oni la kwanza ningomba katika Katiba hii kuwe na sheria ya kwamba mtoto anapozaliwa apate birth certificate either ni nyumbani au ni hospitali. Halafu akifikia umri wa kupata kitambulisho apate kitambulisho halafu passport nayo apate. Halafu kuwe na sheria ya kwamba akipata kitambulisho pale pale kuandikishwe kura kwa hivyo hayo ni maoni. Swali pia maoni mengine. Hawa foreigners ambao huja halafu wakafanya business niko na maoni ya kwamba wawe na partnership na Wakenya. Iwe sheria. Akitaka kuwa businessman awe na partnership na Mkenya.

Swali. Tumesikia qualifications za rais na wale wengine. Sijui kama Wabunge watakuwa na academic qualifications ama ni wale wawili. Na swali lengine. Kumekuwa na udhuluma na hii imesabishwa na pesa. Kwa mfano mtu ukiwa Malindi ametoka tuseme somewhere from upcountry, anakuja pigania kiti cha Ubunge hapa malindi kwa vile ako na pesa na mtu huyo anaweza kupita lakini baada ya kupita hata anaanza kudhulumu wale wenyeji. Kwa hivyo natoa oni ya kwamba yeyote atakaye gombania kiti cha kisiasa awe mwenyeji wa eneo lile na kwa muda fulani awe ameishi pale wenyeji wa eneo lile wamemjua vizuri. Kwa hayo machache Mungu akabariki Bwana Commissioner.

**Bw. Munyole:** Mimi naitwa John Henry Munyole. Mimi niko na maoni na maswali. Maoni yangu, nataka iwe sheria moja kulingana na forces, watu wasiandikwe permanent. Kenya mzima iko na watu wengi. Mtu akiaandikwa pale anakaa miaka thalathini, mtu mwingine atafanya kazi saa ngapi? Nataka watu wakae pale kwa contract. Miaka tano zikiisha, kama anataka kusign asign miaka tano zikiisha aende apumzike mtu mwingine afanye kazi. Kwa sababu watu wa Kenya wote wanakosa kazi kulingana na hao watu wanakatalia kabisa kwa Forces.

Ingine nataka sheria ya polisi ipunguzwe. Ile nguvu yao ipunguzwe kwa sababu wanaingia jijini wanapiga piga watu. Nataka vijiji viwe na watu wale watakuwa mtu akiwa amefanya makosa polisi anaripoti kwa yule mtu. Basi hiyo ndiyo tunataka. Sasa kitu kingine mimi kama citizen wa Kenya tangu tupate uhuru tumefaidika na nini? Na hii constitution itasaidia mimi nini? Kwa sababu hamjatetea maskini. Maskini mpaka dakika hii bado ananyonywa. Ukienda hospitali ni pesa. Ni sasa kama constitution inaandikwa ifanye kazi juu yetu. Wasikuwe wanatukamua huko kwa polisi, wanatukamua huko kotini, wanatukamua huko hospitali. Tunataka vitu viwe free visaidie maskini.

Na ingine kulingana na maoni ya wenzetu wale wamezaliwa hapa, zile ofisi ziko na maneno mingi sana na hizi office za serikali, wewe ukienda na maneno yako mpaka watakoroga hivi hivi. Office ya kwanza ni ya labour. Mbovu sana. Haijalii maslahi yetu. Inatetea tajiri. Kwa hivi sisi maskini tunageuza constitution namna gani kwa sababu huko juu kuna pesa, wewe sasa huwezi kujulikana. Hapa ni pesa. Hiyo kitu kitatoka namna gani. Hiyo constitution itasaidia kutoa hiyo kitu? Ahsante.

**Bw. Mnyeto:** Jina ni Seif Ahamad. Nina maoni na swala. Kwanza ni kwamba- ndugu yetu ametuzungumzia hongo. Hili hongo ni miongoni mwa ufisadi na unyanyasaji. Na imeenea kila mahala na tumeambiwa kwamba itachukuliwa hatua kwa mwenye kutoa hongo na mwenye kuchukua hongo. Je hatua kama hii itakuwa ya namna gani? Kwa sababu jambo hili limeenea kila pahali la hongo na unyanyasaji.

Pili demokrasia. Kwamba tunachagua viongozi wa Bunge na kadharika kama ilivyo. Lakini tunapowachagua Wabunge huwa hawapewi nguvu ya kututetea ama kutetea wananchi wao. Kwa sababu kule city hubanwa wakawa hawana sauti ya kuweza kutetea wananchi wao. Wanabanwa na serikali, kwa sababu utakuta yale wanayoyazungumza kutaka kutetea watu wake akitaka jambo fulani anaambiwa litazungumzwa au litafikiriwa. Basi miaka inaenda lakini hakufanyiki jambo. Natoa rai kwamba apewe uwezo mbunge wa kuweza kuwatekelezea wajibu wananchi. Lakini imekaziwa sana na serikali.

Ndani ya maforest kunapatikana miti na miti tunapata mbao, kuna wanyama lakini utakuta vimewekewa vikwazo vikwazo, kiasi cha kwamba mtu hawezi kujenga kama hana uwezo wa mablock, hawezi kupata chochote katika maforest. Mali imeekewa wale ambao tunawaita watalii, kuja kuangalia miti, mapaa, ilihali sisi wenyewe ambao tuko katika tumeketia forests kama hizo hatufaidiki. Masalan kama Gede Forest utaona majirani wa pale pengine hawawezi kujenga mpaka kwa taabu sana ilihali miti iko karibu. Kwa hiyo ningependelea serikali ambao kwamba itakuwa kwenye mamlaka iweze kuweka free sehemu kama hizi watu waweze kufaidika. Yangu ni hayo.

**Bw. Gikundi:** Kwa majina ni Alex Gikundi Dewa Pilipili Manga. Mimi ni mshairi. Yangu ni matatu tu, ambayo ni kuhusu mambo ya umilikaji wa ardhi. Je tumesika katika umilikaji wa ardhi, watu wale ambao ni wageni ikipitishwa hii Katiba itakuwa lease yao ni ya 99 years. Swali langu,je, yale mashamba au public utilities zile ambazo zimekuwa grabbed, je, zitaregeshwa? Maanake tukiangalia hapa hapa mimi nasikitika sana tena natoa machozi kwa sababu hapa especially Malindi, vile viwanja vyote ambavyo viko hapa ambavyo vijana walikuwa wanachezea vyote vimeuzwa na unajua hapa tunapigiwa kelele hapa kunatumiwa madawa ya kulevya. Je, kama hatuna mahali pa kwenda kucheza itakuwa hiyo kitu si itaendelea?

Okay. Lingine nalo ni misuse of public funds by the ministry. Tunaangalia ya kwamba kila siku tunasikia minister fulani leo amekuwa hapa ametoa laki tano. Wiki ijayo anatoa laki tano. Wiki hiyo inapita laki tano. Je hizi pesa zinatoka wapi? Kwani mshahara wake ni pesa ngapi? Sasa hiyo kitendo lazima twangalie vile ita-limit ile pesa ambazo zinatumika.

Lingine, nasikia hizi presidential powers sasa hatukujua vile ambavyo zitakuwa trimmed. Maanake kama ule wimbo tunasikia unaimbwa kila siku, Chancellor of all universities in Kenya - the president, commander in chief of all armed forces - president, sasa hiyo kitu tunataka tujue vile itakuwa ikiendelea.

Lingine ni presidential trips. Na hapa Kenya president wetu ameenda ziara nyingi sana za nje. Hizi ziara lazima awe kama anaenda zijadiliwe na Bunge. Sio lazima kila wakati ni trip trip hiyo lazima ijadiliwe na Bunge.

Ya mwisho ni kuhusu utumizi wa mali ya umma. Unaweza kuangalia kama ni bwana mkubwa fulani hii gari tunajua ni ya serikali, ikifika saa kumi na mbili ofisi zote zinakuwa zimefungwa, lakini unaweza kuona ukipitia kwa manight club utaona gari ya serikali iko nje ya club. Hiyo ni lazima iangaliwe maanake hiyo petrolil inatumika pale ni pesa zangu mimi mwenyewe zinatumika pale maanake serikali ni mimi. Kwa hivyo kitu kama hicho kiangaliwe.

Na pia zile presidential escorts pia ningependa zipunguzwe kidogo. Unaona kama rais zile gari anazo ni gari zaidi ya arobaini na siku hiyo yale mafuta yanayotumika ni mingi sana. Na ni pesa zangu mimi mwenyewe zinatumika. Kwa hivyo hiyo kitu lazima iangaliwe. Ahsanteni sana.

**Bw. Bazmale:** Mimi kwa jina naitwa Abid Salim Bazmale. Na mimi hapa ninamaoni manne, na kisha swala. Katika Katiba hii najua imechukuliwa mpangilio wa majimbo lakini mapendekezo yangu ni kule there is a complete federal government ambayo kila jimbo litakuwa na Bunge lake na serikali yake ikishirikishwa na serikali kuu. Ya kwanza.

Ya pili ni kuwa foreign investors wanaokuja ku-invest tuseme wanakuja Kenya ku-invest kama mji wa Malindi. Tunataka kumpe ile community ya Malindi wapate share kama 60% ije kwa wale wamalindi na 20% iende juu kwa serikali hiyo ya majimbo na 20% iende kwa serikali kuu.

Na la tatu ni kuwa pia NGOs ambazo zinasaidia umma au miradi ya umma isifikiri miradi ile kuwa kama kuna mradi fulani unasaidiwa na NGO fulani kutoka nje na miradi ile iko hapa Malindi, pesa zile zisipitie kule serikali kuu, zije direct kwa wale wenye zile NGO ziwasaidie.

Na ya nne ambayo ni ya mwisho ni kuwa nguvu za hii polisi kwenda kuarrest watu mpaka usiku manyumbani without a warrrant kusiwe na ruhusa ya polisi yeyote au security yeyote kwenda kumshika mtu nyumbani kwake au kusearch nyumbani kwake bila warrant na bila sababu fulani kwa ile warrant. Na tena iwe ni time za mchana sio kuwa watu wamelala aende akavunjiwe mlango, avutwe kitandani atolewe. Ahsante.

**Bw.Odhiambo:** Ahsanteni wananchi. Jina langu naitwa Dan Ayoo. Lile jambo naona linasikitisha hapa Malindi ni moja, serikali wanapesa, wanaitwa pesa trade, pesa trade ni mtu ambaye anafaa na kibanda. Kibanda ya kuuza chumvi, kuuza sigara ile pesa tunaona ajabu. Wale ambao wanazo ndio wanapewa hizi pesa tena na wanaunga hii pesa. Wewe ukiwa ni mtu mdogo hutaipata hii pesa. Tunashangaa serikali yetu wako wapi. Huko wanatwambia watu ambao hawakusoma wanaweza kuendesha biashara. Biashara utaendesha na nini na huna kitu ambacho unaweza kuanzisha biashara?. Mikopo iko kwa trade. Hiyo pesa serikali inatoa every year. Pesa hiyo nadhania kuna watu wengi hawajui hapa Malindi lakini kuna watu wanajua hiyo pesa. Ni watu ambao wana pesa investors wakubwa.

Jambo la pili. Hakuna investor tunasema tunao hapa Malindi. Wao ni wale wanakuja kuchuma na kuenda na pesa. Na serikali imewapa nafasi ya kutumia njia ya kubadilisha hiyo pesa into Euro money. Wanapeleka hiyo pesa direct kwa sababu wanasema wanapeana milioni thelathini kwa serikalki na hiyo ina watu binafsi. Unaweza kuhesabu watu kadha ambao wanapewa hiyo pesa. Kitu kama Casino inaingiza pesa zaidi. Kuingiza pesa kwake ananyanyasa wale wafanyi kazi- hakuna night allowance, hakuna vitu vingi. Na hiyo tukisema namna hiyo anakwaambia you go where you want. If you go to the head office we are ready. Hiyo ndio tunaomba kwa serikali ya sasa. Mnasema mnabadilisha constitution. Constitution yenu iwe itasaidia. Na ikiwa tutadanganyana sitaona kama ni sawa.

**Bw. Nyuleh:** Kwa majina najulikana kama Nixon Kingi na niko na machache nataka kuongea. Mwanzo ni hii duration ya land. Nafikiri 99 years ni miaka mingi sana kwa makadirio ya mwanadamu wa sasa. Hapa nchini Kenya sidhani kama kuna mtu hapa

ataishi miaka tisaini na tisa. Hiyo nafikiri watakuwa wamesha pewa absolute ownership kwa hivyo ningeomba hiyo kama itawezekana na kwa nini isiwezekane basi ni kitu ambacho chawezekana kwa sababu Katiba ni ya sisi wakenya na sisi wenyewe ndio tunafaa kuiunda hivi sasa. Hii miaka ipunguzwe sana. Ni miaka mingi sana. Miaka nafikiri ingewekwa miaka kumi nafikiri ingekuwa sawa. Miaka kumi tu lakini miaka tisaini na tisa hiyo ni absolute ownership na itakuwa si sawa.

Halafu about capital, tunaona kwamba kwenye Katiba hapo kumeandikwa Nairobi is the capital city. Mimi nafikiri haitakuwa sawa. Hiyo ingetolewa kwenye Constitution iwekwe iwe free ambapo tunataka maendeleo ya nchi nzima. Pengine tumeona Mombasa isha-develop ilikuwa capital city lakini isha-develop kwa hivyo tu-shift tupeleke pengine Nakuru i-develop tufanye Nakuru capital city. Lakini isiwekwe kwenye Constitution kuwa Nairobi is the capital city. Hiyo itakuwa ni makosa. Tunataka maendeleo ya nchi nzima.

Halafu about presidential qualifications. Mimi naona ingekuwa bora zaidi wazazi wa mtu anayegombea kiti cha urais wawe wakenya halisi - baba na mama kwa kuzaliwa, sio watu wa kuja kisha mbali na hayo, mgombeaji wa kiti kile awe mwenyewe ni Mkenya halisi na awe ameishi hapa Kenya kwa miaka kadhaa. Si mtu amezaliwa ni Mkenya lakini maisha yake yote ameishi Amerika kule halafu amesikia kuna uchaguzi amekuja hapa kwa pesa zake nyingi amesema ataka kuchaguliwa kuwa rais, ilihali yeye mwenyewe hajui shida za hapa Kenya, zinazowakumba wakenya wenyewe ni zipi. Mkimpa urais iwe ni mambo ya kuponda raha na mambo mengine hata hajali maslahi ya Wakenya.

Halafu kuna jambo lingine hapa ambalo limeleta utatanishi kwa siku nyingi. Ni baadhi ya Ministers kila siku tunasikia pesa milioni mbili zimepotea halafu mambo yanaenda yanazimwa, hakuna kitu chochote ambacho kinafanyika. Hivi sasa uchumi wa Kenya kusema ukweli umeanguka kabisa. Hawa watu Katiba ilikuwa inawapangia nini.? Mimi ningeona ingekuwa bora watu kama hawa akiwa ameshikwa na kuna evidence wazi kuwa pesa zile ndiye aliziiba basi ashikwe awekwe ndani halafu pesa zile zitafutwe alizipeleka wapi ziregeshwe kwa serikali ili zikafanye ile miradi ambayo imepangwa na serikali. Sio mtu aachiwe mara anakimbia anaenda kule. Hivi sasa serikali inayotoka, ni maovu mengi ambayo wamefanya na ni pesa nyingi ambazo zimeliwa. Ningeomba ingekuwa bora zaidi hao watu accounts zao zichunguzwe tujue mishahara yao walikuwa wanapata kiasi gani. Halafu zile pesa nyingi ambazo walibindikizandikiza walizitoa wapi. Na kama itawezekana ziregeshwe kwa serikali. Hawa watu pia wapewe adhabu kali sana. Kama ni kufungwa na mambo mengine kama hayo, lakini wasiachiliwe. Mara Bunge litakapovunjwa watu kama hao watakimbia, watachukua pesa hizi watazipeleka kule nje wataanza kuinvest kule nje halafu hapa nchini kwetu tutakuwa tukifaidika na nini? Kwa hivyo nafikiri hatua yastahili ifanywe watu hao. Nimeshukuru.

**Bw. Kamau:** Ahsanteni. Mimi ningependa kuongea juu ya investment. Kama yule alitangulia hapa aliongea, juu ya investment. Tumekuwa tukisema hapa kuna international investments ambazo zimekuwa zikija, lakini wakati mwingi tunakuta ni wanyanyusaji. Unakuta mtu anatoka nje, ni Mwingereza ama ni mkabila gani anatoka nje ya nchi, amekuja hapa Kenya na pesa, anapokuja hapa anakuta watu wanafanya biashara zao ndogo ndogo. Lakini zile biashara akiangalia hivi na akona zinaingiza pesa anachukua pesa yake anakuja anaingiza kila mtu hapo anaanza kumlipa pesa kidogo kidogo. Zile biashara

zingine wale wengine ambao walikuwa na pesa kidogo ambayo walikuwa wakijaribu kujiinua zinakufa. Sasa anabaki yeye kuwanyanyasa. Ile inakuja tena ni slavery lakini kwa sababu ana pesa inatamkwa jina lingine lakini bado ni slavery.

Nyingine ni kuhusu hii president. Hapa tumekuwa na presidents wengi ambao wanakimbilia, lakini ningependelea hata ikiwa president watakuwa arobaini ama wangapi, baada ya wale mapresident kufanyiwa election yao, tunakuwa na presidents wawili ambao kama hawatakuwa wamepata more than 50% turudie- kuwe na runner up ambaye yule president atakayekuwa na majority votes- more than 50% the total votes cast.

Ingine ni citizenship. Tumekuwa na kura hii ya uraia. Kuna watu wanatoka nje wanakuja Kenya. Wakifika Kenya kwa sababu wanapesa wananunua uraia. Na wewe mkenya halisi unapokwenda kule kwa registration unaenda unasumbuliwa unarudishwa huku na huku lakini yule aliyekuja hapa jana Kenya anapata uraia na wewe ambaye ni raia wa Kenya unabaki kusumbuka, leta birth certificate ya nani na nani, unasumbuka. Mimi kwa maoni yangu ningependelea hivi. Mtu anapozaliwa hapa Kenya na anapokuwa na guardian ambaye ni mzaliwa wa Kenya pia, zaidi ya wawili kama hakuna birth certificate, apate kitambulisho chake. Ahsanteni.

**Bw. Kesi:** Kwa majina naitwa David Kesi. Niko na maoni haya. Kwanza kabisa ni national currency. Tumeonelea kama kila president akiingia hapa anataka kubadilisha national currency kwa picha yake. Ile noti tu akiingia anataka iwe na picha yake. Sisi tunaonelea kuwa ikiwezekana ile national currency iwe na original picture ya the founding father peke yake. Kwa sababu tutakuwa tukibadilisha kila mara atakayeingia ni kumaanisha miaka kumi ikija kutakuwa na picha zaidi ya mia.

Halafu kitu kingine ni moral corruption. Nafikiri tume-address corruption upande wa mali na nini lakini hatujaangalia jinsi watu wanastahili kukaa katika public. Tumeona cases where wanawake hata wanaume wanaenda karibu uchi. Sijui Constitution itaangaliaje hali hiyo. Kila mtu wote kwa public awe anaweza kuwa yuko decent hawezi ku-cause provocation kwa mtu yeyote. Anavaa nadhifu ili kusiwe na hali zote zile ambazo tunaweza kuziita kama rape case. Na rape cases pia ziangaliwe kwa upande wa kwamba zile conditions ambazo zinaexist pale. Wakati mwingine unasikia ati mtu na bibi yake wamerapeiana au mtu na rafiki yake wamenajisiana. Hiyo iangaliwe ni conditions gani zilikuwa zina-exist wakati ule. Kesi ya kwamba ikipelekwa kortini hawezi kuwa na fair treatment. Halafu tumesikia watu wengine wamekosana kwa sababu juu ya biashara walikuwa wapenzi. Unasikia kuwa huyu anasema amenajisiwa.

Halafu kitu kingine twataka kuwe na free medical services kwa kila mkenya. Ahsante.

**Bw. Ngala:** Asanteni. Kwa jina naitwa Jefwa Ngala. Mimi ningependa kugusia sana upande wa natural resource - mali za asili. Kwa kweli siku za nyuma, wazazi wetu na ndugu zetu walikuwa wakienda baharini kule kuvua samaki ambapo walikuwa wao wanapata riziki zao kule. Lakini kutoka hii wildlife iingie unakuta wale hawawezi kwenda kuvua samaki. Tumewekewa mipaka, na nikiangalia hiyo ni uonevu kwa sababu hiyo ni mali ya asili ambayo wale walikuwa na bidii kutoka siku za nyuma. Na upande

pia wa msituni ndio hivyo hivy wanadhulumiwa. Kwa hivyo ningeomba hii Katiba katika ubadilishaji wenu muweze kushughulikia hili jambo vile wale wazazi na watu wa kitambo walikuwa wakitumia zile njia kujipatia haki zao warudi katika hali yao sawasawa kuliko hivi sasa.

Ukienda kule chini utakuta madau mengi yamewekwa juu na wazazi hawapati zile haki zao za zamani. Kwa hivyo hii serikali iliyoko sasa naeza kusema ni serikali zadimu. Naomba ile serikali ambayo itafuata iwe nzuri kwa kila mkenya aweze kufurahia matunda yake ya uhuru. Ahsante.

**Bw. Issa:** Mimi kwa jina naitwa Nassir Khalifa Issa. Mimi ni mkaazi wa Malindi, nimezaliwa Malindi, nazungumza kama mmalindi; kwanza nitazungumza habari ya ardhi. Katika hii Katiba naona kuhusu mambo ya ardhi bado hayakutiliwa mkazo sana. Kwanza ningependelea ardhi ya Mkenya yeyote yule pale anapokaa ile sheria ya kuwa yeye ana uwezo wa kwenda futi tatu chini kule kwingine kwa serikali. Hapo ningependa pawe pameondoshwa ili awe na uwez kamili ikiwa mkenya yule atakuwa pahali pale anapopamiliki pametoka madini ama kitu chochote ambacho kina manufaa yeye awe ni stakeholder. Serikali iwe itachukua kiasi fulani na yeye kiasi fulani. Isiwe kama hii mipango iliyoko sasa. Kwa sababu unakuta hivi sasa, ardhi hiyo ikiwa hapo pana madini yule mwananchi wa pale anaondolewa anapelekwa kwingine mali ile ya serikali. Serikali hiyo ni nani, si ni yeye? Hiyo iangaliwe vizuri.

Swali la elimu. Elimu hii hapa, tunasema elimu ni ya bure. Mapendekezo yangu ningesema elimu iwe ya bure kutoka nursery school mpaka form 4 au mpaka form 6 vile ilivyokuwa. Hivi sasa Wakenya wamegawanywa vipengo vitatu. Kuna wale matajiri wanaowasomesha watoto wao kwenye ma-academy, kuna wale wengine wanawasomesha watoto wao katikati kuna wale kama Nassir watoto wao husoma chini za mikanju. Ikiwa ni namna hii Kenya mimi siipendi. Tungependa elimu yote iwe sawa. Private school ziwe hakuna, awe mtoto wa waziri awe mtoto wa mwenye duka, awe mtoto wa maskini, sote tukutane pale salaali ili lile salaali lipate kuwa na mazingara mazuri. Kwa sababu yule tajiri ama waziri yule hatakubali mtoto wake kuja kukaa chini pale na uwanja wanamfunza. Kwa hivyo tuwe na elimu ya namna hiyo.

Elimu ya university hatutaki tena hayo mambo yanaendelea. Mtoto wa Fulani kwani babake ni waziri huyu anapata university hiyo ama college hiyo. Tunasema elimu iwe kwenye misingi sawasawa. Kila district itoe namba sawasawa. Ikiwa ni university, katika medical faculty itagawanywa watoto mia mbili wagawanywe kwenye mikoa saba. Watoto mia mbili wale wagawanywe katika madistrict yale. Ili wakati wa kufuzu wale watoto katika medical faculty tumejua katika mkoa wa Pwani tumepata madaktari saba na baada ya miaka kumi utaona tunakwenda sawasawa. Lakini leo hii unakuta elimu imekuvunja. Hatutaki elimu hiyo.

Na katika macollege iwe namna ile ile. Vile mimi nakumbuka, wakati mimi nikienda college, ilibidi hivyo. Nilikwenda watu washakwenda nikaambiwa wewe kutoka Pwani mbona umejiondoa? Andika jina lako pale, uende huko class. Kwa sababu nafasi yangu ilikuweko. Leo hii ukitaka kwenda kwa public health college, elfu arobaini kwanza zimuendee Principal, kisha fees,

kisha mambo mengine. Hiyo hatutaki.

Kenyan citizens. Nasema kuwa mkenya yeyote akifika miaka kumi na minane pale katika eneo lile chifu anayetaka kuchaguliwa na serikali ile ya wilaya ikichaguliwa pale watoto hawa wa miaka kumi na nane waambiwe wote nendeni pale mjaze fomu na uwape vitambulisho na passport zao pale pale. Sio kama sasa inavyokwenda mpaka ukaombe passport, ukaombe kitambulisho kisha mutu huyo anachukuliwa anapelekwa kotini wewe huna kitambulisho. Atoe wapi kitambulisho hicho?. Hata mie hapa nashangaa sina kitambulisho kile kipya. Na maneno haya nilimwambia chairman tukiwa pale social hall akaniambia kwa nini wayasema hadharani? Nikamwambia nayasema hapa hapa. Nitakupa barua, nikamwambia sitaki barua, nitakwenda kwa process zile zile kwa sababu hao wengine watapata wapi barua. Kwa hivyo nataka kitambulisho na mambo mengine mkenya atambulike, mkenya awe mkenya sawasawa.

Mali ya asili na rasli mali kama tulivyozungumza. Sasa hapa utakuta mambo kama haya maeneo ya reserve, maeneo ya mbuga za wanyama, maeneo ya chumvi hivi sasa yana watu maalum waliopewa. Kwa mfano kama maeneo ya chumvi kuna watu waliokuwa wakiishi pale na kufanya kazi. Lakini Bwana fulani alifanya kazi nzuri huko akapewa acre elfu tano kule. Hiyo chumvi yote yeye ndiyo anachimba pale akipeleka, wale wenye pale hawakupata. Maswala kama haya Katiba ikinge vizuri kwa sababu unakuta kuwa sasa mali ya asili haisaidii mtu wa pale.

Mwisho ni security. Security ninaposema mimi ni police. Utakuta leo hapa kuna recruitment ya polisi, ya jeshi, Kenya Navy na kadhalika. Waimbia pale uwanjani, watapelekwa mbio wale watoto watasema ah! Kisha baada wakachukuliwa watu wa hapa ni wawili ama mmoja. Watu wote washaandikwa hapo Nairobi.Tunasema tunataka community police, yule mtoto awe ni wa hapa Malindi, kwao ni hapa hapa, aandikwe police aende akampige babake na mamake na mjombake kule Lito. Ahsante sana.

**Bw. Adamba:** My names are Rodgers Adamba. Nitachanganya. Kwanza, nimetoka kwa shirika la CJPC- Malindi. Kuna ofisi ya Ombudsman. Nilisikia akiongea kuhusu District Defender. Sijui kama inaingiana na hiyo. Hiyo ndiyo nilikuwa nataka kuuliza.

Kuna transparent ballot boxes. Constitution inashughulikia vipi? Maanake tunajua bila transparent ballot boxes tuna uhalifu unafanyika wakati wa elections. South Africa ni nchi moja ambayo ilitumia transparent ballot boxes wakati wa election yao.

La tatu ni kwamba, kuna watu hao wana-cross from one political party to another. What steps does the Constitution take on these people? Inawa-treat vipi? Wataendelea kufanya hivo? Maanake kuna wengine ni matajiri lakini they are not giving people democracy. Watu wanatakikana wawe na demokrasia. Hawapati democrasia kwa sababu wao bado wananyanyaswa kwa njia moja au nyingine kwa sababu ya pesa za huyo mtu.

Jambo lingine ni kwamba the Draft Bill will have to go to Parliament before it becomes the country’s constitution. Which criteria will be used to make sure that there is less obstruction or impediment since, before it goes to parliament it will have to

pass through diffent stages?

Nyingine ni kwamba the constitution must provide for a free and fair election atmosphere and all political parties must benefit from the public fund equally during campaigns as what happened in Uganda - all political parties were funded and given the necessary assistance by the government.

**Interjection**: (inaudible). Umechelewa

**Mr. Adamba**: Sikuwako pengine (I am sorry. La saba ni kwamba the commission told us to work as providers as and that our money was to be paid later as plans were underway. What went wrong? Who do we blame, as that money which is used by the commission comes from the consolidated fund?

Number 8: a parliamentary committee should be made to check on companies that are awarded tenders by the government since some are doing substandard work. Asante.

**Mr. Mwaniki**: Kwa majina naitwa David Mwaniki. Swali langu lahusu kama katiba inatupatia utaratibu wa Kenya kupata Kazi, nanimwelekeo gani katiba imtutengea wananchi kupata kazi zao.

Swali lingine: kuna hizi pension dues after retirement. Katiba imetuonyesha kwamba, to take an example, unapewa your pension dues kama ni shilingi mbili wakati unaretire. Hiyo shilingi mbili itaendelea maisha yako yote ama ni vipi?.

Pili, kuna Kenyans ambao ni maskini sana upande wa magonjwa. Matajiri watapeleka watoto wao nje. Wakenya wale ambo ni maskini, watoto wao wataweza kupelekwa nje namna gani? Serikali ina utaratibu wa kupeleka watu maskini kupata matibabu nje?

Tatu: Katiba hapa inatupatia mambo ya freedom of association. Kenya ni nchi ya waafrika. Kwa sasa, kuna mambo ya association ambayo wakenya wanafuatana nayo. Sijui katiba kama imeongea kuhusu wanaume kuoana, sijui kama katiba imeongea kitu kama hicho. Swali langu ni hilo.

**Com. Swazuri:** Mtu wa mwisho.

**Bw. M'rojia:** Jina langu naitwa William M'rojia. Swali la kwanza ni kuhusu intake ya Armed Forces- Police, AP. Hapa, wanachi wa kawaida hutumia pesa nyingi sana kuingiza watoto wao katika hizi kazi. Kwa hivyo, hapa tungetaka kujua katiba yetu, is it defending us tusiwe tunatumia pesa kwa mambo kama hayo ya kuchukuliwa Forces?

La pili ni these police officers. Wana-interfere with our personal property. Kwa hivyo police ni lazima wawe notified. Akija pale kama amekushika, ujue kwamba huyu askari ndiye utapelekana naye kortini. Hakuna kwenda kubadilisha askari ndani ya cell: Unachukua CID, unachukua hata professional people. Kama yule amekushika ndiye mtaenda naye kortini na ndiye mtamaliza naye kesi- amekushikia nini na ni nini iko pale.

La tatu ; kuna hizi professional unions kama KNUT ya teachers. Lazima tuwe na national body ya kutetea na setting of salaries of every profession. Kama wewe ni mwalimu, mfanyikazi wa hoteli, mfanyi kazi wa wapi, there must be specified salary for your profession, sio ati employer anakwambia anakupa elfu mbili, anakupa elfu moja mia tisa sababu wewe ni security officer sijui Panasonic guards.

Ingine ni hii about the president. Ukiwa a candidate you must be working for your country for not less than 10years. Si kuwa ati we unafanya kazi nje kule, you were an ambassadeur halafu unakuja kuwania urais hapa. You must be currently working in our country for not less than 10years.

Kitu kingine kinachotuchezea ni hii mambo ya NSSF. Lazima kuwe na a notified duration. Kama mtu amefikisha miaka thelathini you should have the freedom to withdraw your money. Sasa kama ulikuwa unataka kufanya development, utafanya namna gani na unataka kufanya development, utafanya namna gani na pesa zako unaambiwa, “until ufikishe 60 years.” 60 years utafanya kazi gani? Kaburini ndiyo utafanyia pesa zako? Lazima kuwe na specified duration. After 20 years you can withdraw your money and invest it for future generations.

Kitu kingine ni these foreigners. Wanakuja kununua ardhi yetu. If you are a foreigner from Italy, England, lazima kuwe na increased land rates ili washindwe kununua hii ardhi yetu, kwa sababu tukiangalia, kama kule beach ni mahali pa Waitaliano. Wakiweka ukuta, tunalipa kwenda beach. Kwa hivyo ni lazima kuwe na increased land rates kwa hao foreign investors.

**Ms. Kamande:** Kwa majina naitwa Maria Kamande. Swali langu ni kuhusu watoto wa mitaani ambao tunawaita chokora. Katika katiba iliyoko- na mtakubaliana nami- hakuna mtu anayeshughulika na wale watoto, na wale watoto ni Wakenya, na wana haki kuishi katika Kenya. Je, katika Katiba mpya tunayoiandika, wale watoto tumewafanyia nini?

Pili, kuna huu ukahaba na watu walalamika. Katika constitution iliyoko sasa, inafanya nini kuzuia na kukinga magonjwa ya ukumwi?

Tatu: biashara zote tumekubali kuzifanya na kuzifanya kwa haki. Sote hata hapa Malindi tunalia kwa ajili ya dawa za kulevya. Hizo dawa haziletwi na mtu wa kawaida kama mimi na wewe. Zinaletwa na hao wakubwa. Je, Katika Constitution tunafanya nini ama tumeandikiwa nini? Asanteni.

**Com. Swazuri:** Haya , mambo ni mengi sasa. Bei za mazao ya Pwani. Sasa hakuna haja ya kulalamika, serikali ya jumbo itaangalia hayo mambo, si tena serikali ya Nairobi kuangalia haya mazao. Ni wenyewe hapa watafanya mikakati ya kuuza mazao yale- kama watatengeneza Development Authority ya nazi, ya korosho – hiyo sasa mmepewa mamlaka.

Bwana Abu alikuwa anataka tushangilie Katiba ya majimbo haya. Halafu Ronald akauliza, mtoto anapozaliwa apewe birth certificate na passport. Tumeandika katika kitengo cha citizenship na nimesema si favor wala si privilege. Ni lazima apatiwe birth certificate, kitambulisho na passport. Ni lazima. Lakini huwezi tu kupewa passport hata kama hutaki kusafiri. Ni kwamba ile siku unaposema unataka kusafiri, isiwe kwamba “kalete sijui nani”. Ni haki yako kupata, sio kwamba ni favour uanze kuchunguzwa au nini. Ni haki.

Halafu kuna jambo lingine ambalo amenikumbusha. Nilikuwa ninesahau kueleza tofauti moja kubwa ni kwamba tumesema kuanzia Katiba hii ikifanya kazi, uandikishaji wa kura sasa ni permanent – continuous, kila siku. Sio kungojea mwaka wa kura ndio watu wapewe mwezi mmoja au miezi miwili wakajiandikishe. Akipata miaka kumi na nane tayari yeye anandikisha kura pale pale. Hiyo ni continous – milele sasa.

Halafu foreigners; hilo ni wazo kuwa mgeni anapotaka kufanya biashara afanye partnership na mtu wa Kenya- hiyo ni sawa, tutaingalia.

Qualifications za MP tumesema awe ni form IV , lakini form IV mwenye Pass, sio form IV ambaye ana ‘E’. Tumesema form IV with a Pass. Na Pass ni ile ambayo inapeleka mtu kwenda Chuo Kikuu. Saa hizi ni C+ kwa hivyo form IV with a pass sio form IV hivi hivi tu.

Kupigania kiti- tumeandika pale waziwazi – lazima awe ni mtu wa pale, ana mali pale, ni resident wa pale. Hiyo tumeandika.

Bwana mmoja hapa amesema wanajeshi au askari wasiandikwe milele wasifanye zaidi ya miaka kumi. Tutaangalia hiyo, na amesema kazi ziwe ni za contract. Haya, hayo ni mawazo mazuri.

Halafu tumesema labor offices zina usherati mwingi. Tumesema tumeoutlaw corruption. Corruption sasa ni hatia, kwa hivyo hayo mambo utaenda kwa Public Defender, na tunataka services zote ziwe free. Tumejaribu kueleza pale lakini tutaandika kwa uwazi zaidi.

Demokrasia: Mmesema kuwa kuna hongo inatokea pale. Temesema kwamba kiongozi asiyefuata kazi sake hata kama ni Mbunge huyo utamtoa. Hata kama ni Rais amefanya mambo ya hongo- corruption – tumesema kwamba hiyo ni ground ya kumtoa.

Forests amesema waruhusiwe. Inategemea zile sheria za pale. Hiyo ni sawa. Kuna watu wengi wanalalamika hawawezi kupata kuni kwenye misitu kwa sababu ya forest officers.

Alex ameeleza kuhusu mashamba – grabbed land – ukisoma section 235 subsection 4b, subsection i ; 235 4b i imesema, ‘ serikali itachunguza katika miaka hii miwili shamba zote za serikali, za public za ministries, za departments ambazo zilichukuliwa kiholela. Ziangaliwe zirudishwe’. Imeandikwa hapa. Section hiyo imeandikwa.

Halafu security: Ni karibu watu kumi na ngapi pale watakuwa hawa ndio watu wanaweza kuamua security ya taifa, kama kuna vita ni hawa watu hawa. Sasa kwa sababu hiyo ndiyo tumesema Rais ataendelea kuwa Amri Jeshi. Lakini mambo ya chancellor wa university, sijui mkuu wa nini na nini, hayo hayapo.

Presidential trips; hiyo tutaangalia kama lazima siwe approved by parliament. Nafikiri Rais ambaye ameshtakiwa kusafiri sana ni Obasanjo. Obasanjo amefanya trips sabini na nane katika miaka minne ambayo amefanya kazi. Saa zote yuko nje yeye. Kwa hivyo kama mnataka tufanye utaratibu wa presidential trips, hiyo tutaangalia.

Habari ya magari; sheria tayari zipo kwamba magari ya serikali yana time zake maalum, isipokuwa kuna kazi maalum ambazo pengine hazina muda- 24 hours- kama za polisi. Magari yale huwa yanaenda. Lakini tunajua vile unavyosema ni kwamba wafanyikazi wengine hutumia gari ya serikali vibaya baada ya masaa yale yanayoruhusiwa. Hiyo ni sawa, sheria iko yake, ni kwamba haifuatwi.

Presidential escorts. Magari mengi – magari mia moja – yanafuata Rais. Hapo ni lazima tu taangalia.

Kila jimbo mbona hatukuambiwa kutakuwa na Assembly? Zimeandikwa hapa. Jimbo la Pwani litakuwa na Regional Assembly yake. Wilaya ya Malindi itakuwa na District Assembly yake. Kwa hivyo hayo yapo sasa.

Foreign investors; tunasema kwamba 60% ya revenue ibaki kwa wenyewe, 20% ya central government. Hiyo ni sawa, tu taangalia pamoja na wale wengine wamesema.

NGO funds; hiyo ni sawa, lazima zi-benefit wananchi wa hapo.

Police ku-arrest watu bila warrant; tumeondoa hiyo. Kwanza sasa katiba hii ikipitishwa, serikali hawezi kushika mpaka akuonyeshe namba yake. Mpaka akuonyeshe ile police service number. Kwa sababu tumesema unaweza kumshtaki, lazima ujue, uandike namba yake. Ikiwa ni makosa, wapeleka kule washtakia. Kwa hivyo, si tena ile muonekane pahali, “ haya haya, piteni kipande hii, haya haya!” Wewe una haki ya kumuuliza, “ wewe nani, lete kitambulisho chako”. Kama polisi hana kitambulisho, hiyo ni unfair administration. Nenda zako.

**Interjection:** (inaudible)

**Com. Swazuri:** Tumesema hiyo hakuna. Nimeeleza kutoka mwanzo. Nimeeleza kutoka mwanzo, huwezi kufanywa kukubali. Kuna sehemu hapa ambayo imesema wazi huwezi kufanywa kukubali kuandika statement, kukufanya ku-confess mambo ambayo hukuyafanya. Yote iko hapa.

**Interjection:** (inaudible)

**Com. Swazuri:** Mi nasema, yote hayo yapo. Kwa sababu wananchi wamekuwa wakilalamika kuwa unaenda kule unatoka msikitini unatoka kazini saa tano usiku, unaandikiwa kwamba ulikuwa na bhang au ulikuwa sijui loitering. Hiyo tumasema hapa. Mpaka utaambiwa wewe ulikuwa kitu fulani, lazima uandike statement wewe mwenyewe. Na una haki ya kuikataa ile statement. Au kuseme kuwa, "sishikiwi mpaka wakili wangu aje, hunigusi wewe mpaka wakili wangu aje" "Yuko wapi?" "Nambari yake ya simu ni hii ili kumfuata. Ukimleta huyo ndiyo nitaondoka" Iko hiyo tumeandika.

Halafu small traders wanataka mikopo. Ni kama ulivyosema. Hizi sheria nyengine zipo. Ni ile kwamba kuna ubadilifu tu, lakini mambo hayo yapo.

Mambo ya wale wageni kwamba pesa wasipeleke nje, pia sheria hiyo ipo, tayari ipo, ni ile kwamba haitumiwi kwa sababu wale wanawahonga wale wakubwa lakini hiyo sheria iko.

Bwana Kingi akaeleza kwamba lease duration anataka iwe miaka kumi. Hiyo ni sawa, tutaangalia, tutapunguza. Watu wamelalamika kutoka juzi kuwa 99 bado ni nyingi. Tutapunguza. Kwanza sisi wenyewe tulikuwa tumesema isizidi miaka arobini. Katika ile task force – na mimi nilikuwa mmoja wao – tulikuwa tumesema isizidi miaka arubaini lakini watu wakasema kuna commercial farmers, huwa wanalima sana wapewe miaka 99 kwa hivyo tutaangalia.

Capital city tumesema itakuwa Nairobi. Lakini ukiangalia ile sehemu inafuatia pale inasema, 'Bunge litaamua kama hiyo itaendelea au itabadilishwa. Ikiwa kunatokea haja kwamba sasa tuondoe mambo tuyapeleke Mombasa, hiyo iko tayari hapo.

President's parents; hiyo tutaiangalia kama mtu anapigania urais lazima wazazi wake wawe ni Wakenya. Awe amefanya kazi hapa kwa miaka kumi; hiyo ni sawa.

Ministers walioiba pesa; ukiangalia upande wa public finance, temesema kama mtu amepatikana na corruption kama hiyo, kwanza ni zile pesa zipatikane. Ile mali aliyoiba ipatikane halafu ndio sheria ifanye kazi yake.

Investment; wale wanafanya inteferance na small businesses hizo ni mbinu wanafanya. Sheria zipo tayari. Hairuhusiwi. Kama ni foreign investor, kwanza kuna Investment Board inaangalia ile kazi yako ambayo unakuja kufanya. Sheria ile ya Investment Board ni kwamba huwezi wewe foreign investor utoke Italy uko uje uweke kiosk. Kiosk ni cha mwananchi. Haiwezekani kwamba utoke Italy huko uache kazi zako sote uje ufungue kiosk kwa barabara. Hiyo, it defeats even the sense of being a foreigner. Lakini sasa wanafanya kwa sababu ya corruption. Wanaingilia haya kwa sababu wanajua yale mambo ni rahisi kufanya. Lakini sheria tayari zipo.

Citizenship; Registration Board tumesema pale. David kesi; we umesema kwamba national currency yataka iwe na pich ya mzee Kenyatta. Sisi twasema isiwe na yoyote.

Moral corruption – kwenda uchi- hili ni swali lilileta utatanishi sana. Tulikuwa tumeweka kwamba kuwe na dressing code lakini kina mama wakalia sana kwamba saa nyingine tunawaonea sana. Kwa hivyo, bado tunalijadili swala hili. Kweli rape saa nyingine huwa inakuwa encouraged na zile nguo ambazo mtu amevaa. Utakuta kwamba kina mama wengine kwa bahati mbaya huvaa nguo ambazo ni very transparent halafu mnajua wanaume nao ni hivyo. Mwanamme wa kawaida akiona vitu kama vile lazima ataanza kusisimuka damu yake, halafu wengine huwa wanafanya mambo mengine. Kwa hivyo hilo ni swala ambalo bado tunaliangalia.

KWS na mambo ya bahari; sasa itakuwa KWS hawawezi kufanya mambo bila kuzungumza na serikali iliyoko pale. Kwa hivyo si sheria blanket. Ni lazima tuseme local resources zi-benefit wananchi wa pale.

Land, kuhusu minerals, kwamba yakipatikana madini katika ardhi isiwe ni ya serikali, hiyo tumeandika wazi. Ndiyo section ya mwisho ya hiyo Article ya land. Section 238 imesema wazi kwamba, 'minerals zozote zitakazo patikana ni za mwenye ardhi'. Ikiwa atakubaliana na serikali na Kampuni ambayo itakuja kuchimba madini yale hiyo ni shauri yake. Hiyo tumeandika.

Private schools ziondolewe, hilo ni jambo jipya nitakwenda kuliangalia. Elimu ya Chuo Kikuu ni ya wananchi wale matajiri. Kwa kweli hapa infact tumeona elimu ya Chuo Kikuu wanaokwenda sana ni wananchi maskini. Wengi ndio wanokwenda maanake, kwa bahati mbaya si matajiri wengi ambao watoto wao wanapita mitihani, kwa bahati mbaya. Sijui Mungu hakupi kila kitu. Pengine tuseme kwamba kila jimbo lipate quota yake au kila jimbo- wengine walisema jana- liwe na Chuo Kikuu. Itakuwa sasa ni urahisi zaidi; lakini hao matajiri wasikutie wasiwasi sana. Kwa private universities ndio wenyewe lakini public wengi tumesoma huko ni maskini kabisa. Hata colleges ziwe na quotas hilo ni pendekezo nzuri.

Citizenship kama vile nilivyoeleza kwamba I.D na passport sasa si kitu cha favour kile sasa ni lazima.

Security police recruitment; sasa serikali ile itakuwa ya capital ya Nairobi, itakuwa na uwezo wa ku-recruit askari lakini wananchi, district iko na uwezo wa ku-determine who to be recruit. Kwa hivyo itakuwa sio kama vile mnalalamika kwamba

wanakuja hapa wanawapeleka mbio mchakamchaka halafu anachukuliwa mmoja au wawili. Hilo tumelisikia kila mahali.

Ombudsman yuko. Bwana Rodgers alikuwa amechelewa nafikiri mambo aliyouliza tumeyajibu karibu yote yako. Public defender ndiyo hiyo Ombudsman yuko

Transparent ballot boxes ziko, election acrobatism, hiyo ndiyo ambayo hatujaiandika ile habari ya mtu kupigania kiti kulingana na vile vyama vingi. Akikosa kule yuaenda kule.

Draft bill, what guarantees against impediment, nimeeleza kile mwanzo haukuwa kwamba tukitoka hapa twaenda national conference halafu ndio inaenda bunge. Kwa hivyo ni wall ndio wataamua.

Sasa free and fair elections hata hiyo imeandikwa. Civic education hamjalipwa; hata sikuwa sijui kama hamjalipwa, kwa hivyo muone District Coordinator.

Parliamentary committee to check on tenderers, hiyo iko- Public Investments, Public Accounts Committees. Ni ile kwamba huwa zinachukua muda mrefu.Kwa mfano saa hizi nafikiri kuwa ripoti yao ya 1996/ 1997 ndio wanaangalia. Sasa mwka ujao pengine tutpata ya 1998. Sasa tumesema kwamba ziwe ni regular badala ya kwamba miaka mine mitano hivi iliyopita.

Employment; is it guaranteed? Hatukutoa guarantee ya employment kwa sababu inategemea hali ya uchumi pale ilipo lakini takasema mambo yakiimprove sasa ni local government yenyewe ndiyo itaangalia.

Pensions; hilo ni swala ambalo ni kweli hatukuliandika, mishahara ya wale wafanya kazi ikiongezeka inastahili ya wale retirees pia iongezeke. Maanake tumetoa haki za wazee. Haki za wazee tumesema kwamba waendelee kuishi hali nzuri kama walivyokua wakifanya kazi. Sasa indirectly inamean kwamba lazima iongezwe. Lakini tutaieka wazi sasa.

Halafu kuna wanawake kuoana, hata hilo ni swala ambalo sasa itabidi tuiiandike wazi kwamba si ruhusa mwanamke kwa mwanamke, mume kwa mume. Maanake imeleta matatizo mengi sana hiyo.

William ameeleza kwamba Police services wana corruption sana na tumesema kwamba hiyo corruption na mambo ya police sasa yatakuwa wananchi wanaangalia. National union tumesema kwamba salaries tumeunda Tume ya Mishahara. Tume ya mishahara kazi yake moja ni kuharmonise kwamba mishahara yote itakuwa fair kulingana na ile kazi inayofanyika.

Rais awe amefanya kazi kwa miaka kumi hiyo ni pendekezo zuri.

NSSF tumejibu pale mwanzo apatiwe mwenyewe mwananchi kama anataka.

Foreigners and land tumesema ni increase land rates hiyo ni vizuri lakini tumesema tunawapokonya absolute ownership tunawapatia lease peke yake

Halafu Mama Maria anaeleza habari ya chokora, haki zao hatukuzitaja waziwazi lakini tumesema kwamba sasa ni jukumu la serikali kuangalia watoto wote. Halafu pili tukasema kwamba watoto wote ni lazima waangaliwe na wazazi. Mzazi mume na mke wote wanajukumu kuhusu yule mtoto. Halafu tukasema mtoto wa nje ya ndoa, wa ndani ya ndoa aliyeaachwa na mamake, aliyekufa na ukimwi aliachwa na nini asiruhusiwe kunyimwa haki zake.

Drug abuse, nafikiri sheria ziko, ni ile tu kwamba zinakuepa maanake ni kweli ulivyosema, ni matajiri wanaofanya mambo haya mtu kama mimi siwezi kufanya mambo ya drug trafficking lakini wao wako na pesa zaidi hata za kuhonga askari kwa hivyo ni vicious cycle inaendelea. Lakini sheria ziko, na wale ambao hushikwa wanapatiwa adhabu ya kutosha.

Haya round ya mwisho sasa. Nataka kuchukua wengine na wewe umeshazungumza. Haya, sawa lakini ujue kwamba tumeshaandika hiyo kwamba awe resident wa ile area, awe na mali area ile sasa huwezi kuwa na mali ikiwa umekaa mwaka mmoja. John hatujaandika direct hiyo miaka lakini hizo conditions tumeziandika. Kwa hivyo unavyosema tuandike miaka fulani tutakwenda kuangalia. Sawa haya. Kuna mama kule nyuma. Wainua mkono ama bado hujaamua? Umeshazungumza ama bado? Bado haya, wewe utakuwa namba one, halafu huyu mzee hapa namba mbili, na mtu ashike namba yake vizuri. Haya nimemaliza upande huo. Nakuja kwa rasta man hapa, namba three halafu namba four, halafu wa mwisho wewe utakuwa namba five. Mzee mwenye kofia karibu na mama six.Bwana ushazungumza, nyingi nyote mshasema. Tuaangalia wale bado-demokrasia. Haya namba seven nyinyi mtapata surwa kama hamjasema baadaye. Namba nine yule wa kule mwisho, where is another mama is number ten. Wewe umeshasema bwana, bado, haya namba eleven huyu hapa. Wasema huyo hapo nyuma, halafu huyu namba twelve. Tuchukue hao halafu tutaongeeza hao wengine ambao mikono yao iko juu. Mpaka kila mtu atoe maoni yake. Namba moja. Mama njoo hapa. Wale ambao wamepata namba wasongee hapa karibu ku-save time, na hiyo microphone yenyewe haifiki mbali. Majina yako.

**Ms. Zainab:** Majina yangu naitwa Zainabu Kalama Mgela. Mimi mwenyewe sikusoma na sijui kuandika na mimi nimefiliwa na mume na kutokea afariki ndio miaka kumi na tatu, na sikusoma. Lakini watoto wangu nimechukua jukumu mwenyewe nawasomesha. Na sikwandikwa na mtu kwa sababu sikusoma. Najiandika mwenyewe – nafanya biashara ya makoti.

**Interjection:** Wasemaje.

**Ms. Zainab:** Nataka kila Mkenya apate haki kulingana na vile ilivyo, aliyesoma na asiyesoma. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Mama andikisha hapa. Namba mbili.

**Mr. Mweni:** Kwa majina naitwa Masha Mweni. Mimi ninazungumzia upande wa wajumbe. Kwa kuwachagua, tumeambiwa itakuwa siku ya Jumanne ya kwanza kila mwaka mwezi wa nane. Na kuna Nyumba mbili za kuchaguliwa; Parliament and Lower House. Sasa, sijui mwongozo gani utatumika ikiwa ballot boxes zitakuwa pamoja. Kwa mapendo yangu mimi, ningependa zikatofautiana wakati wa kuchagua hasa – ikawa kuna siku mbili.

**Com. Swazuri:** Namba tatu. Jina lako

**Bw. Kithi:** Habari ya leo wazalendo wenzangu? Kwa jina naitwa Denis Ngari Kithi. Nina maswali mengi lakini mengi yashajibiwa. Niliyonayo saa hii ni machache tu. La kwanza ni kuhusu private gangs. Kama leo hii nasikia kuna mashifta na kamjesh, Mungiki, Jeshi La Mzee. Ingekuwa bora gangs hizi zote ziwe demolished, kwa sababu zaleta maovu kwa jamii.

La pili, kama tujuavyo, knowledge is power. Dunia ya leo bila elimu mtu si chochote. Ingelikuwa bora universities ama National schools zijengwe kote huku nchini. Elimu iwe spread all over the country.

La tatu lahusu foreigners, hawa wazungu huwa wanadharau sana ngozi nyeusi, sijui ni kwa nini. Kwa mfano, juzi tulivyokuwa matembezini beach, tuliona kisa cha kuskitisha ndio, lakini chachekesha pia. Tulikuwa na rafiki fulani alikuwa na girlfriend yake wanatembea. Kukatokea Mzungu from nowhere. Akaenda akamgonga gonga kwa mabega yule msichana akamwambia she is good for …… Akatumia lugha chafu sana hapo, ambayo yaudhi. Mtanisamehe sana baba zangu na mama zangu na ndugu zangu. Alimwambia she is good for tomba tomba ikiwa yule girlfriend alikuwa na fiance au mume wake pale. Yule mume alipandwa na hasira akataka kuleta vita pale. Sijui watu kama hawa wanachukuliwa hatua gani.

La zaidi ni, Constitution Review Commission yetu ingekuwa bora zaidi baada ya tumejadiliana na wamejadiliana na Wakenya wote, hii Constitution isambazwe kote kwa kila mwananchi ajielewe yeye kama mwanakenya. Asanteni.

**Com. Swazuri :** Shukrani. Namba nne.

**Bw. Angore:** Kwa majina naitwa Mbitha Mole Angore. Mimi nina hivi kuhusu huyu Rais. Kama anachagua ministers wake, ni mtu ambaye ile ministry ameisomea. Na hawa magovernor wetu ambao watakuwa wanachaguliwa, tunataka mtu ambaye ni mtu mwenye heshima zake. Kwa mfano, si mtu wa kwenda bango huko au aonekane vichoronichochoroni.

Hawa investors wetu wanaokuja, at least serikali ichunguze kule waliokotoka, wako kivipi. Si mtu aje na vimillioni vyake vitatu hapa vina vishindo siku mbili tatu ashafunga. Huyo ashakwenda. Watu hawakulipwa na vitu kama hivyo. Halafu kuna vitu hawa watu wanaleta kutoka nje. Kuna kampuni kama vile Ramisi imefungwa, umesikia sukari imetolewa Brazil huko, kuna vitu kama hivi; mvinyo, pasta, maziwa, unaona zinafungwa kwa sababu mtu analeta vitu kutoka nje kwa bei rahisi, anakuja

anauzauza tayari.

Halafu kuna hawa wendawazimu hawa. Unakuta wengine watembea uchi. Sijui kama Katiba yenu mmewafikiria vipi. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Andikisha pale. Namba tano.

**Bw. Rajab:** Mimi kwa majina naitwa Said Rajab. Mimi naona kama Katiba ambayo iko under Yash Pal Ghai imependekeza kama Rais atangaze utajiri au vile mali yake anayoimiliki. Naona pia kama yuaretire, atangaze. Na si yeye peke yake. Pia hawa local government kama hao madiwani hao, mayors, mambo kama hayo. Katika MPs, ambao tunawachagua, naonelea ni bora kama, katika ule muda ambao watakuwa wamehesabiwa na serikali wahudumie wananchi wao, kama wakionekana kama wana matatizo- hawatoshelezi wananchi hao kwa njia bora, wafutwe au wananchi waweze kuwachukulia hatua kabla muda wao haujaisha.

**Com. Swazuri:** Hiyo tunayo.

**Bw. Rajab:** Okay. Jamaa mwenzangu hapa rafiki yangu anasema hawa wageni wakija wawe na share na mtu fulani. Ni naona ni afadhali ile pia iondolewe. Wasiwe na share yoyote hapa kwa sababu utakuta hawa wageni wakija, wanaingilia businesses ambazo kama kukodisha baiskeli, wanachukua hizo ambazo pia Mwafrika wa kawaida aweza kuchukua hizi vitu. Utakuta itafikia wakati watachukua hata na mikokoteni pia. Wheelbarrow watakodisha, na Waafrika watakuwa hawana kitu ya kufanya.

**Com. Swazuri:** Kwa hivyo wasifanye biashara yoyote?

**Bw. Rajab:** Kwa hivyo wasifanye biashara yoyote. Ni hayo tu. Shukran.

**Com. Swazuri:** Namba sita.

**Bw. Waiharu:** Bwana Commissioner nachukua nafasi hii, nashukuru. Sikusikia mkizungumza – hata kama sikuangalia Katiba hii vizuri – mambo ya parastatals. Sijui kama parastatals katika maandalizi yenu mmeivunja ama itakuwa ni parastatal ama itakuja kuwa katika ministry. Iondolewe kwa sababu hiyo ni ya wakora ambayo tuko nayo. Mtu akitoa fujo huko, akiiba, anapelekwa ingine na hakuna punishment amepewa. Kwa hivyo, mimi ningeomba hiyo mambo ya parastatals iondolewe, irudishiwe ministry kwa sababu maminister mmesema watakuwa na nguvu. Wawe katika parastatals, maanake hizo zote ni pesa za wananchi zinatumika huko na ukora mwingi ni wizi. Zikae na minister. Akifanya kazi mbaya, awe anashtakiwa yeye na mambo yake. Hilo ni jambo la kwanza.

La pili ni mambo ya VIP. Sikusikia katika mjadala wenu mambo ya VIP vile vile, kwa sababu nao pia wanachukua jukumu la ukora. Wakitoka airport wanabeba drugs kwa sababu VIP wanapita tu bila kuangaliwa alichobeba. Sijui katika maandalizi yenu mmefikia wapi habari ya VIP- watakuwa na cheo gani na madaraka gani isije wakawa wanaleta madawa hapa kuletea watoto wetu. Wanaharibika vichwa hapa na ni VIP hao, watu wakubwa wakubwa, wenye matumbo kubwa ndio wanaleta hizo drugs. Hilo ni la pili.

La tatu ni hili janga letu la HIV. HIV imeleta janga kubwa sana na sote tunajua. Sasa, imefika kiwango kuwa watu wanakufa sana hata hospitalini. Wakilemewa sana – na wengine ni yatima – unaitiwa watu wenu unaambiwa "pelekeni hawa nyumbani." Sasa ukiitiwa huyu umpeleke, baba amekufa, mama amekufa, labda hata ni ndugu yako unaitiwa, ama labda ni wanyonge zaidi na hawana watu wa kuwasaidia nyumbani. Wewe wachukua maiti tu uende nayo nyumbani. Ni nani atasaidia katika hali hii? Mayatima hawa wawe wakishugulikiwa zaidi na serikali kuliko vile inakuwa ni jukumu la wananchi kushughulikia nao.

Parliament: Sijui sasa, ikivunjwa katika hii Katiba tuliyo nayo, kwa kuwa President angali ako na hizo powers, hii sasa itafanya kazi lini? Hiyo nayo tungetaka kujua kwa sababu tunasikia ni mzuri sana lakini yatatiza kwa sababu watu wengine wanapigania isiondoke ndio wawe na nguvu, na tungependa hii ifanye kazi.

Ya mwisho ni foreigners, kama vile ilivyotajwa. Tumejifunza mengi hapa kwetu Malindi. Wanakuja na ujeuri mwingi sana. Hawatuheshimu sisi wananchi wenyewe. Anakuja anashikana na tajiri, anakuwa kama ni partner wake kwa upande mwingine, lakini raia wa kawaida, hata ukizungumziwa unaambiwa, "wao wako hapa mfukoni". Hata tushawahi kuambiwa, kama Muitaliano- na sitaki kuzungumza kama tunawadharau. Tunawapenda. They are tourists and we like them, but they really ignore us- wanasema, kama ni polisi, "ako hapo mfukoni" Hakuna mahali utampeleka. Kwa hivyo, katika Katiba yenu, tungetaka kujua kama mtalinda wananchi kwa njia gani kwa hao watu watukutu na wanaojidai. Thank you.

**Com. Swazuri:** Andikisha. Namba saba.

**Bw. Kithuku:** Asante sana Bwana mwenyekiti. Kwa majina naitwa Stephen Kithuku. Yangu ni machache. First and foremost ningeongea juu ya hii jambo ya free market. Ninaomba kwa ile serikali ambayo tutakuwa nayo hii soko huru iondolewe ili tuweze kuwa ns stabilized prices of all the commodities in Kenya- stabilized control kama chumvi yote yauzwa shilingi tatu, hata Kakamega iwe inauzwa shilingi tatu.

Second, kama mtu kwa mfano ni daktari asiruhusiwe aweke clinic. Aruhusiwe tu aweke wakati ata-retire. Lakini for the duration he is serving as a doctor he is not supposed to invest or establish a clinic. Na pengine aki-establish basi ni makosa na achukuliwe hatue.

La tatu. Sijasikia bwana mwenyekiti what the qualification for the Prime Minister will be and also what the level of education for the councillors will be.

The second one is Bwana mwenyekiti I still instist on the type of dressing. Tukiangalia kwa upande wetu sisi wakristu it is very much condemned in the Bible that our women should wear zile nguo ndogo. They are not supposed to be short. Sasa kama Biblia inakataa Bwana mwenyekiti, kwa nini na sisi kwa Katiba tusikatae? Basi kama hatutakataa kwa Katiba tutakuwa tunaenda against God's will. Because the Bible says hatutakiwi kuvaa nguo short. Basi na hii tabia ya kuvaa nguo fupi ndio inakuja kusababisha tuwe na huu ugonjwa wa Ukimwi na tutazidi na itakuwa lawama kwetu na Mungu atatuhukumu vibaya. Kwa hivyo we still insist on that. Hata wakisema tunawaonea hatuwaonei. Mungu ndiye alisema wavae nguo ndefu sio sisi.

Another one ni follow up ya acquiring of wealth. Vile watu wameacquire wealth zao. Tumejua for the forth coming Government, hao watu watachunguzwa kila mtu amepata mali namna gani; na pia wale ambao wameinvest huko nje walazimishwe na Government walete hizo pesa hapa halafu wakishaleta hapa waambiwe invest, let that be the law. Walazimishwe wainvest hapa ndiposa waandike wananchi na wakishaandika wananchi half of 100% what they are going to get, 80% iwe distributed kwa wananchi na yeye apewe kama 20%. Because all that investment has been helping the overseas people. Kwa hivyo kama inawezekana ile share kubwa akishainvest hapa kwanza aandike wananchi wa hapa, secondly ile profit atapata almost 80% iingie kwa Government halafu 20% apewe.

Ile ingine na ndiyo ya mwisho ni hii ya presidential escort. Hiyo sitaongea sana, ni kitu kidogo I just wanted to mention. Tumesikia sana wakati Rais anaenda nje anaenda na Wajumbe wengi sana Bwana Mwenyekiti. Tunauliza kama inawezekana aendeyeye and the Minister of Foreign Affairs and his P.S. Only those. Hatutaki watu wengi maanake they are misusing the government money. Thank you.

**Bw. Agung'a:** Ahsante sana. Kwa majina naitwa Alfred Agung'a. I have one question to put across. The question is concerning the District Governor. We find that in the new Constitution which has been drafted, it emphasises mostly on national income and the resources of the nation rather than national unity. Kile ambacho nauliza; ni kitu gani Constitution yetu inafanya ili to put in place that all people staying in one region are unified. That's my first question.

Second is the freedom of ownership. You have tried to explain it but it has not reached home properly. Because when you say that freedom of worship provides that you have a worshipping centre where you don't interfere with others, my question is, is devil worship allowed? Because you are worshipping in your room and you worship the devil. Is it allowed in the Constitution? Thankyou.

**Bw. Kalama:** Jina langu naitwa Steven Kalama. Swali langu ni kuhusu umri uliowekewa wasichana, miaka ishirini kuwa

hayuko chini ya sheria anaweza kufanya atakavyo hata kama ni kinyume cha sheria ya ndoa. Hawezi kuadhibiwa, na mwisho mzigo huo unamlemea mzazi na ukienda kwa serikali unaambiwa utakua mwenyewe na binti yako. Hakuna mtu atamwadhibu- binti yako na chaguo lake. Si hivi ni kudimisha umalaya na chokora kuongezeka? Je Katiba imepanga vipi kwa sheria hii? Na kama bado naomba sheria hiyo, sheria ya ndoa idumishwe katika Katiba. Atakaye enda kinyume cha ndoa msichana ama mvulana aadhibiwe. Ni hayo.

**Bw. Karisa:** Kwa majina naitwa Emmanuel Karisa na niko hapa kama shirika la Table Banking Association. Nataka kuchangia mambo matatu. Jambo la kwanza ni kuhusu hotel industry. Imekuwa kuna mtindo sasa wa hawa investors. Wageni wanalipa wakiwa kwao, wanaiita 'all inclusive.' Mgeni akiingia Kenya amelipa pia maji ile utakunywa hapa Kenya. Sasa hiyo imechangia umaskini kati ya wale watu wanaokaa Malindi. Utapata wakati wageni walipokuwa wanakuja na pesa wananunua watu wengi walikuwa wanafanya biashara, lakini sasa mpaka uwe na tender ya kuuza mali yako kwa hoteli ndio utafanya biashara. Zile pesa zao wanalipia kwao na pia serikali inakosa ushuru kutoka kwa pesa ambazo wangetuletea hapa kwetu.

Na jambo la pili ni kuhusu barabara- infrastructure. Kutokana na experience niliyonayo kidogo, umaskini mwingi hapa Kenya ni kwa sababu ya ukosefu wa barabara. Watu ambao wanaishi mashambani ndani kule huwa wana shida ya kusafirisha mali zao kuja kuuza Malindi town ama kupeleka mahali kwingine. Kwa hivyo ingekuwa serikali ama Katiba ingeingilia kuwe na mpango, sehemu zote za Kenya ambazo hazina barabara- hata kama si lami- iwekwe lakini iwe kuwa itawekwa murram ili uweze kusafirisha mali yako kuleta na wale wanapatikana na magonjwa kule kama ni usiku awe anaweza kuletwa haraka hospitali. Tunasikia watu wengine wanasema kuwa barabara zimetengenezwa huko Baringo ambazo mpaka zinaanikwa Mahindi na ni lami. Hakuna magari yanaenda, na kule kuna watu ambao wana shida barabara hazitengenezwi. Kutoka hapa kwenda Marafa inaeze kuchukua 20 minutes lakini kwa ile hali ya barabara unachukua almost 2 hours kufika Marafa. Kwa hivyo katiba iangalie mambo ya barabara.

Jambo la mwisho ni kuhusu tax – VAT. Zamani, wakati wa Mwingereza watu walikuwa wakikata kodi ambayo kuwa ulikuwa ukilipa shilingi kumi, ilikuwa ni shilingi kumi mwaka mzima. Sasa serikali ikaja ikageuza ikasema hakuna kodi lakini sasa imeleta tax- VAT. Ukienda ukinunua kitu ambacho kinaku-cost sumni, umechangia serikali. Ukinunua kitu cha shilingi mbili serikali imepata. Na hii pesa, VAT sijui kama katiba imepitia hapo kuelezea kama pengine inasaidia nini sana kuhusu maisha ya mwananchi kwa sababau hiyo collection ya VAT kwa mwaka mzima serikali inatengeneza pesa nyingi sana, na inabaki mwananchi maisha inakuwa magumu kwa sababu huwezi kununua kitu cha shilingi tatu ambacho, ingekuwa hakuna VAT ingenunuliwa kwa shilingi mbili. Kwa hivyo hii mambo ya taxation pia ningeomba Katiba ya sasa ichunguze sana.

**Ms. Chipande:** Hamjamboni wananchi. Kwa majina naitwa Mama Elima Chipande. Mimi hapa nitachangia kuhusu hawa wanaokuja katika mahoteli. Tuseme kama kuna hawa watalii ama yeyote anayetoka nje, huwa ana hoteli hapa. Yeye ana nyumba private, huyo huyo anavibanda huko Pwani. Yeye tena atakuwa na maduka kila aina. Mtu huyo mmoja anapewa kazi nyingi na malicence, hali hapa raia anatafuta na hapati. Akienda anaambiwa hapana huwezi kuanzisha kitu hiki. Kwa hivyo

naomba Katiba mpya iangalie hasa hapa Pwani kuhusu jambo hili.

Na jambo lingine ni kuhusu ugonjwa uliozuka ambapo kule hospitali kwasemekana kuna dawa za kuwasaidia lakini unakuta wanarudishwa majumbani huna dawa yoyote. Ukienda kule hupati, unaambiwa ni ghali au vipi. Nafikiri serikali yetu ingejaribu kuchunguza jambo hili pia na kuweka madawa haya yawe free kwa watu kama hawa, na pia kusaidia wale mayatima.

Jambo lingine ni kuhusu wendawazimu. Ijapo wametajwa, lakini mara nyingi wanazurura ovyo na tuna health officers, kuna hospitali zao pia. Sijui kwa nini hawawachukui na kuwaweka mahali kama pale na kuangalia hali zao. Huwa wanatembea njiani ovyo ovyo, wanakula vitu vichafu na pia saa nyingine hata nguo hawana, na serikali iko hapa hapa inawaangalia tu. Tunabishana nao na wengine ni ndugu zetu, watoto wetu. Ningependa pia, serikali mpya itakapochukua jambo kama hili liangaliwe zaidi. Sina mengi ni hayo tu. Ahsanteni.

**Bw. Oroni:** Ahsante sana Bwana mwenyekiti. Mimi swali langu na nitafanya haraka sana ni mliaddress issue ya religion ambao Waislamu watakuwa katika judgement wana Kadhi wao. Sasa wakati wengine unaona kuna intermarriage. Katika intermarriage utaona Charles ameo Fatuma. Sasa katika judgement ikiwa wao wawili wanaenda kortini, sasa kesi itaamuliwa kulemea wapi? Kwa sababu ukiangalia Fatuma, yeye msingi wake ni dini ya Kiislamu. Pengine sasa kumetokea divorce, akienda nyumbani ataenda kushtaki. Sasa yeye atasikizwa na hiyo mila ya Kiislamu ama atasikizwa na mila gani? Hilo ni swali langu la kwanza.

Halafu kuna hii mambo ya religion pia ambao kuna kipengele moja ambao hakinipendezi, katika nchi yetu kuna breach of peace. Utaona wakati mwingine tumelala na mwenzako pengine in the name of preaching or in the name of anything, yeye anakupigia kelele. Hii Constitution mpya ita-address hii issue vipi? Watu watakuwa unapigiwa kelele na huna mahari pa kulalamika ama hii Constitution mpya itaangalia hili jambo, la kwamba mtu akilala ni alale na awe na peace.

La tatu, katika education system ya Kenya, kuna mabadiliko mara kwa mara, na hii haipendezi wananchi kwa sababu mnaingia expenses. Mara unanunua kitabu hiki na kesho yake unasikia imechange system ni nyingine. Hata hapa system ya education ama the type of education we need itakuwa inaangaliwa na board gani? Ni nani ataangalia kama education tunataka Kenya hii ni hii, na itadumu kwa miaka ngapi ili tuwe na nyingine?

Halafu katika issue ya accidents, katika nchi yetu these accidents zimekuwa nyingi na tunajua ni kwa sababu ya reckless driving na mambo mengine lakini sasa katika Constitution hii mpya tungetaka iwe addressed vizuri ama ingawa ajali haikingiki lazima tu-take precautions.

Ya sita, wakati mwingine utaona watu wengine wanaruhusiwa kutembea na silaha, sasa anasema ni mila yake- ana panga ambalo limenolewa. Kwa mfano kuna ndugu zetu Wamaasai, unaona wanatembea na rungu, wanatembea na silaha kali kali.

Lakini ukiuliza unaambiwa kwamba hao ni mila yao. Sasa hii mambo ya utamaduni namna hii watu wanatembea na silaha na ni mila itaisha lini?

Halafu katika mji kama huu wa Malindi kutakuwa umejengwa vizuri. Pia hakuna mahali unaweza kustarehe, kwa sababu sisi katika nchi yetu tumefika kiwango sasa mtu anataka kustarehe, unataka mahali ambapo kuko wazi ambapo unataka kuketi na familia yako, ambapo kuna swimming pool, ambapo kuna miti mizuri imepandwa na eneo kubwa ambapo unaweza kutembea na kuona wanyama. Issue kama hiyo hakuna, ni magorofa yanajengwa, mengine yanajengwa juu ya choo. Hii issue ya recreation, mmeiangalia katika Constitution?

Pia lazima tu-address haya mambo ya usafi. Vile tutaishi katika nchi yetu na usafi. Utaona kwamba kila mtaa utaonaona maji machafu yakitiririka, watoto wakila vitu vichafu na hatupandi miti mizuri ya kuvutia haya mambo ya usafi. Kwa hivyo haya mambo ya usafi ningependa yawe addressed vizuri.

Na mwisho ni kwamba mambo ya Rais ni vizuri kwamba mmepunguza powers zake. Lakini mimi ningependa rais ambaye atachaguliwa katika nchi hii awe pia historia yake ifuatiliwe mpaka chini, mpaka alipokuwa nursery. Alipokuwa nursery alikuwa anafanya vituko gani. Yeye amewahi kurape, kuua mtu, kunyang'anya mali ya mtu mwingine ama yeye anakuja anasema mimi nataka urais kwa sababu ana Pajero mnasema kwamba huyu kweli anafaa kuwa rais kwa sababu anaweza kuzumgumza vizuri na nyinyi. Hiyo iwe ya mwisho lakini nilikuwa na nyingi. Ahsanteni.

**Bw. Njenga:** Mimi ningependelea kuchangia swala la Katiba mpya ambayo imefanyiwa marekebisho mengi na itakuwa na marekebisho imerekebishika. Ningependelea serikali ikishirikiana na chama kinachoshughulikia Katiba watafute siku na muda angalau unaopata nusu saa kwenye redio angalau siku moja kwenye Kiswahili, maanake kuna wananchi wengi wa Kenya ambao hawakusoma na hawajui Kiingereza, wapate kuelezwaa ile Katiba angalau kipengele kimoja katika hiyo nusu saa ili wananchi wapate kujua Katiba yao iko namna gani.

Swala lingine ni kuhusu lugha viongozi wote wakihutubia Bunge, mikutano yote ya hadhara iwe lazima uzungumze Kiswahili kuchangia swala hilo hilo ambalo wengi wafahamu lugha nyingine zaidi ya Kiswahili, kutokana na ukosefu wa elimu ya kutosha.

Na kitu kingine ni kuhusu hii pension ya rais, haswa huyu Rais Moi. Tunafahamu kwamba amekuwa kwenye power zaidi ya miaka arobaini. Sasa ikiwa miaka hiyo yote amekuwa ni mtu ambaye sio chini ya Mbunge pesa hizo zote amekuwa anapata na apate pension ambao inapitishwa apewe kwa sasa huwa ni pesa nyingi sana, na je hao marais watakaokuja watapewa pension kiasi gani hicho ama ni vipi. Hata kama ni kupewa hiyo pension ipunguzwe maanake ni nyingi. Kulingana na vile ninavyojua ni pesa nyingi sana, hizo ilikuwako imepitishwa apewe. Kwa hivyo hilo ni swala linatakiwa lishughulikiwe zaidi. Ni hayo tu.

**Bw. Mboobu:** Ahsanteni. Swali langu la kwanza ni kuhusu hukumu. Mtu anaweza akafanya kitendo kibaya, uovu na

akapelekwa kotini na akapatikana na hatia, lakini tunapata hapa hukumu, yule hakimu anamwambia ninakuhukumu kifo. Tumeamua kwamba ufe. Tuona kwamba hukumu hii ni ya Mungu wala si mwanadamu. Kwa hivyo mimi maoni yangu ama nilikuwa nauliza kama hii constitution mpya inasema kuna hukumu ya kifo au imesema nini kuhusu hukumu kama hii. Ahsanteni.

Jambo lingine lilikuwa linahusu urithi. Mtu anaweza kuwa anafanya kazi kama mimi na baadaye Mungu ananiita nyumbani mapema. Ninaacha familia- mke na watoto,- je basi ikiwa nimekufa, niko kazini kuna zile pesa zangu ambazo napaswa nilipwe. Kwa wakati wa sasa inachukua muda mrefu sana. Mtu anatafuta hizo pesa kwa miaka mingi na hata ameacha watoto wadogo, wanataka kusoma kwa zile pesa na zinazuiliwa kwa miaka mitano au kumi. Hawa watasomeshwa namna gani? So, hii utaratibu ama masheria tunazoongea hapa zimesema nini kuhusu jambo hili. Mimi ningeomba kuwa huu muda wa kutoa mapato kama haya ufanyike mapema sana ili yule aliyeachiwa wale watoto wa yule mke au mume na bado wazazi wazee wapate na kuzitumia kwa wakati unaofaa.

Jambo lingine kuhusu huo urithi tunaojua kuna huo utovu wa nidhamu wa wanawake na wanaume lakiini nasema hivi kwamba mimi naweza kuwa na mke wa kinyumba, unaishi naye, hakumuoa, hakupeana chochote na baada ya kuishi naye kama miaka mitano au minne uzae naye mtoto mmoja au wawili, wewe ufe, unafanya kazi, una wazazi na ndugu zako wadogo ndio unawatumikia lakini huyu naye amekuwa pale. Hukumlipia chochote, hajulikani pale na watu hapo nyumbani. Sasa wewe umekufa, mazishi na gharama zote zimefanywa na watu hapo nyumbani, baadaye yeye anasema mimi nataka ule urithi wa bwanangu maana nimeishi naye miaka mitano. Nataka niulize, hizi sheria zasemaje juu ya jambo hili? Maoni yangu ni kwamba mtu huyu ameingilia kama bibi amekosa adabu kwa huyo ambaye amekufa. Kwa hivyo anyimwe ama ile jamii ipewe zile pesa iamue kama alikuwa akiishi nao vizuri watamsaidia kama alikuwa mkorofi amekaa na huyo bwana mbali ya ghala kwa miaka mitano, na huku hupatiwi chochote na umekufa, amekula haki yake, haki iliyobaki ya wazazi. Ahsanteni sana. Hayo tu ndiyo yalikuwa maoni yangu.

**Bw. Mlewa**: Habari zenu. Kwa jina naitwa Edward Mlewa. Kuna haya mambo mengine ya kununua unga, mara sukari, mara nyingine bei hupanda bila notice kwa wananchi. Mara unasikia unga ilikuwa shilingi arobaiini, mara shilingi ishirini, sijui hii katiba inatwambia nini kuhusu hii control.

Na lingine ni kuhusu hii serikali ambayo bado iko kwa mamlaka, ambayo inasema haitaki katiba ina unafiki. Je mimi mwananchi naweza kupewa uwezo gani ili kumpinga huyu Rais Moi asiweze kunishinda mimi mwananchi, katika hii Katiba inayokuja, kwa sababu Moi anataka kuipinga. Nami nataka kumpinga kwamba asiipinge. Nyengine ni kwamba, Wabunge wanatafuta kura kwa maneno matamu. Hata hii serikali inayokuja mpya inatwambia maneno matamu pia najua. Lakini mtu akiingia katika kiti tu hata ukienda tafuta msaada atakudharau, na mimi nitakuwa nikitumia hii Katiba mpya. Je ikiwa kama ni Mbunge, na amedharau hii Katiba mpya na uwezo gani kumfuta tena pale, ambapo mimi nitamwambia toka. Je mimi nitatumia kibali gani mpaka nimwonyesha kuwa nina uwezo. Maanake kama kura ya maoni, kunatakikana kuwe na baraza fulani la wananchi. Ahsanteni. Ni

hayo tu.

**Bw. Nyambu:** Nashukuru kwa kupata nafasi hii. Sina mengi, ningalichangia jambo moja hivi kulingana na Katiba mpya ambayo kwamba tunaikadiria kuifanyia uchaguzi. Ambalo nalalamika nalo ni la karatisi ya kumiliki ardhi. Wakati wake uliowekwa ni mwingi sana ambapo kwamba hakuna mtu anayefikia miaka tisaini na tano hapa. Itakuwa kama mtu umempa urithi huo na mababu zake. Kwa hivyo, nalalamika nalo ni hilo moja tu, kama kuchangia. Sina zaidi. Ipunguzwe. Kuanzia 40 kurudi chini.

**Bw. Mwamrima:** Mimi nataka kuchangia kuhusu huu utawala wa vijijini. Elimu ya Mbunge imeonyeshwa lakini ya wale waakilishi wa kijijini haikuonyeshwa na yule atakaye wakilisha location vilevile haikuonyeshwa.

Tukifikia District Government tunaona kwamba kuna waakilishi ishirini hadi thelathini, lakini hata hivyo wale ishirini au thelathini hawakuonyeshwa watakuwa wanawakilisha maeneo gani wa district kutegemea na ukubwa wa eneo lao. Lakini haijulikani yule mmoja ili kwenda kuunda lile baraza la wilaya atakuwa anachaguliwa kutoka wapi mpaka akawe katika wale ishirini, na elimu yake yule district administrator, vile vile haikutajwa.

Kwa hivyo kwa maoni yangu mimi ninasema kuanzia wale wawakilishi wa vijijini wawe labda na elimu ya msingi, primary certificate. Yule district administrator kwa sababu atahusika hata kwenye utawala wa mkoa awe vile vile na elimu ya form 4, pass.

**Com. Swazuri:** Jiandikishe hapa. Haya mama Zainabu amesema yeye hakusoma na kadhalika. Katiba hapa imesema Wakenya wote wako sawa mbele ya sheria. Na tumesema hatutaki kubaguana. Watu wote wako sawa mbele ya sheria. Vile vile ambavyo watu wote wako sawa mbele ya sheria ya Mungu.

Uchaguzi : Bwana Masha amesema kwamba hajui itakuwaje kuhusu uchaguzi wa Lower House, Upper House na Wabunge na kadhalika. Tumesema kwamba sasa ile Electoral Commission, hizo ni details ambazo watatupatia. Haja yetu ni kuwa uchaguzi wa watu hawa utafanyika siku ile, sasa ni wao ndio watatoa huo utaratibu utakuwaje. Kulikuwa kuna mapendekezo ya kwamba uchaguzi wa kila aina ufanywe siku mbalimbali, lakini tukakuta gharama nazo pia huwa ni nyingi. Kwa sababu majibu tunajua area yetu ya Kenya ilivyo. Hata nikisema uchaguzi ufanywe siku ile moja kuna wengine siku hiyo ndio masanduku yanafika. Halafu majibu pia husikia yanakuja nyingine baada ya siku mbili au tatu kwa hivyo itakuwa ni kazi yao sasa hao kutoa taratibu maalum.

Private gangs: Kuna sehemu ambayo imeabolish private militias. Tumeziondoa, hakuna tena mambo ya majeshi haya ya watu binafsi.

Spread ya national schools; hiyo tutachukua, na universities ziwe kila mahali. Infrastructure itatengenezwa na serikali zile

tumeziweka za chini.

Wale wageni ambao wanatukana raia wa Kenya; basi hata ukipanda katika gari ya watalii saa hii, hiyo sheria iko. Wanaandikiwa kwamba waangalie mila na desturi za wananchi local. Lakini wengine hawafuati. Hiyo sheria iko tayari.

Kwa Katiba isambazwe Kenya nzima, hiyo ni nia yetu – tumesema itakuwa ni document ambayo iko accessible; Mashuleni, msikitini, malibraries – tumesema Katiba itakuwa accessible.

Governors; Wamesema kwamba, masomo yao kweli hatukuandika. Wawe ni watu wa kuheshimiwa. Tutaandika hayo masomo yao.

Investors; tumesema sheria iko, kwamba waangaliwe pesa zao walizonazo na kazi watakayofanya kabla hawajaja. Lakini wao huwa wanatumia njia nyingine, halafu wanaruhusiwa, kumbe wanakuja kukodisha baiskeli hapa. Haya.

Upande wa vitu ambayo tunavikuza hapa lakini vinakuwa imported; nafikiri hii sehemu ya agriculture tulikuwa bado hatujaimaliza wakati tunaandika huu mswada, bado utaingia. Wananchi wamelalamika kuhusu sukari, maziwa, mchele, siku hizi hata nyanya nazo pia zinatoka kutoka nje na hapa zipo, mayai. Ile free market ambayo tumesema. Kuna mswada ambao utaingia hapa kabla kwenda kwenye National conference.

Wendawazimu; sijui tufanye nini hapa lakini nafikiri hii sasa ni Idara ya Afya, ndio iko na kazi ya kuangalia hawa watu ambao wanatembea ovyo ovyo, wengine wako uchi na kadhalika.

Bwana Said amesema hata wale viongozi wanaostaafu wanaomaliza kazi zao- nao pia lazima waeleze pesa zao wamezipata vipi. Hiyo ni sawa tutaangalia mambo yake. Halafu akasema wageni wasiwe na share yoyote. Hapo tutakuwa tumefunga sana. Lazima tuwaruhusu lakini kwa sheria ngumu. Lakini ukisema wasilete kitu na sisi wenyewe hatuwezi, tutakuwa tumezuia tusifanye biashara.

Parastatals bado zipo, lakini tumesema, wale wakuu wake sasa watateuliwa na Bunge- Sio Rais kwamba atachagua. Atateua tu, lakini uamuzi utatoka kwa Bunge. Na zile parastatals ziko na Parastatal Reform Commission ambayo inaangalia zile zinawezekana, ambazo haziwezekani zinaondolewa. Lakini shida pale ni kule kuuzwa. Huwa zinauzwa kiholela.

VIPs: Tuseme VIPs ni wananchi wa Kenya, na kila mtu yuko sawa katika sheria ya Kenya.

HIV orphans – wale watoto ambao wazazi wao wamewaacha, nafikiri hapo tutaangalia kwamba serikali iwaangalie maanake kuna wazazi wengine wana watoto zaidi ya kumi, wajukuu kumi, kumi na tatu, wote baba zao na mama zao wamefariki.

Bwana mmoja akauliza itakuwa je ikiwa Bunge litavunjwa na Katiba hatujapitisha. Tumeeleza kwamba lengo letu ni kwamba uchaguzi ufanywe na Katiba hii. Ndio maana tunafanya hii kazi kwa conditions hizi za haraka haraka angalau tupate kuitumia. Lakini sasa uamuzi si wetu tena. Ni nyinyi na viongozi wenu wa siasa.

Free market –nafikiri tumesema hiyo, lakini tumependekeza kwamba tuwe na price control- standardized price. Hilo ni swala ambalo tutaliangalia, ingawaje wananchi wengi walisema itategemea mali yako unaipata wapi. Wengine wanaipata kwa rahisi wengine kwa ghali, lakini bado tunaliangalia swala hilo.

Halafu upande wa qualifications za Prime Minister. Prime Minister tulisema ni Mbunge, na tukasema Mbunge ni lazima awe Form IV pass. Kwa hivyo, hiyo yake iko. Nafikiri qualifications za councilor ambapo ni sawa na locational administrator ndizo hatukuweka, hiyo tunakubali.

Women dressing – kina mama mavazi yao; Mungu amesema kwamba wavae nguo ndefu, hiyo tutakwenda kuangalia.

Pesa zilizowekwa nje zirudishwe; huo ni mwito ambao umekuwa ukitolewa kila siku, kwa hiyo tutaenda tuangalie kama tunaweza kuweka sheria.

Rais; tumesema watu ni wengi ambao wanaenda kuandamana na Rais. Watu wengine walisema hata wale wanaoenda kumlaki pia. Utasikia kuna watu ishirini, sijui Mawaziri wameenda kumlaki, government yote imeenda kumlaki Rais. Watu wamesema hata wale pia, kama amekuja amekuja tu, ataonana na watu, sio lazima ulimwengu mzima uende ukamngojee. Watu wamesema hivyo pia.

District governor; anasema Bwana Alfred kwamba je tutafanya hakika gani kwamba serikali hizi hazitatufanya tuwe tunatengana. Principle ya kwanza kuunda hizi serikali za chini ni kwamba tuzingatie sisi ni Wakenya. Ndio muhimu. Uwe Mkenya kwanza ndio tuangalie haya mambo mengine.

Devil worshipping; nafikiri sasa tutaiweka wazi. Tumetaja pale lakini haikutokea. Kwa hivyo tutakwenda kuiweka.

Wasichana ambao wanatungwa mimba halafu wanaletwa nyumbani, kwa hivyo ndoa idumishwe. Kudumisha ndoa tumeitaja. Kuna Section ya Family pale kwamba ndoa ni lazima idumishwe, na tumesema kwamba wananchi wa Kenya warudi pale ambapo family ilikuwa ndio basic unit ya kuangalia maslahi yao. Kwa sababu siku hizi kama vile Bwana mmoja ameeleza, wale wanawake wazee wana weka wasichana wanasema wanamweka kinyumba- ile come-we-stay.Tunataka kuoondoka kidogo pale turudi kwa kama ni ndoa ni ndoa inajulikana, sio ile mipango mipango ingine ile. Kama hataki kuolewa basi akae nyumbani. Maana tumesema atarithi hata yeye.

Hotel industry- ile all-inclusive- watu wanalipa huko nje. Nafikiri ni mbinu zile zimekuja kwa sababu wizi ulizidi na corruption ikazidi. Sasa unakuta tukibeba pesa zetu mfukoni hivi tunanyang'anywa. Sasa afadhali tukalipa huko, hoteli hapa ndio tutaenda kununua maji. Sasa hapo tujilaumu sisi wenyewe. Kama tutapunguza visa kama hivyo, watakuwa hawana shida kuja na pesa hawa.

Barabara; sasa hiyo si shida tena- ni jukumu la district government na provincial government kutengeneza barabara. Sasa hiyo huwezi kuwalaumu ministry sasa. Hiyo yenyewe government ya chini ndio itaangalia mambo ya barabara.

VAT; kuna mjadala mkubwa sana uliendelea kabla ya hii sheria ya VAT kupitishwa, na kweli tunakubali kwamba wananchi wa Kenya ndio wanalipa tax nyingi zaidi, kwa hivyo hilo swala litaangaliwa.

Upande wa public finance, tumesema kwamba huwezi ku-impose tax kabla ya Bunge kuipitisha.

Halafu tena kuna maswala mengi kuhusu wageni ambao wanafanya biashara mpaka za chini za kukodisha baiskeli kukodisha mikokoteni. Kwa hivyo haya mambo tuyaagalie nafikiri ni vile tulisema hawaruhusiwi lakini wanatumia ujanja ule wa kwamba wanajua yule anayekata licence wakimpatia laki moja itakuwa ni basi. Lakini kwa kweli hawaruhusiwi. Maanake sidhani kama tunaweza kuruhusu mtu atoke Uingereza aje akodishe mkokoteni hapa.

Religion; Mwislamu na Mkristo wakioana. Kwanza ni wao wenyewe wataelenwa kama wataenda na dini zao ama mmoja ata-dissolve dini yake. Sasa hatuwezi kupisha sheria kwamba kuna Waislamu watakuwa na Wakristu sasa tutengeneze alternative wao wakiungana sheria itakuwa ni hii.Hapana. tumesema kila mtu ana haki ya kuamua dini gani atauata halafu ndoa ikifanyika itaangalia na ile maslahi ya dini ile.

Breach of peace; amesema kwamba kuna kelele. Tumesema kwamba dini sisifanye ili wengine wawe wakapata shida. Kama mnataka tuweke open hiyo tutaweka.

Education system: Ni kweli kwamba mnataka hapo hatukuweka education system. Watu wengi walisema 8.4.4 iondolewe ije ile ya zamani lakini hatukuiweka hiyo tunakubali, tutaenda kuangalia. Na isibadilike saa zote.

Ajali- accidents – zinatokea sana, lakini tumekuta kwamba kuna sababu kwa nini ajali huwa zinatokea sana: Magari mengine hayako katika hali inayofaa, lakini yanaruhusiwa kupita kwa sababu ya corruption. Corruption sasa tumesema ni hatia. Barabara nyingine hazifai kwenda magari tumesema sasa Districts zitaangalia, barabara.

Offensive weapons. Sasa kuna wale Wamaasai wanabeba mikuki na tunaambiwa kwanba ni culture yao. Sasa hapo sijui mnataka tufanye nini. Mkisema kwamba watu wote wasibebe silaha ya aina yoyote hapo tutakwenda kuangalia.

Lakini upande wa recreation nafikiri kuna mzee amesema kwamba mzee hujui utakwenda kaa wapi upumzike na watoto kwa sababu ardhi ile public recreation land zimeenda zote. Tumeshasema pale kwamba zitachunguzwa. Ambazo zinanekana kama zilichukuliwa kiholela zitarudi katika miaka miwili hii ijayo halafu tena ni jukumu la Government ile ya urban areas kuangalia kwamba wananchi wanapata vitu kama vile;

Clean environment sasa tumeweka katika Katiba. Ni lazima mwananchi wa Kenya aishi katika mazingira safi. Hiyo sasa ni sheria.

President's life-history yake to be investigated: Hiyo tayari iko, lazima awe achunguzwe kwanza kabla hajaupigania urais.

Radio programmes tuko nazo tulianza radio programmes za kueleza hii Katiba, kila Jumapili saa sita mpaka saa nane nafikiri, kwa Kiingereza saa nane mpaka saa kumi kwenye KBC ni Kiswahili. Hiyo itaendelea mpaka katiba hii itakapopitishwa . Kwa hivyo msikize KBC Jumapili vikoo vipindi viwili kimoja cha Kiingereza, kimoja cha Kiswahili, masaa mawili mawili. Mnaruhusiwa kupiga simu kuuliza maswali.

Pension, alisema pension ya Rais Moi ipunguzwe. Hiyo siwezi kuingilia kwa sasa na wale wengine watakaokuja pension zao zianguliwe, hapo ndio naweza nikasema kwamba tutaangalia mambo hayo lakini hii ya sasa iko moto sana siwezi kuigusa.

Japheth Muramba alikuwa ameeleza habari ya death penalty, tumesema tumeondoa urithi, umesema kwanza kwamba inachukua muda mrefu kweli. Tunataka procedure zipunguzwe pale ili iwe rahisi kupata kwa yule marehemu. Halafu ulikuwa unasema kuna bibi come –we – stay ambaye nimezaa naye watoto lakini hukumwoa. Sasa kuna mambo mara mbili pale. Kuna watu ambao watadai uridhi mara mbili kwa mfano umefariki. Kuna watoto ambao umewazaa na yule bibi na yule bibi hukumuoa halafu kuna huyu bibi mwenyewe sasa anakuja ku-claim kwamba hata mimi pia nilikuwa kwenye msururo huo, na anataka chake. Kwa hivyo upande wa watoto tumesema watoto wote wana haki ya kurithi. Hao watoto wako safe. Sasa upande wa bibi huyo ndio hatukuweka, sasa hapo itategemea dini yako, na mila yako lakini sisi lengo letu lilikuwa ni wale watoto.

Edward, bei zinapanda kila sasa nafikiri tukisharegularise zile agricultural section mambo hatapunguka

Halafu Moi anapinga Katiba ya sasa; hiyo sina uwezo wa kujibu.

Mbunge kama hafanyi kazi tumesema ni 30% ya wale waliompigia kura, wananchi wa area ile au hata councilor pia wanaandika

petition, wanatia sahihi wanamtoa.

Lease ya shamba, mmoja amesema iwe miaka arobaini, hiyo nisawa.

Qualifications za village government hatukuweka, tumesema iwe form 4, lakini tumeshaweka pale kwamba wale viongozi wa districts ambao wataunda lile bunge la district watachaguliwa moja kwa moja na wananchi, pamoja na yule district governor wao.

Hapo tumemaliza maswala yote tumeyajibu natumaini mmetupatia mengi sana kama tulivyosema katika sheria yetu sisi sio miungu tunajua kwamba hatuko kamili tunajua kwamba kuna mambo mengine ambayo lazima hatukuyapata vizuri, mengine tumeyaacha kwa hivyo hii imetupatia msaada mkubwa tukirudi Nairobi tutakwenda tuyajadili haya na hakika tutaingiza hapa. Kama kuna mtu ana a very burning question, very very burning, sasa haiwezi kuwa watu wote wana burning question. Unaona wamezidi kumi. Haya sasa nitatoa yule ambaye hajasema. Tafadhalini. Yes huyu bwana hapa, wewe waangalia nyuma, wewe njoo, mama njoo hapa. Ukisema hatutatoka hapa, nakwambia kwamba mimi nmekuja kuwaletea kirasmi hapa lakin district co-ordinator, sheria inamwambia afanye miadhara mingi zaidi na wananchi wa Malindi ambapo mtatoa maoni yenu zaidi.

Hii leo sio mwisho, hapo mnielewe vizuri; hapo sikuwa nimesema. Baada ya mimi kuondoka hapa, Bw. Kingi anatakiwa kulingana na sheria kufanya mikutano zaidi ambapo mtajadili haya maswala halafu atuletee kule. District Coordinator yuko hapa? Kingi. Yuko hapa nje. Hebu kamwite aje wamwone hawa. Huyo ndiye mtu wa Katiba hapa. District Co-ordinator tumefanya naye kazi zaidi ya mwaka mmoja ambao hawamjui pengine hawahudhurii mikutano yetu ya Katiba. Wewe ulikuwa umeongea mwanzo wewe. Nawapatia nafasi wale hawajaongea. Mwache mama.

**Bi. Nasat:** Kitu ambacho ningetaka kupendekeza ni kuhusu hawa Members of Parliament. Wao kama kwamba inajulikana wanafanya kazi kwa muda fulani, miaka mitano. Ikiwa nchi yetu itaendelea kila anayetupwa nje aende on pension sidhani economy ya nchi hii inaweza ku-afford. Pendekezo langu ni wawe on gratuity, after 5 years wapewe gratuity yao na waende zao. Ya. No pension at all.

Jambo la pili ni kwenye prastatals. Mpaka hivi sasa parastatals hawajadeclare financial statements zao. Sijui wanafanya vipi. Na baadaye tunakuta kwamba hata zile public funds ambazo wanacollect; Pay As You Earn, NSSF and NHIF hawazipeleki, zinaliwa. Kwa hivyo na wao pia waonyeshe financial statements zao.

Kwa upande wa wafanyakazi, wanaoumia zaidi ni wale wako employed by junior companies, ordinary companies na business people. Nafikiri sheria ingeangaliwa pia kuwe na some type of employment rights na ziwe publicised, mwananchi akiandikwa kazi ajue haki yake ni nini na ziwe in public ili waweze kujua kudai haki zao wanaponyimwa.

Nafikiri pendekezo ambalo lilitajwa hapa ni kuhusu hawa ambao wamenyonya damu ya Kenya wakatoa pesa nje. Pendekezo ilikuwa warudishe na wa-reinvest, lakini mimi naona kwamba si ministers peke yao, hii inahusu hata very senior civil servants na wale ambao wamenyanyasa zaidi mbali wamepewa mishahara mikubwa. Zaidi na hao, Kenya Revenue Authority wanapokwenda wanaenda kwa miguu ku-report duty na wakitoka baada ya mwaka wana Mercedez. Hawa nao vijijini waanze kuchunguzwa because tunajua vile wanavyofanya.

Jambo ambalo naona ni muhimu ni political aspirants. Tukifuata jirani nchi ya Uganda tunapata kwamba mapolitical aspirant anatakiwa atangaze C.V. yake, iwe public. Ajulikane yeye ni nani, education yake, anaweza kufanya nini katika nchi hii. Ile C.V iwe public ili kila mmoja anapomchagua anajua anachagua mtu gani.

Lakini kitu muhimu wananchi mwende mkatangazie ndugu zetu msinunuliwe na kanga, na chupa ya pombe. Tuchague watu watakao tutumikia. Ahsante.

**Bw. Kapombe**: Kwa majina ni Samuel Kapombe. Mimi nilikuwa nataka kuzungumzia tu hili jambo la kumiliki ardhi. Hii Katiba haikutwelezea kwamba kumiliki ardhi. Nafikiri sheria ingeweka kiwango cha kwamba kila mkenya ana uhuru wa kupata ardhi acre fulani. Kwa sababu kunao matajiri na kuna watu ambao wamefanya kama ni biashara ya kwamba anashika ardhi hapa, anauza, anasikia pahali pengine kuna ardhi anapata ananunua anauza tena. Ingekuwa kuna kiwango maalum cha kwamba kila Mkenya amiliki ardhi kiasi fulani, Na wale ambao watamiliki ardhi zaidi ya vile ambavyo inatakikana na sheria awe labda ni kwa sababu ni mfanyibiashara na ataajiri watu.

Halafu lingine ni kuhusu hizi national holidays. Naona kwamba Rais akichaguliwa anaweka siku yake kama ya kitaifa. Serikali inatumia pesa nyingi kwa kusherehekea siku zile. Na kama itaendelea namna hiyo unakuta kwamba hata hizi siku ambazo zitakuwa zote za kusherehekea-hakuna kazi tutafanya. Kwa hivyo sheria ingewekwa kwamba kutakuwa na taratibu za kuangalia zile siku ambazo ni muhimu na zisherehekewe. Samanani ni vile labda sikuwa nimeingia wakati huo.

Jambo lingine ni kuhusu hawa wawekaji rasli mali. Sisi tunakosa kazi mahotelini kwa sababu Waitaliano wamejenga nyumba zao za private wageni wanaotoka kule wanakuja karibu wageni thelathini, arobaini anasema hii ni family yangu. Sasa tunangojea wageni waje hotelini tuendelee na kazi. Wageni hakuna lakini ukiangalia, Malindi imejaa wageni. Kwa hivyo hawa wawekaji rasilmali wangechunguzwa na zile nyumba zao na zile pesa wanapata, iwe kama ni mtu ana nyumba, familia ni ya watu watatu au wanne- tunajua familia za Wazungu vile zilivyo, hawana zaidi ya watu arobaini au thelathini. Ile wanafanya hapa ni biashara ambayo inaikosesha pia pesa kwa serikali.

Jambo lingine; upande wa polisi- idara ya Traffic iwe ni requirement ya Katiba kwamba hizi sheria za barabarani pengine kama kwa mfano ni mwenye biashara ya matatu au basi awe haruhusiwi kabia kisheria kubeba watu zaidi ya vile inatakikana ili hata yule Mkenya wa kawaida wakati anapoona vile awe anaweza kumshtaki, na ushahidi ukipatikana kama ni kotini awe anaweza

kuchukuliwa hatua.

Mwisho ni upande wa baharini. Sisi tuko katika mkoa wa bahari. Watu wengi, vijana wengi wanavua samaki kule baharini lakini tunaona hii idara ya Marine ama Fisheries wanalinda karibu kila eneo halafu tunakosa kule kwa kuvua. Wale watu ambao wana uwezo, wageni kutoka Tanzania ndio wanakuja wanavua. Wakiulizwa huwa wamepata licence halafu ukimfuatafuata utaona kwamba hao wanatakikana hata kama ni kuvua wavue kule ambapo ni deep sea ili sisi ambao hatuna uwezo tuweze kuvua. Sasa hawa watu wa Marine badala ya kulinda lile eneo ambalo wame-demarcate ambalo ni eneo lao wanalinda mpaka zile sehemu nyingine. Sasa kila mara ni kufukuza watu, kukimbia huku na kule. Kwa hivyo naona sheria hapo haijaangalia pia. Ahsanteni.

**Bw. Tunje:** Ahsante sana kwa kupata nafasi hii. Kwa majina naitwa Salim Tambo kutoka Watamu. Mengi niliyokuwa nataka kuzungumza ashagusia tayari huyu mwenzangu. Lakini imenibidi nije hapa pia mimi niseme kwa sababu naishi karibu na utuo wa bahari, tuseme shamba yangu iko baharini. Lakini shida ambayo niko nayo ni kwamba watu wa Marine saa zote wananinyanyasa. Mimi mwenyewe nina kibanda changu nimefanya kama café nalipa ushuru kwa munisipaa. Halafu huko beach, hiyo shamba yangu imeenda mpaka beach. Wageni wakitaka kula chakula kwa mfano niwawekee hapo beach, wanataka nilipe dola thelathini na tano kwa kichwa kimoja na mimi hubidi nimlipe mtu wa Marine dola thelathini na tano ambapo pale mahali ni natural nichunge ile miti kwa sababu ni ufuo wa bahari. Ni shamba langu nikatengeneza vizuri, vile vivuli nikavichunga kwa muda mrefu, pamekuwa mahari pazuri na pia si kwamba nimeweka meza au nini. Yale madau ya wavuvi yale yameisha ndio huweka kama meza ama viti lakini wageni wenyewe wanafurahia kula chakula pale, na kule nami kibanda changu nalipa. Inanibidi mimi nilipe dola thelathini na tano kwa kila kichwa cha mtu. Just imagine mgeni mwenyewe mimi humlipisha shilingi mia mbili nao wanataka mimi nilipe dola thelathini na tano kwa kichwa kimoja. Naomba katika Katiba mjaribu kutulinda kwa sababu hii serikali iliyoko naona sasa inatumeza kabisa.

Natamani nikirudi nitapata hiyo shamba- na nikiangalia ni haki yangu - lakini sasa hivi inashinda, gharama zinanishinda kwa sababu mgeni baada ya kwamba amesema nimtengenezea maharagwe na samaki wa kuchoma na mkate lakini anataka ale pale beach, basi kila siku mimi huwa nachunguzwa. Kuna warden fulani ambaye huwa ananichunguza pale. Yeye akija badala ya kwamba aangalie mambo ya marine kule watu wasivue na net ambazo hazitakikani na kuangalia watu wanaotumia sumu kuvua samaki ameshakuwa mimi ni kidonda sasa yeye ni nzi. Yeye ataningonja mpaka nikiona mgeni atakuja kule chini, ni lazima mimi nilipe thirty five dollars. Naomba tafadhali katiba itusaidie.

Ingine nauliza hivi, kwa nini sisi tunaotaka kusimama -katika hii Katiba, kwa nini mtu hawezi kujitolea- yeye mwenyewe tayari akaomba kwamba wananchi wampigie kura bila chama chochote. Iko eh! Ahsante sana. Nimeshukuru.

**Bw. Wanyama:** Kwa majina mimi naitwa Osman Wanyama. Ninapenda katiba yetu mpya hii iangalie sana kwa sababu ukiangalia Kenya hii kuna vijana wengi ambao wamesoma kweli lakini hawana kazi.

Upande wa sector ya security- watchman. Sijui Katiba yetu hii, sijasikia kipengele ambacho kinalinda maslahi ya watchman Kenya nzima, kwa sababu hao ni vijana. Zamani ilikuwa kazi ya wazee lakini kwa vile upungufu wa kazi hapa Kenya vijana wakajiunga na hii sector na wanafanya kazi muhimu sana kulinda usalama na mali ya Kenya. Lakini utapata kuona huyu watchman anakatwakatwa anakufa na hali kadhalika hawezi kulipwa chochote. Anaambiwa kuwa yeye ndiye amefanya hiyo kuleta wakora.

Jambo lingine ni kuhusu hii mishahara ya watchmen. Hawa matajiri ambao wanaajiri hawa vijana wanaongea na client halafu wanapata pesa nyingi kule na hali kadhalika hawa watchmen wenyewe hawalipwi, wanalipwa elfu moja mia tano au elfu mbili, na mtu ana family ya kutosha. Je, Katiba yetu hii itatuangalia vipi hapo? Sina memgi ni hayo.

**Bw. Kyalo:** Kwa jina naitwa Samuel. Nataka kujua ni vipi hii Constitution mapya imesetiwa for the new government, na how ita-eradicate poverty. Maanake ukichunguza vizuri sana utaona kwamba umaskini ndio unaeneza mambo mengi tuseme kama hii social immorality kama umalaya, tuseme hii mambo ya taushoga hivi. Kutokuwa na pato fulani utakuta mtu analazimika kutenda mambo yale ya kigaidi kwa sababu hana pato ama hana kitu cha kufanya. Utakuta amelazimika kufanya kile hataki kwa sababu ya ule umaskini. Kwa hivyo ningeomba kama serikali ama Constitution mpya ina-set strategies ambazo zitaweza ku-create job opportunities or maybe a way everybody is earning in a way such that huko idle na hutalazimika kufanya vile. Kwa hivyo naomba hiyo Constitution mpya iangalie.

**Bw. Simiyu:** Ahsante sana. Kwa majina naitwa Wafula Simiyu. Yangu kwanza ningependa kuunga mkono kwa dhati kazi ambayo imefanyika na Constitutional of Kenya Review, nikipinga hatua ya majudge wawili kwenda kotini kutaka kazi iliyofanyika na watu milioni thelathini na moja ibadilishwe. Kwa hivyo endapo watataka kuendelea ningeomba watayarishe mahakama ambayo itaweza kutoshea sisi Wakenya million thelathini na moja tukae na tujibu mashtaka.

Ya pili naomba katika Katiba mpya iwe sawa sawa na vile inavyofanyika nchi ya Amerika. Tuwe na haki ya kupiga kura ya maoni kama raia wa Kenya. Kwa sababu vile tunataka kuzungukwa na hao wawili huenda hata wengine wakatuzunguka kupitia criteria ambazo mnasema university, form 4 baadaye kupata vyeti vya kuwawezesha kuwa Wabunge.

Ya tatu ningependa pesa za NSSF na NHIF ambazo sasa zinachezewa machoni petu sisi wafanyikazi wenyewe sheria iwekwe ya kulinda hizi pesa. Kwa sababu sisi wafanyikazi tunakatwa hizi pesa lihali hatuna nafasi hata ya kusema lolote juu ya ofisa wa NSSF anayejiita trustee na ambaye sasa hizi tumwite frauder. He is a frauder! Kwa hivyo kuundwe kamati ya wafanyikazi - sisi wenyewe -ambao tutakuwa karibu na hicho kituo cha trustee kuhakikisha ni tajiri gani ame-remit dues za wafanyikazi, na nani haku-remit and for what reason. Kwa hivyo tunaona manyumba yanazidi kuanguka ya maofisa na sisi wafanyikazi tunarudi nyumbani kitupu.

Lingine ningependa Kenya Wages Council ihakikishe kazi inayofanya inatekelezwa na ofisi ya labour, Kenya Wages Council

Tatu ningependa kwa labour disputes processing, kuwekwe sheria ambayo itakubalia serikali kutenga kiasi fulani cha pesa kutoka kwa hazina ya NSSF ya kulipia waathirika ama watakaotafutwa kazi mapema baada ya kuhakikisha kwamba kulingana na taratibu za labour disputes hii dispute itafaulu. Halafu baadaye tajiri anapolipa hizi pesa ziregeshwe katika hazina ya NSSF. Na ofisa wa labour atakayehusika na ile kesi endapo amekosea kwa sababu ya ulafi wake amepoteza pesa za mfanyikazi kwa sababu amehongwa kwa sababu ya personal weaknesses, huyu ofisa mshahara wake uwe attached ili pesa ziregeshwe katika hazina ya NSSF.

La mwisho ningependekeza kuwe na free medical services. Maanake tangu hapo nyuma tulikuwa tunapata matibabu ya bure lakini kulipoingia waziri ambaye mnanjua nyinyi Wakenya akatumia hasira zake baada ya kuwa amepoteza cheo fulani katika serikali, akatuegemeza mzigo wa cost sharing. Kwa hivyo cost sharing iondolewe kwa sababu ushuru tunaolipa kupitia mauzo unatosha kulipa madawa. Haina haja sisi tutozwe mzigo mzito ilihali VAT inatuumiza.

**Bw. Maro:** Jina ni Juma Maro. Mimi nauliza kuhusu vitambulisho. Kitambulisho unakata bure, sawa. Na wakati kwa bahati mbaya mfano kimepotea ukienda unaambiwa ni pesa, sijui ni kwa nini.

**Bw. Mwamure:** Mimi kwa majina naitwa Joseph Mwamure na ningetaka kutoa maoni yangu kuhusu commissioners ambao mmetengeneza Katiba. Mmesahau kuhusu watu wabaya ambao ni wachawi ambao wanaharibu kabisa maendeleo katika Pwani. Kwa hivyo ningeomba kipengele ambacho kitaonyesha wachawi- kama hamtambui wachawi basi ni nyinyi, huko mashambani. Na Katiba yetu itengenezwe kulingana na utamaduni wetu. Kwa hivyo uchawi ni kitu ambacho kinarudisha nyuma maendeleo, haiko kabisa katika hiyo Katiba.

Pili kuhusu uhuru wa kuabudu. Mmeandika uhuru wa kuabudu katika ile Katiba lakini ningeongezaa mstari fulani; uhuru wa kuabudu na kutoingiliana. Ukiangalia kuna watu wengine wanasema Yesu hakuzaliwa, Yesu hakuwa mtoto wa Mungu. Sasa hiyo ni kuingilia dini ya wengine, kwa hivyo kuna ugombano kati ya Wakristo na Waislamu. Ikiwa kutakuwa na kipengele hicho hakuna dini ambayo itaweza kuingiliana katikati na mambo yataendelea vizuri. Kwa hivyo kuwe na uhuru wa kuabudu na kutoingiliana katika dini. Ahsante.

**Bw. Katana:** Hamjambo wananchi: Kwa majina naitwa William Katana. Mfanyakazi tu raia mwenzenu hapa. Ninatoa yangu kuhusu mapendekezo. Maoni yangu ni kwamba hizi district labour offices ambazo zinahudumia wananchi hapa ikiwa kutakuwa na taratibu za ili kwamba tusiweze kuwa na wale maafisa wasonge watu kwa sababu ya haki zetu ichukuliwe. Naomba katiba iwe hivyo.

**Bw. Mutwiwa:** Ahsante Mwakilishi wa Commission ya Katiba yetu ya Kenya, na kikundi chako. Kwa majina naitwa James

Mutwiwa. Mimi ningependa kuongea kuhusu mambo ya housing – manyumba. Nimeona kwamba katika Draft Katiba kwamba hilo jambo halikuangaliwa kwa urefu na kuna shida ambayo ni kubwa sana kwa sababu kila Mkenya, kila mtu aliyehapa akitoka hapa atahitaji kwenda kulala mahali. Na ile nyumba itakuwa imejengwa na mtu aende akalale ndani yake. Kwa hivyo kuna mambo ya mpangaji na mwenye nyumba ambaye hamkuzungumzia. Kwa sababu mmsema mambo ya eviction - mtu asitolewe kwa nyumba pasipokuwa na court order. Mimi ni mshuhuda kwamba watu wanatolewa wanakuwa evicted bila ya court order. Hata hivyo sasa ni mweke msingi kamili kwa sababu pia ile procedure huwa saa zingine inakatwa. Hata sasa katika Katiba iko lakini sasa kuna shida katika hiyo hali ya mgongano. Mwenye nyumba pia hajalindwa. Mpangaji amelindwa sana kuliko mwenye nyumba. Sasa unakuta saa zingine mwenye nyumba hana pahali pa kusimamia kisheria akajitetea. Umekuta tumeangalia mpangaji sana tumemwacha mwenye nyumba. Halafu kuna ma-agent ambao wanaingia katikati. Sasa unakuta ile sheria naomba ifafanuliwe, tutaandika halafu tutume maoni kwa urefu.

Ile kitu ingine ningependa kuzungumzia na kupongeza Commission hii ya Katiba na sana sio nyinyi wananchi wa Kenya waliotoa yale maoni ni kwamba hii mambo ya Review ifanywe. Kuhusu hii makoti ya Kenya, majudge, magistrates na nini, hii kitu lazima ifanywe kwa maana koti zetu zimeharibika. Si Professor Ghai na kikundi chake walisema haya mambo ni sisi wananchi. Kwa maana kitu cha kwanza mimi nimefanya kesi zaidi ya miaka kumi na mbili. Kotini uingie iwe mimi nitakaa na lawyer wangu nitaketi na magistrate na prosecutor isemekane wewe fulani sasa tafuta kitu ndio uletee mzee ndio tuone vile kesi yako itaenda. Kwa hivyo ndio nasema na nazidi kusema kwamba mpaka hii mambo iangaliwe kwa undani zaidi kwamba hata itawezekana wakati mnatakikana ku-reapply kwamba hata names ziwe published tutoe our own comments and Kenyans kuhusu fulani. How do we know so and so as a magistrate or as a judge of the High Court? Tunamjuaje, we have information wa can give. Kwa hivyo hiyo mambo iangaliwe.

Hii mambo ya investment ambao kidogo uliigusia na ukajibu nadhani kuna undani. Si mambo ya pesa kuibiwa. Unaona kwa mfano unaona these hotels zimesimama hapa zimejengwa, lakini zile title deeds za hizi mahoteli zitawekwa kwa banks overdraft. Kwa hivyo hakuna pesa inayoingia Kenya. Wale wageni wanalipa every money kwao. Wakilipa zile pesa kule there is no money coming in. Mimi nimefanya kama accountant. Sasa zile pesa wakati wageni wamefly Kenya wameingia kwenye hoteli zile pesa zote ziliachwa Germany. Sasa wakiingia hapo ile pesa wanayo ni ya kunua sanamu, kuchanga wanunue kinywanji. Pesa yote imeingia kule. Kama mimi nataka kufanya payment ilikuwa lazima nifanye budget 2 months ndio pesa iwe released from Germany ije Mombasa in another bank halafu iwe transferred to Malindi. Sasa unakuta hata tax tunakosa. We are not getting anything actually out of that na on top of that hao watu wameweka hizo title deeds kwa overdraft. Unakuta zile accounts they are running on overdraft. We are not doing anything. Kwa hivyo hiyo ninaomba kwamba Katiba yetu ijaribu kulinda kwa sababu utakuta kwamba ukisema Malindi tuna tourists lakini you find that we are not doing anything. People are suffering. Hizi investments hazifaidi Mkenya. Kwa hivyo hiyo mambo pia naomba iangaliwe. Kwa hivyo nadhani mambo mengine tutaandika halafu tutoe kwa Coordinator. Thank you.

**Bw. Katana:** Mimi nataka kutoa mapendekezo moja kwa moja ili kuokoa wakati. Kuna agricultural economy-uchumi wa

mashambani. Hapo kabla ya uhuru kulikuwa na sub-ginneries kila baada ya 5 km. Na halafu seedlings za pamba zilikuwa zinadistributiwa kwa wakulima, wakiimwizwa kuwa pamba ni mali. Pamba ilikuwa ikilimwa sana na hizo sub-ginneries zikinunua halafu zikinunua halafu zaletwa katika main ginnery. Ule uchumi wa mashambani ulikuwa unaendelea vizuri kwa upande wa pamba. Hivi sasa pamba hailimwi tena kwa sababu zile ginneries zilifungwa baada ya independence ikaletwa co-operative ingine.

Kulikuwa na maduka ambayo yamefungwa mashambani. Yalikuwa na licence ya kununua cereals. Mimi napendekeza yaregeshwe tena kama vile zamani. Yale maduka yaliofungwa mashambani yafunguliwe watu walikuwa wakiuza mpaka mbono. Ile agricultural economy ya mashambani irudishwe tena.

Kitu kingine napendekeza; tuna mito miwili ambayo tumebahatika nayo. Galana River na Tana River. Hiyo mito katika nchi nyinginezo huko watu wanapigana vita kwa sababu ya mito. Na hapa tuna mito tunaiacha kumininika bure, katika bahari inakuwa waste. Mito hiyo mimi napendekeza tuwaite ndugu zetu ambao wana experience ya mito kama Sudan na Egypt, engineers wale waje wapangilie. Wakati maji inafurika itengenezwe channel. Kuna semi-arid land baina ya Malindi na Garsen ambayo iko empty. Hayo maji yafanyiwe channel- ifanyiwe artificial lake hapo katikati. Yakikusanyika hapo, patafanyika settlement hapo kwa irrigation system, yaani watu watapata makao. Uchumi wa agriculture utainuka.

Pendekezo lengine la mwisho ni kuhusu habari hii ya agricultural economy. Kwa hakika hayo mashamba ya huko twaweza kuyapanga kuanzia Garsen mpaka huko kwa hiyo mito miwili. Nimemaliza.

**Bw. Katore:** Mimi kwa jina naitwa Martin Katore na natoka Malindi. Ninaregelea kwenye ule upande wa tourists. Katika wafanyikazi wa hoteli ama maprivate plots naona ya kwamba mtashughulikia vilivyo kulingana na mambo ya mishahara, isipokuwa sasa kuna kitu kimoja ambacho mishahara ile inayokuja – ama kupitia upande wa labour inakuja – ni mambo ya magrade. Kwa mtu ambaye amesomea amepata grade fulani lakini utaona katika hapa Malindi ni wengi ambao hawakusomea ile kazi ya hoteli, ni watu ambao wamejitahidi. Wamefanya kazi hapa na pale na wamepata ujuzi ule ambao ni wa kutosha, hata labda pengine hakusoma lakini anajua mambo ya lugha vizuri na ile kazi amefanya kwa miaka mingi. Sasa maoni yangu yanakuja kwa upande wa mishahara. Ichunguzwe vizuri kwa watu kama wale ambao hawakusomea zile grade kama vile inavyofanyika huko lakini huku nako lakini wana ujuzi na kuweza kupangiwa mishahara ile ambayo inatakikana.

**Bw. Menza:** Mimi kwa majina ni Julius Menza. Nataka kuchangia tu kwa swala moja na ni upande wa hii NHIF. Kusema kweli shirika hili la kiserikali tukiliangalia ni kama halifaidi mwananchi. Husema wao kwamba wanasaidia katika matibabu lakini ingelikuwa labda unapochangia pale unashughulikiwa zaidi ya malipo ya kile kitanda. Pengine tungelisema ya kwamba inafaidi lakini wenye kuchangia tunaambiwa ya kwamba inalipia tu kitanda. Sasa pendekezo langu ni kwamba shirika kama hili lifutiliwe mbali kabisa. Ikiwa mtu pengine amegonjeka, alipe mwenyewe kitanda kama ni madawa na kadhalika.

**Com. Swazuri:** Haya hilo pendekezo la mwisho hilo tulifanya kwamba NHIF inasaidia wafanya kazi. Badala ya kwamba tuifute, labda afadhali tuitengenezee sheria ya kwamba ifanye kazi vyema.

Upande wa MPs, mama amesema kwamba wapewe gratuity, hilo ni wazo nzuri.

Parastatals to declare their financial statements, hiyo ni sawa.

Rights za wafanya kazi tumezitajia tutazipanua pale.

Halafu wale wanataka kupigania kura watoe C.V zao ni wazo nzuri. Kuna wengine walisema lazima wafanye mijadala ya kitaifa. Pia tulipata maoni hayo.

Ardhi, kila Mkenya apate ardhi. Kusema hivyo tumesema kila Mkenya anayetaka kupata ardhi iwe mipango ya kuipata ardhi ile inapatikana.

Halafu hawa foreigners; nafikiri maswala mengi hapa ni kuhusu hawa wageni ambao wanatumia njia za kupata kazi na kukwepa sheria za Kenya. Kama tulivyosema sheria zipo lakini ni vile zinataka kutiliwa mkazo.

Traffic Act; tunasema wananchi waweze kuiangalia. Tumesema sasa ni jukumu la wananchi. Kama mtu amefanya makosa kumsema kwa Public Defender.

Bahari imefungwa na Kenya Marine na kadhalika; nafikiri hii ni jukumu la serikali ya mikoa na wilaya kuhakikisha kwamba mambo haya yanafunguliwa.

Halafu huyu Bwana ambaye anachargiwa dola thelathini kulisha mzungu mmoja, nafikiri hii ni kesi ambayo inataka kuangaliwa na leadership. Hayo ni maonevu ya hali ya juu sana. Sijasikia mambo kama hayo.

In guaranteeing employment, tumesema kwamba kila mwananchi ana haki ingawaje kazi zetu ndizo ambazo zimekuwa kidogo.

Watchmen haki zao tumeandika. Kama wafanyikazi wengine lazima wapate mshahara mzuri, mazingara mazuri.

Samuel; Poverty eradication hatukuitaja wazi wazi lakini imo katika Bill of Rights, labour relations, devolution of powers. Hapo pote tumetaja mambo ya poverty eradication kwa sababu serikali za chini za majimbo, za location na za wilaya tumesema kwamba ni lazima zidevelop sehemu zao, zitafutie watu maisha mazuri.

Wafula; mambo ya referendum tumesema kwamba sheria fulani zipitishwe na wananchi.

Bado kuna vita vya NSSF, NHIF. Nafikiri mashirika haya yanashida sana na sheria zao zinazidi kubadilishwa kila siku ili kuhakikisha zinafanya kazi lakini inaonekana kila mkieka sheria mpya kuna watu wanajua kuikwepa sheria ile. Kwa hivyo tutakaa chini zaidi kuhusu haya mashirika.

Salaries Board iko, tuliiunda hiyo Wages Council. Halafu mambo mengi ni ya NSSF bado.

Free health, education iko lakini hatukuiweka wazi. Tumesema kila mtu ana haki ya kupata afya bora which includes the right to health care services including reproductive health care. Hilo neno free ndilo halipo pale.

Kitambulisho tumesema ni haki, sasa kikipotea unalipa lakini kinatakiwa kiwe bure.

Wachawi; jana pia tuliulizwa swali hili tulipokuwa Kilifi.
Ni kweli nafikiri hatukuliangalia kwa hivyo hata jana tulisema tutaliangalia. Nafasi ya wachawi, huko rural areas wachawi wanadhuru watu wengi haswa huku kwetu. Huyo mtu wa jana aliuliza kuhusu watu ambao huua. Mtu anayeshukiwa kwamba ni mchawi, tuwafanye nini watu kama hao?

Uhuru wa kuabudu na kutoingiliana; hiyo tayari iko ni ile kwamba haikutaja Mwislamu na Mkristo.

William Katana; District labour offices ziwe abolished. Zitakuwa sasa ni mambo ya serikali za wilaya. Wataangalia.

Housing laws- mpangaji anafaidika kuliko mwenye nyumba hiyo ni kweli, juu ya hiyo bado watu wanang'ang'ana.

Judiciary is corrupt. Nafikiri umeeleza kila kitu ndio maana tumeandika hapa kwamba wakifika miaka sitini na tano wata-retire. Sheria hii ikipitishwa wale ambao wamezidi miaka sitini na tano wakitaka lazima wafanyiwe uchunguzi. Kama hawataki walipwe chao waende zao.

Investment: umetupa siri ambayo hata mimi sikuwa najua, title deeds ziko kwenye overdraft. Hiyo ni kweli wananchi wa Kenya hawapati pesa, hilo tulikuwa hatulijui tutaliangalia kama ni hivyo. Basi kama ni hivyo lazima kuwe na investment laws ambazo zinakuwa slorted. Maanake hiyo haiwezekani. Huwezi kurun company on overdraft. Overdraft ni kitu ambacho ni cha muda - una shida fulani sasa unaenda kwa bank manager unapewa overdraft. Maelewano ni kwamba hali yako ikiwa sawa utarudisha pale uendelee. Lakini you cannot be on overdraft permanently. Hiyo sheria ya Kenya kwanza hairuhusu lakini inakuwaje haya mahoteli makubwa makubwa hayo yanaendeshwa na overdraft. Ni hongo tena imekubalika hapo.

Agricultural economy: hiyo ni sawa kabisa lakini ni kama nilivyosema sasa ni serikali za majimbo zitakazoangalia mambo haya. Lazima whakikishe kwamba wanchi wanafanya ukulima na maendeleo. Kwa hivyo ni jukumu lao kufungua hayo maduka na sub-ginneries.

Martin ukasema kuna wafanyikazi ambao pengine hawana elimu lakini wana ujuzi na mambo yao yaangaliwe. Tumeandika haya mambo kwa hivyo wafanyakazi mambo yao yataangaliwa katika labour relations chapter 55. Tumeandika hayo.

Halafu Bw. Julius alisema kwamba NHIF tuifute. Tumesema hatuwezi kuitupa jongoo na msiki wake. Afadhali tuangalie tutengeneze vizuri, likishinda tena kabisa ndio tutaitoa.

Haya nafikiri tumeshukuru sana tumefanya kazi ya kutosha leo kwa hivyo bado mko na nafasi wananchi ya kutoa maoni yenu tena. Sisi tutaenda haya mambo mtayaona. Na halafu tutawapatia wajumbe wenu waende kwenye kikao cha kitaifa kuanzia tarehe ishirini na nane za mwezi huu kwa mwezi mzima nao pia wakachangie tena, mpaka tuhakikishe kwamba hii Katiba inareflect mawazo ya watu milioni thelathini na moja wa Kenya, ndio ipitishwe iwe ni sheria ya Kenya. Kama itafanyika na uchaguzi unaokuja au la nishasema kwamba maoni yetu ndio hivyo,lakini funguo ziko na watu wengine. Haya asanteni sana.

Bwana mmoja atuongoze kwa maombi ya Kikristo. Tuliahidi kwamba tutafungua na maombi ya kislamu sasa maombi ni ya kikristo. Unaweza kuja hapa ukatumia kipaza sauti.

**Rev. Kahindi:** Tusimame tumheshimu Mungu. Baba yetu uliyembinguni unayeishi na kutawala tunakushukuru mchana wa leo kwa vile umeleta watumishi wako ambao umechagua. Kutoka kuumba ulimwengu ulifahamu ya kwamba siku hii ya leo tutakuwa katika hall hii kwa ajili ya kuchangia matatizo inayokumba Kenya yetu. Wakati huu tumezungumza mengi na mengine hatukuyataja kamwe. Mungu uende ukaweze kuwapa ufahamu wale ambao wako nafasi hii kama mwenyekiti na kamati yake ambao wamesimama ili waweze kuyazungumza kwa urefu na kwa na kwa upana ili katika Kenya yetu tuweze kuwa na maendeleo na amani katika ushirika wetu.

Baba ni wakati ambao tumefungua mkutano huu kwa maombi na wakati huu tunaenda kuufunga. Hatufungi baraka bali tunafunga mkutano huu kwa ajili ya kwenda manyumbani. Wabariki viongozi wetu ambao tumekuwa nao na ukawasaidie hata watakaposafiri kurudi huko Nairobi maana watasafiri na vyombo vilivyoundwa na mwanadamu. Mwenyezi Mungu uende ukawasafirishe ili wakaweze kuendelea mpaka watakapofika kwa jamii zao na kazi ile watakayoifanya na ripoti ambayo wataipeleke katika kamati kuu yetu ya Kenya. Tubariki na sisi ambao tutabaki tukapoondoka hapa, angalia jamii zetu ukaweze kutusaidia.

Tunaombea hata uchanguzi unaokuja mungu tunauweka mikononi mwako. Tunahitaji kuwa na amani ili Bwana tukaweze kufanya uchanguzi wetu kwa njia ya busara. Tunaomba kwa jina la mwanao Yesu mwokozi wetu. Amen.

Meeting ended at 3.37 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**